# UWASILISHAJI WA MAUDHUI KATIKA

# HADITHI FUPI TEULE ZA SAID A. MOHAMED

**NA**

**MWENDA ELIZABETH MAKENA**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI YA KISWAHILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**2018**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa katika chuo chochote kingine kwa minajili ya kutosheleza mahitaji ya shahada ya uzamili.

**Mwenda Elizabeth Makena** **Tarehe**

Kazi hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

**Dkt. Evans M. Mbuthia** **Tarehe**

**Mwl. Mary Ndung'u** **Tarehe**

## TABARUKU

Tasnifu hii ninaitabarukia mume wangu mpendwa Bw. Stephen Kaulani, aliyetambua umuhimu wa kuelimisha mwanamke katika jamii, pamoja na watoto wangu Prudence, Beatrice, Peter na Branson.

**SHUKRANI**

Sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa hekima ya kuendeleza masomo yangu katika utu uzima wangu. Shukrani za dhati pia ni kwa wasimamizi wangu, Dkt. Evans M. Mbuthia na Ms. Mary Ndungu walionielekeza vyema na kunisaidia kujipanga ili nikamilishe kazi hii kwa wakati uliotakikana. Nawashukuru wahadhiri wote walionifundisha tangu nilipojiunga na Chuo Kikuu cha Nairobi mnamo mwaka 2015. Wahadhiri hawa ni Dkt. Evans Mbuthia, Prof. Iribemwangi, Dkt. Zaja Omboga, Dkt.Jefwa Mweri, Prof. Mwenda Mbatiah, Prof. Kineene Wa Mutiso, Prof. John Habwe, Dkt. Rayya Timammy, Dkt. Prisca Jerono na mwalimu Leonard Sanja. Walijitolea kuhakikisha ndoto yangu ya kupata shahada hii imetimia. Aidha, namshukuru Prof. Kyallo Wadi Wamitila kwa mawaidha na uelekezi wake wa kiakademia.

Shukrani zangu pia ziwaendee wahadhiri wote Idara ya Kiswahili kwa ushirikiano wao na mipangilio mwafaka kuhakikisha mafunzo yanaendelea vizuri.Kadhalika nawashukuru wanafunzi wenzangu tulioshirikiana katika masomo ya shahada ya uzamili. Baadhi yao ni Irene Kilingo, Bernice, Mbaabu,Glory, Joy, Cyrus, Barasa, Agnes, Mwaniki, Mweti na wengineo. Shukrani za kipekee nazitoa kwa Irene Kilingo kwa maelekezano na midahalo tuliyokuwa nayo kipindi chote cha masomo ya uzamili. Mawaidha yako yalinifaa sana na uwe wa manufaa kwa wengine kama ulivyokuwa kwangu.

Shukrani nyingi ninazielekeza kwa Tume ya uajiri ya walimu TSC pamoja na walimu ninaofundisha nao na marafiki wote walionitia moyo wa kuendelea na masomo.Pia ningependa kuwashukuru wazazi wangu wapendwa Bw. Henry Mwenda na Bi. Marsellah Kalayu kwa kunipa msingi bora katika elimu na motisha katika masomo yangu.Aidha nawashukuru watoto wangu wote ambao wamenivumilia kwa muda ambao sikuweza kushhirikiana nao katika mambo mengi waliponihitaji. Pia, nawashukuru Doreen Murithi na Kobia Pius waliopiga chapa kazi hii.

Mwisho nawashukuru wote waliochangia kazi hii. Ingawaje haingewezekana kuwataja nyote, nawahimiza muendelee kuwa mwanga na kielelezo bora kwa wasomi wengine kama mimi. Mungu awabariki nyote.

## IKISIRI

Kazi yetu imechunguza jinsi baadhi ya vipengele vya fani: mandhari, wahusika na mianzo na vimalizio vinavyochangiana na kukamilishana ili kuwasilisha maudhui katika hadithi fupi za Said A. Mohamed. Fani ni jinsi ambavyo msanii hufinyanga kazi yake ili msomaji apate ujumbe wake kwa njia iliyo nzuri. Kazi yetu imetumia Nadharia ya Umuundo kuchambua vipengele vya fani. Tumechunguza jinsi mwandishi ametumia mandhari katika kufanikisha uwasilishaji wa maudhui. Pia tumetathmini nafasi ya wahusika wakuu na wadogo katika kufanikisha uwasilishaji wa maudhui. Aidha, tumeangazia jinsi mwandishi alivyotumia mianzo na vimalizio vya hadithi fupi katika kufanikisha uwasilishaji wa maudhui. Kutokana na uchunguzi huu, imebainika kuwa mwandishi ametumia vipengele vya fani kukuza maudhui kwa ufundi mkubwa sana. Vipengele vyenyewe ni kama vile mandhari tofautitofauti yaliyofanikisha uwasilishaji wa maudhui. Mwandishi ametumia wahusika kiufundi katika kuupitisha ujumbe wake. Usawari wa wahusika umefanywa kiufundi ili kuafiki matarajio ya hadithi fupi.Hatimaye tumeshughulikia kipengele cha msuko na kudhibitisha kwamba msuko wa hadithi fupi huwa sahili. Tumemulika msuko wa hadithi fupi hasa kwa kuangazia uanzaji na utamatishaji wa hadithi husika. Mwandishi wa hadithi fupi zilizoteuliwa amedhihirisha ya kwamba vipengele vya fani: mandhari, wahusika na mianzo na vimalizio vya hadithi fupi vinachangiana na kukamilishana ili kufanikisha uwasilishaji wa maudhui. Tumegundua ya kwamba nadharia ya Umuundo imefaa kazi hii kwa sababu tumeona ya kwamba nadharia hii inaangazia vipengele vya kazi ya sanaa jinsi vinavyohusiana na kujengana.

## YALIYOMO

UNGAMO ..... i
TABARUKU ..... iii
SHUKRANI ..... iv
IKISIRI ..... v
YALIYOMO ..... vi

## SURA YA KWANZA

1.1Usuli wa Mada ..... 1
1.2 Tatizo la Utafiti ..... 3
1.3 Maswali ya Utafiti ..... 4
1.4 Malengo ya Utafiti ..... 4
1.5 Sababu za Kuchagua Mada ..... 4
1.6 Upeo na Mipaka ..... 5
1.7 Msingi wa Kinadharia ..... 5
1.8 Yaliyoandikwa kuhusu Mada ..... 8
1.9 Mbinu za Utafiti ..... 12
1.9.1 Uteuzi wa Sampuli ..... 12
1.9.2 Ukusanyaji wa Data ..... 13
1.9.3 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data ..... 13
1.10 Hitimisho ..... 13

## SURA YA PILI

## MANDHARI NA UWASILISHAJI WA MAUDHUI

2.1 Utangulizi ..... 15
2.2. Mandhari ya Mahali ..... 15
2.2.1 Mashambani ..... 15
2.2.2 Nyumbani ..... 20
2.2.3 Mandhari ya Danguroni ..... 25

2.3 Mandhari ya Wakati ........ 26
2.3.1 Mandhari ya Asubuhi ........ 26
2.3.2 Mandhari ya Mchana ........ 27
2.3.3 Mandhari ya Usiku ........ 27
2.4 Hitimisho ........ 31

**SURA YA TATU**

**NAFASI YA WAHUSIKA KATIKA KUFANIKISHA UWASILISHAJI WA MAUDHUI**

3.1 Utangulizi ........ 32
3.2 Wahusika Wakuu ........ 32
3.2.1 Mzee Siwa katika 'Sadiki Ukipenda' ........ 33
3.2.2. Mussa katika 'Sadiki Ukipenda' ........ 34
3.2.3 Kondo katika 'Ngondo Pangoni' ........ 36
3.2.4 Jecha katika 'Ngondo Pangoni' ........ 37
3.2.5 Subira katika 'Uhuru wa Subira' ........ 39
3.2.6 Mrisho katika 'Uhuru wa Subira' ........ 40
3.2.7 Bwana Haji katika 'Mwungwana' ........ 41
3.2.8 Saada katika 'Mwungwana' ........ 43
3.2.9 Mwanamaua katika 'Mhanga wa Mwanamaua' ........ 43
3.2.10 Dadi katika 'Mhanga wa Mwanamaua' ........ 45
3.2.11 Fumu katika 'Njia Fupi' ........ 46
3.2.12 Naima Mambo katika 'Njia fupi' ........ 47
3.3. Wahusika Wadogo ........ 48
3.3.1 Baba yake Mussa katika 'Sadiki Ukipenda' ........ 48
3.3.2 Wachawi katika 'Sadiki Ukipenda' ........ 49
3.3.3 Bi. Sihaba katika 'Ngondo Pangoni' ........ 49

3.3.4 Bi. Mwamboje katika ‘Ngondo Pangoni’ ........ 50
3.3.5 Biti Shomari katika ‘Uhuru wa Subira’ ........ 51
3.3.6 Mzee Farijala katika ‘Uhuru wa Subira’ ........ 52
3.3.7. Kibwana katika ‘Mwungwana’ ........ 52
3.3.8 Bi. Sikitu na Bwana Ali katika ‘Mwungwana’ ........ 53
3.3.9 Ng’ombe Kipelele katika ‘Mhanga wa Mwanamaua’ ........ 54
3.3.10. Wanakijiji wa Pemba katika ‘Mhanga wa Mwanamaua’ ........ 54
3.3.11 Mama Kitimbi katika ‘Njia fupi’ ........ 55
3.3.12 Makahaba katika ‘Njia fupi’ ........ 56
3.4 Hitimisho ........ 56

**SURA YA NNE**

**MIANZO NA VIMALIZIO VYA HADITHI FUPI KATIKA UWASILISHAJI WA MAUDHUI**

4.1.Utangulizi ........ 58
4.2.Uanzaji wa Hadithi Fupi katika Diwani za Said A. Mohamed ........ 58
4.2.1.Mwanzo wa Kitathmini ........ 58
4.2.2. Mwanzo wa Kirejeshi ........ 59
4.2.3.Mwanzo wa Kitaharuki ........ 60
4.2.4.Mwanzo wa Kidrama ........ 62
4.2.5.Mwanzo wa Kiishara ........ 63
4.2.6.Mwanzo wa Kimgogoro/ Kipeo ........ 64
4.3. Miisho na Utamatishaji wa Hadithi Fupi za Said A. Mohamed ........ 65
4.3.1.Mwisho wa Kikwelikinzani ........ 65
4.3.2Mwisho wa Kidhamira/ Kimotifu ........ 67
4.3.3. Mwisho wa Kiasilia au Kikawaida ........ 67

4.3.4 Mwisho wa Kitatuzi ........ 68
4.3.5Mwisho wa Kitanakuzi/ Kilinganuzi ........ 69
4.3.6.Mwisho wa Kiadili ........ 70
4.4 Hitimisho ........ 71

**SURA YA TANO**

**MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

5.1Utangulizi ........ 72
5.2 Muhtasari waMatokeo ya Utafiti ........ 72
5.3 Hitimisho ........ 77
5.4 Mapendekezo ........ 77
**MAREJELEO** ........ 79

# SURA YA KWANZA

## 1.1Usuli wa Mada

Vipengele vya fani kama vile mandhari, wahusika na mianzo na vimalizio vya hadithi fupi huwa ni muhimu sana katika kufanikisha uwasilishaji wa maudhui katika kazi za fasihi. Vipengele hivyo vya fani hutegemeana na kukamilishana vinapokuwa vinatumika. Kwa mfano, katika kuzungumzia msuko, wahusika watashirikishwa na mandhari kuzingatiwa ili kufanikisha uwasilishaji wa maudhui. Hali hii inasababisha lazima ya kuchanganua katika ujumla wake vipengele vyote wakati wa kuihakiki kazi ya fasihi ili kubainishwa mchango wa kila kipengele katika kufanikisha kazi husika. Hali si tofauti katika hadithi fupi.

Fani ni dhana muhimu katika utanzu wa hadithi fupi. Wamitila (2008) anasema kuwa fani ni jumla ya nyenzo zinazotumika kuwasilisha kazi yoyote ya fasihi. Anaongeza kwamba mawazo ya mwandishi wa kazi yoyote ya fasihi huwa katika uchi wake hadi pale fani inapotumika na kuyavisha nguo mawazo hayo ili yaweze kuwasilishika. Hivi ni kusema kwamba fani pamoja na maudhui hutegemeana na kukamilishana. Mawazo ya Wamitila yameungwa mkono na Mbatiah (2001) anaposema kuwa fani katika kazi ya fasihi hujenga kiunzi cha kubebea ujumbe na maana mahususi. Mbatiah ana maana kuwa hapatakuwa na ujumbe katika kazi ya fasihi iwapo fani itakosekana katika kazi hiyo. Hivyo basi inamlazimu msanii yeyote wa kazi ya fasihi awe mweledi katika kufinyanga nyenzo hii ya fani ili kuwasilisha kazi yake vyema. Wataalam wa fasihi kwa wakati mmoja wamefananisha uhusiano uliopa kati ya fani na vipengele vingine vya fasihi kama mfumo. Hivi kwamba mfumo huu hauwezi kukamilika pasi na sehemu zote kuwepo.

Kulingana na Wamitila (2002), msuko wa hadithi fupi huwa na mwanzo, kati na mwisho. Sehemu hizi huwa na maana kuliko tanzu nyinginezo. Katika ufunguaji wa hadithi fupi, mwandishi anadhihirisha waziwazi funzo lake katika hadithi hiyo. Sehemu hii huonyesha ufumbuzi au utatuzi wa tatizo kuu katika msuko wa hadithi fupi. Hadithi fupi inapaswa isukwe kwa namna ambayo inapofika mwisho, msomaji anahisi mkokotezo fulani au anajiwa na athari kubwa.

Hadithi fupi huwa na mianzo tofauti tofauti. Inaweza kuanza kwenye upeo, mwisho au ianze kama kawaida. Aidha, hadithi fupi huanza kwa kilele kisha ikaelekea mwisho au ikaanza mwisho kisha ielekezwe kileleni. Hadithi za aina hii huishia kwa taharuki kubwa na kumwacha msomaji na maswali mengi.

Mwisho wa hadithi fupi huwa na mkokotezo na msisitizo fulani. Pia msisitizo mkubwa huwekwa kwenye jinsi hadithi itakavyokwisha. Ikiwa msomaji ana haja ya kujua ni kitu gani kitakachotendeka, ni lazima atamani kuona mwisho wa hadithi fupi. Hivyo, mwisho wa hadithi fupi unachukua nafasi kubwa katika muundo mzima wa utanzu wenyewe (Wamitila 2002).Hadithi fupi zinaweza kuwasilisha mambo kwa njia ya moja kwa moja, kwa haraka na kwa njia bora. Pia hadithi fupi ina uwezo wa kuyaelezea mabadiliko yanayojiri katika jamii.

Hadithi fupi ni utanzu wenye historia ndefu.   Wamitila (2002) anasema kuwa msingi wa utanzu wa hadithi fupi unahusishwa kwa kiasi kikubwa na mtunzi na mhakiki wa Kimarekani anayefahamika kama Edgar Allan Poe. Kimsingi, Poe anachukuliwa kama mwasisi wa utanzu huu pamoja na mhakiki aliyefahamika kama Brander Mathews ambaye inaaminika ndiye aliyelitumia neno la Kiingereza la "Short Story" (hadithi fupi) kwa mara ya kwanza.

Kulingana na Wamitila (2002), utanzu huu umekua sana, hasa kiuchapishaji katika fasishi za lugha nyingine za Ulaya ikilinganishwa na Kiswahili. Hata hivyo, fasihi ya Kiswahili imekua sana na inazidi kupevuka. Waandishi wengi wa hadithi fupi walianza kuandika hadithi zao na kuzichapisha magazetini. Kulingana na Mbuthia (2005) hadithi nyingine zilishiriki katika mashindano ya uandishi wa hadithi fupi zilizosomwa katika idhaa za BBC na hatimaye kuchapishwa katika mifululizo ya: *Mapenzi ni Kikohozi*, *Kinywa Jumba la Maneno* na *Pavumapo Palilie*. Hatua hii ilichangia ukuaji wa utanzu huu.

Kwa sasa, kuna diwani nyingi sana za hadithi fupi ambazo zimechapishwa hasa nchini Kenya kutokana na sababu kadhaa; mojawapo ni kule kutahiniwa katika shule za upili na vyuo kufuatia somo la Kiswahili kuwa la lazima katika shule za upili na vyuo vya walimu nchini Kenya.

Diwani hizi za hadithi fupi zilichapishwa kwenye hayo magazeti ziliweka msingi wa kuandikwa na kuchapishwa kwa hadithi fupi katika siku za usoni. Diwani nyinginezo zilizochapishwa katika miaka ya sabini ni: *Pepeta* na S.S. Yahya, *Zaka la Damu na Hadithi Nyingine*, *Parapanda na Hadithi Nyingine* na *Uwike Usiwike Kutakucha* za G. Ruhumbika, *Si Wazimu Si Shetani* (S.A. Mohamed), *Dhuluma na Hadithi Nyingine* (Y. Barshad), *Twen'zetu Ulaya na Hadithi Nyingine* (F. Macha), *Tamaa Mbele na Hadithi Nyingine* na *Nipe Nikupe na Hadithi Nyingine* (A. Banzil), *Nitakuja kwa Siri* (M. Msokile), *Hapa na Pale* (*Jamila Mpenzi na Hadithi Nyingine* (F.E.M.K. Senkoro) na *Papa la Mji* (J. Rutayisingwa). Hizi ni baadhi ya hadithi fupi zilizochapishwa katika miaka ya themanini.

### 1.2 Tatizo la Utafiti

Utafiti huu ulichunguza jinsi baadhi ya vipengele vya fani: mandhari, wahusika na mianzo na vimalizio vimetumika ili kufanikisha uwasilishaji wa maudhui katika hadithi fupi za Said A. Mohamed: *Sadiki Ukipenda na Hadithi Nyingine*, (2002), *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine,* (2005), na *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine*, (2005). Vipengele vya fani ni vingi lakini tunashughulikia hivi vitatu katika kazi yetu.

Uwasilishaji wa maudhui hutegemea jinsi vipengele mbalimbali vya fani huwa vimetumika ili kuwasilisha ujumbe unaodhamiriwa. Maudhui na fani haviwezi kutenganishwa katika kazi ya fasihi, vyote hutegemeana ili kuwasilisha maana kamilifu. Kila mwandishi ana uhuru wa kutumia vipengele vya fani kama atakavyo. Jambo hili hufanya kazi ya kifasihi kuwa tofauti kutoka msanii mmoja hadi mwingine. Pia, tofauti za kitanzu huwafanya waandishi kutumia mitindo inayofaa kwa kutegemea utanzu husika.

Totauti na tanzu nyingine za kiufasihi kama vile riwaya na tamthilia, utanzu wa hadithi fupi humfunga mwandishi na kumfanya kutumia vipengele vya fani kwa njia mahsusi. Tumedhihirisha namna Said Ahmed anavyotumia ufundi wake katika muktadha wa hadithi fupi.

### 1.3 Maswali ya Utafiti

Utafiti wetu utaongozwa na maswali yafuatayo:

i. Je, mandhari imetumika vipi ili kufanikisha uwasilishaji wa maudhui katika kazi teule za Said A Mohamed?
ii. Je, wahusika wakuu na wadogo wana mchango upi katika kufanikisha uwasilishaji wa maudhui katika diwani zilizoteuliwa za Said A. Mohamed?
iii. Je, mianzo na vimalizio vimetumika vipi katika kufanikisha uwasilishaji wa maudhui katika diwani zilizoteuliwa za Said A. Mohamed?

### 1.4 Malengo ya Utafiti

Malengo ya utafiti huu ni:

i. Kutathmini namna mandhari yametumika ili kufanikisha uwasilishaji wa maudhui katika kazi teule za Said A Mohamed.
ii. Kutathmini mchango wa wahusika wakuu na wadogo katika kufanikisha uwasilishaji wa maudhui katika diwani za hadithi fupi zilizoteuliwa za Said A. Mohamed.
iii. Kutathmini jinsimianzo na vimaliziovilivyotumika ili kufanikisha uwasilishaji wa maudhui katika diwani za hadithi fupi zilizoteuliwa za Said A. Mohamed.

### 1.5 Sababu za Kuchagua Mada

Hadithi fupi huwa na sifa za kipekee na ambazo huutofautisha utanzu huu na tanzu nyingine kama vile riwaya.  Mojawapo wa sifa hizo ni mandhari. Mandhari katika hadithi fupi huwa ni finyu; hayahamihami na kubadilika. Isitoshe, kuna ufupi wa yaliyomo kutokana na kwamba ni kipengele kimoja tu katika maisha ya mhusika mkuu ndicho kinamulikwa. Kuna pia sifa ya uchache wa wahusika kutokana na sababu tuliyoitoa. Sifa hizo za hadithi fupi zilichochea hamu yetu ya kutaka kuchunguza vipengele vilivyoteuliwa ili kubainisha mchango wake katika ufanikishaji wa uandishi wa hadithi fupi kimaudhui kupitia fani.

Hadi sasa, hakuna ushahidi wowote unaothibitisha ya kuwa kuna uhakiki wowote wa kina uliofanyiwa kuhusu diwani za Said A. Mohamed kuhusiana na vipengele vya mandhari, wahusika na mianzo na vimalizio vya hadithi fupi;namna vinavyochangiana na kukamilishana ili kuwasilisha maudhui. Utafiti wetu utalenga kuliziba pengo hilo.

## 1.6 Upeo na Mipaka

Utafiti huu ulishughulikia baadhi ya hadithi katika diwani zifuatazo za hadithi fupi: *Sadiki Ukipenda na Hadithi Nyingine, (2002), Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine, (2005) na Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingin*e (2005). Mtafiti amemulika namna mandhari, wahusika na mianzo na vimalizio vimetumika katika uwasilishaji wa maudhui katika hadithi fupi za Said A. Mohamed. Utafiti huu haukuchunguza hadithi zote katika diwani zilizotajwa kwani ulihitaji baadhi tu ili kudhihirisha vipengele vilivyolengwa. Hadithi zilizoteuliwa kwa hivyo ni zile zilizotekeleza lengo la utafiti.

Mtafiti ameteua hadithi fupi sita zifuatazo: 'Sadiki Ukipenda', 'Ngondo Pangoni', 'Uhuru wa Subira', 'Mwungwana', 'Mhanga wa Mwamamaua' na 'Njia fupi'. Mtafiti ameongozwa na haja ya kupata hadithi ambazo zinatofautiana kiuwasilishaji ili kuamua zile atakazoziteua.

## 1.7 Msingi wa Kinadharia

Utafiti huu umeongozwa na Nadharia ya Umuundo ambayo iliwekewa msingi na mawazo ya De Saussure (1957). Hata kama uwanja wake ulikuwa wa Isimu, mawazo yake pia yanatumika katika utafiti wa nyanja nyingine kama vile fasihi na anthropolojia. De Saussure alibuni dhana za *Langage*, *Langue* na *Parole*. Anaeleza dhana ya *Langage* cha usemi ambacho kila binadamu asiye na upungufu wa kusema huwa nacho. Kwa hivyo dhana ya 'Langage' inasimamia lugha zote na kwa hivyo, tunaweza kuchukulia *'Langage'* kama fasihi zote za Kilimwengu. *Langue* ni mfumo dhahania wa lugha fulani ambao hutumiwa na jamii fulani. Kwa hivyo, lugha huchukuliwa kama mfumo changamano, ambao ndani yake kuna mifumo tofauti kama vile fonolojia, sintaksia, semantiki na mofolojia. Mifumo hii huhusiana na kukamilishana kama vilivyo vipengele vya fani na maudhui katika fasihi. Hawkes, (1977:20) anaeleza tofauti kati ya *Langue na Parole* kwa kuonyesha '*Langue'* kama mfumo wa Lugha na 'Parole' kama ubainikaji wa mfumo – Lugha katika usemi; vipengele hivi viwili ndivyo muhimu katika utafiti wetu. Kwa mfano *Langue* na *Parole* zinaweza kutumika katika uchanganuzi wa data katika utafiti huu. Hii ni kwa sababu muundo wa fasihi una vipengele vinavyoelezwa katika muktadha wa vipengele vingine. Kwa mfano jinsi mandhari, wahusika na mianzo na

vimalizio vya hadithi fupi vinachangiana na kukamilishana katika kufanikisha uwasilishaji wa maudhui.

Kulingana na mawazo ya De Saussure fasihi inastahili kuchunguzwa kama muundo mmoja uliojengwa kwa vipengele tofauti vinavyoshirikiana kukiunda kitu kizima. Kwa mujibu wa kazi yetu tutaangalia uwasilishaji wa maudhui katika hadithi fupi zilizoteuliwa za Said A. Mohamed kwa kumlika mandhari, wahusika na mianzo na vimalizio vya hadithi mbalimbali.

Nadharia ya Umuundo huchunguza vipengele mbalimbali vya mfumo wa fasihi kwa kuchunguza jinsi vinavyohusiana katika kukamilisha kazi husika. Hili limetokana na mawazo ya De Saussure ya kupinga kuchanganua lugha kwa kuangalia kiungo kimoja kimoja bila kuhusisha viungo mbalimbali. Kwa mfano, hadithi fupi ina viambajengo kama vile vya wahusika, mandhari, msuko na matumizi ya lugha vyote katika mfumo mmoja wa yaliyomo.

Nadharia ya Umuundo iliendelezwa na akina Roman Jakobson, Vikta Sklovij, Juri Tynjanov na wengine, mwaka wa 1920. Walikuwa ni wanaisimu katika Shule ya Isimu ya Prague nchini Urusi. Shule ya Prague ilishughulikia uchunguzi wa Lugha Kiisimu (Wamitila 2002). Walihusika sana na kazi maalum za kifasihi wala sio chimbuko wala athari zake kwa wanaohakiki fasihi. Hamu kuu ya wananadharia hawa ilikuwa kubainisha sifa za kuitambulisha fasihi na kuweka mipaka kati ya fasihi na taaluma tofauti kama saikolojia, wasifu, historia na taaluma nyinginezo. Waasisi hawa walisisitiza kuwa uandishi wa kibunifu unaotambulishwa na msisitizo wa njia za uwasilishaji. Wanaisimu hawa wanasema kuwa fasihi inajinasibisha na vitu ambavyo vinakuwa vya kawaida au kidesturi katika maisha yetu na kuvifanya vionekane kama vya kigeni.

Nadharia hii pia inashikilia kwamba vipengele mbalimbali vya lugha haviwezi kutenganishwa ili kuleta maana. Muundo mzima wa lugha huchunguzwa ili kuibua maana kamili. Mawazo haya yanatiliwa mkazo na Scholes, (1974); Hawkes, (1977); na Culler, (2003), wanapolinganisha muundo wa lugha katika kazi ya fasihi na umbo la dunia lisiloweza kugawika kwa kusema kwamba, dunia ni umbo lisiloweza kugawika. Ni

umbo linalopaswa kufikiriwa kijumla. Hivyo hata muundo wa lugha katika kazi ya fasihi unastahili kuchunguzwa kwa pamoja ili kuibua maana, (Wafula na Njogu, 2007).

Kwa mujibu wa nadharia hii ujumbe fulani unaweza kufafanuliwa kwa njia nyingi kulingana na jinsi lugha imetumika. Lugha ina uwezo wa kusanifiwa na kusarifiwa kwa njia nyingi. Kiisimu, kuwepo kwa sanaa ni ushahidi unaonyesha kwamba lugha inaweza kuvyaziwa miundo mingi kadri mtumiaji wake anavyotaka. Lugha ina uwezo wa kuvuka vizingiti vingi kimaana. Dhima kubwa ya waandishi wa hadithi fupi na wahakiki ni kubainisha na kuchanganua lugha kama kipengele kinachomwezesha mwanasanaa kutumia maneno machache kuwasilisha dhana pana.

Baadhi ya mihimili ya nadharia ya Kimuundo ni kama ifuatavyo:

- Nadharia ya Umuundo inaweka mkazo kwenye unasibishaji wa maana. Maana nasibishi ya neno ni maana inayohusishwa na neno hilo wala sio kile kinachorejelewa. Matumizi ya lugha hudhihirika katika muktadha maalumu. Lugha ya kifasihi hutilia maanani muktadha kila wakati. Fasihi inahusu uchanganuzi, uteuzi na matumizi ya maneno kwa uangalifu. Hivyo inapasa jamii kutumia lugha kulingana na miktadha na hali mbalimbali.

- Katika kazi ya kifasihi kuna udhihirishaji wa muundo wa jumla ambao hupuuza maswala yanayohusiana na yaliyomo au maudhui. Kwa kuwa maana ya kazi ya kifasihi inatokana na kaida za mifumo ya kuashiria.
- Kulingana na Wamitila (2003), nadharia hii inashikilia kwamba mbali na lugha ya kifasihi tunayoiona katika kazi ya fasihi pana uwezekano wa kuwa na maana zaidi ya zile tunazozijua. Hivyo mhakiki anapaswa kuchunguza maana zaidi kulingana na muundo wa maneno kwani yatumiwapo kuisanii kazi ya fasihi huweza kuashiria maana tofauti na zile ambazo tumezoea. Neno linaweza kuwa na maana fulani funge inayotambuliwa na ung'amuzi wa msemaji. Kuuacha mmuliko wa lugha kimaongezi na kuumulika uandishi na suala la matini.

Kwa jumla, kama ambavyo muundo wa lugha ni mfumo, muundo wa hadithi fupi una vipengele vinavyotegemeana na vinavyoelezwa katika muktadha wa vipengele vingine.

Katika kazi yetu kuna vitengo vya kifasihi kama vile maudhui, mandhari, wahusika na msuko. Hakuna kipengele cha hadithi fupi kati ya hivi kitakachoelezwa vizuri katika upekee wake. Lazima kielezwe kwa kuzingatia kuwepo kwa jukumu la vipengele vingine. Katika, kwa mfano kuzungumzia msuko, wahusika watashirikishwa na lugha yao kuzingatiwa.

Nadharia ya Umuundo husisitiza vipengele vya kazi ya sanaa, jinsi vinavyohusiana hadi kuikamilisha kazi hiyo. Huangalia namna sehemu mbalimbali za kazi ya sanaa zimefungamana kwa mfano, hadithi fupi ina msuko, wahusika na mandhari ambavyo huingiliana na kuchangiana. Hivyo, utafiti wetu umekitwa katika muundo wa kazi nzima kwa kuvihusisha vipengele vyote vya fasihi ili kuwasilisha maudhui.

Kwa mujibu wa kazi yetu, tutatumia mihimili ifuatayo:

a) Muundo wa hadithi fupi una vipengele vinavyotegemeana na vinavyoelezwa katika muktadha wa vipengele vingine.
b) Hakuna kipengele cha fani kinachoweza kujisimamia katika uwasilishaji wa maana na hasa maudhui bila kuhusishwa na vipengele vingine. Kwa mfano kuzungumzia msuko, wahusika na mandhari kama vipengele vilivyotengana.

### 1.8 Yaliyoandikwa kuhusu Mada

Muindi (1990) alichanganua usawiri wa wahusika makahaba katika vitabu vya Said A. Mohamed. Wahusika hawa wamepewa wasifu kimaumbile unaooana na majukumu waliyosawiriwa kuyatekeleza. Hata hivyo, kazi yetu ni tofauti na yake kwa sababu sisi tunaangazia vipengele vya mandhari, wahusika na mianzo na vimalizio vya hadithi fupi katika kufanikisha uwasilishaji wa maudhui. Kazi ya Muindi hata hivyo ilitufaa kwa sababu ilichunguza wahusika ambayo ni sehemu ya suala letu.

Mohochi (1995) amehakiki fani katika hadithi fupi za Kiswahili katika tasnifu yake ya uzamili. Hadithi fupi ambazo amehakiki ni*Wasubiri Kifo* ya Kezilahabi, *Siri ya Bwanyenye*, ya Mulokozi, *Kicheko Cha Ushindi* ya Mohammed S. Mohammed na *Msiba Wa Pamoja* ya S.A Mohamed. Baadhi ya vipengele ambavyo amehakiki ni lugha. Katika utafiti wetu tumeshughulikia jinsi mandhari, wahusika na mianzo na vimalizio vya hadithi fupi vinachangiana na kukamilishana katika kufanikisha uwasilishaji wa maudhui.

Utafiti huu unatusaidia kuelewa jinsi vipengele vya fani vimesaidia kufanikisha uwasilishaji wa maudhui. Hata hivyo, utafiti wetu ni tofauti na wa Mohochi kwa sababu amehakiki fani katika hadithi fupi za Kiswahili lakini hakujikita katika mtafiti maalum kama sisi.

Ndung'u (1996) alishughulikia uhakiki wa fani katika riwaya za Katama Mkangi. Riwaya hizi ni pamoja na *Ukiwa, Mafuta* na *Walenisi*. Ndung'u alichanganua jinsi baadhi ya wahusika wameumbwa na majukumu yao. Aligusia kuhusu mbinu zilizotumika kuwaumba wahusika hao kama vile majazi, drama na nyinginezo. Kazi hii ni tofauti na yetu kwa sababu inaangazia vipengele vya fani katika riwaya za Katama Mkangi, ilhali sisi tunachunguza uwasilishaji wa maudhui katika hadithi fupi za S.A. Mohamed. Kazi ya Ndungu inatufaa kwa sababu inaangazia kipengele cha wahusika jinsi wanavyoumbwa na majukumu yao katika kuwasilisha maudhui.

Musyoka (1996) amehakiki vipengele vya fani katika fasihi kama vile ploti, wahusika na matumizi ya lugha. Musyoka akifafanua maana ya fani anasema kuwa, fani ni vipengele vya kisanaa ambavyo kwa pamoja hujenga umbo la kisanaa. Kazi ya fasihi hujengwa kutokana na uteuzi wa vipengele vya fani vya kibinafsi vilivyotumiwa na mtunzi ambaye pia huwa na uwasilishaji wa kipekee na wenye kutambulisha ubinafsi wa uumbuji wake. Musyoka anaeleza kuwa matumizi ya fani kazi za fasihi. Imedhihirika kuwa, kila msanii ana mtindo wake wa kutumia fani hizi. Wakati mwingine mtindo huu wa kibinafsi humtambulisha kati ya watunzi wengine. Hata hivyo, utafiti wetu ni tofauti kwa sababu unaangazia jinsi mandhari, wahusika na mianzo na vimalizio vya hadithi fupi vinachangiana kufanikisha uwasilishaji wa maudhui katika diwani za Said A. Mohamed. Kazi hii imetusaidia kufahamu aina mbalimbali za fani za lugha na jinsi zinavyotumiwa kuwasilisha maudhui katika hadithi fupi za Said A. Mohamed.

Nzuki (2003) amechunguza mwingiliano wa fani na maudhui katika diwani mbili za Kithaka wa Mberia: *Mchezo wa Karata* (1997) na *Bara Jingine* (2001). Alitumia nadharia ya Umuundo. Mchango wa utafiti huu ni kwamba, uteuzi wa vipengele vya fani una mchango mkubwa katika kuyaunda maudhui. Nzuki ameshughulikia kipengele cha fani ambacho ni matumizi ya lugha. Ameorodhesha mbinu za lugha kama vile tashbihi, takriri, sitiari, taashira, maswali ya balagha na msisitizo bayana. Kazi yake imetufaa kwa

sababu ni kupitia matumizi ya lugha ambapo tunaelewa tabia na mienendo ya wahusika, kuelewa mandhari na msuko wa hadithi mbalimbali. Hata hivyo, kazi hii ni ya ushairi ilhali yetu ni ya hadithi fupi za Said A. Mohamed.

Mbuthia (2005) amehakiki mtindo na maudhui katika hadithi fupi za Kiswahili. Baadhi ya maswala aliyoyahakiki ni msuko na mandhari katika hadithi fupi za Kiswahili. Hata hivyo, utafiti huu ni tofauti kwa sababu katika kazi yetu, tunaangazia jinsi mandhari, wahusika na mianzo na vimalizio vya hadithi fupi vinavyofanikisha uwasilishaji wa maudhui katika hadithi fupi teule za Said A. Mohamed. Kazi ya Mbuthia imetufaa kwa sababu inaangazia vipengele vya msuko na mandhari katika hadithi fupi za Kiswahili.

Ongarora (2007) ameshughulikia mtindo katika *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine*. Ameangalia mtindo kama matumizi ya lugha. Amehakiki ukiushi katika mpangilio wa nomino, vitenzi, vielezi, viunganishi na vihusishi katika sentensi. Tena ameangazia baadhi ya ukiushi wa kisemantiki na mbinu nyingine za lugha katika *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine*. Diwani hii haijashughulikia uwasilishaji wa maudhui katika hadithi fupi za Said A. Mohamed kama vile tunavyofanya katika kazi yetu. Hata hivyo, uchanganuzi wake ni muhimu kwa kuwa umetupatia mwanga wa kuhakiki uwasilishaji wa maudhui katika hadithi fupi za Said A. Mohamed.

Mwilaria (2011) amehakiki fani katika *Utenzi wa Ayubu*. Ametumia nadharia ya Urasimu. Matokeo ya utafiti wake ni kwamba, fani ina mchango mkubwa katika kufumbata malengo ya msanii. Kwa hivyo, alichukua fani kama kipengele muhimu sana cha fasihi. Tofauti na utafiti huu, sisi tumejikita katika uwasilishaji wa maudhui katika hadithi fupi za Said A. Mohamed. Hata hivyo, utafiti huu umetusaidia kubainisha aina mbalimbali za fani na jinsi zinatumiwa kuendeleza maudhui katika kazi ya fasihi.

Tambasi (2011) alihakiki vipengele vya kisanaa katika *Utenzi wa Tambuka*. Tambasi alitumia nadharia ya Umuundo. Tofauti ilioko na kazi yetu ni kuwa yeye alifanya uhakiki wake katika kazi ya Tambuka ambayo ni utanzu wa ushairi ilhali kazi yetu ni hadithi fupi za Said A. Mohamed. Kazi yake imetufaa kwa maana dhana ya muundo imeelezewa kwa sababu ni mojawapo ya fani za kifasihi.

Were (2012) ameonyesha jinsi vipengele vya fani: Ploti, wahusika, dayolojia na monolojia vinavyohusiana na kufanikisha ujenzi wa tamthilia ya *Kilio Cha Haki* (1981) ya Alamin Mazrui na *Kijiba Cha Moyo* (2009) ya Timothy Arege kwa kutumia nadharia ya Umuundo. Kazi yake inatufaa katika kushughulikia ploti kwa lengo la ujenzi wa maudhui. Hata hivyo, kazi hii ni tofauti na utafiti wetu kwa sababu mhakiki ameshughulikia vipengele vya fani katika tamthilia ilhali sisi tumechunguza jinsi mandhari, wahusika na mianzo na vimalizio vya hadithi fupi vinavyofanikisha uwasilishaji wa maudhui katika diwani teule za Said A. Mohamed.

Katutu (2013) amehakiki mtindo katika *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine*. Anasema kwamba, mtindo ni sifa bainifu za kazi fulani, hasa kwa kurejelea lugha iliyoandikwa. Hivyo fasihi hutumia lugha kama malighafi ili kufanikisha majukumu yake. Mwandishi husuka lugha kwanamna apendavyo ili kupitisha ujumbe wake. Utafiti wa Katutu umeongozwa na nadharia ya Elimumitindo. Akimnukuu Wamitila, (2008), anasema umitindo hutumiwa kurejelea mkabala wa uchanganuzi unaohusisha maarifa ya Isimu na huweza kuelezwa kama nadharia ambayo iko katikati ya isimu na fasihi. Nadharia hii ina mwelekeo wa kifani na inadhamiria kuchunguza mtindo wa matini za kifasihi. Hata hivyo, utafiti wetu ni tofauti kwa sababu unashughulikia hadithi fupi za Said A. Mohamed: *Sadiki Ukipendana Hadithi Nyingine*, (2002), *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine*, (2005) *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine, (2005)* ilhali Katutu ameshughulikia mtindo katika diwani moja ya mwandishi mmoja *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine* ya Said A. Mohamed. Pia ametumia nadharia ya Elimumitindo. Utafiti wa Katutu unatufaa kwa sababu unaangazia kipengele cha fani ambacho ni mtindo ilhali sisi tunaangazia vipengele vya fani: mandhari, wahusika na mianzo na vimalizio vya hadithi fupi. Vipengele hivi vya kifani vinachangiana na kukamilishana katika kuwasilisha maudhui.

Kanyua (2013) amehakiki mtindo unavyoendeleza maudhui katika *Natala*. Kanyua ametumia nadharia ya Umuundo na Ufeministi wa Kiafrika. Alishughulikia vipengele vya kimtindo vya wahusika, matumizi ya lugha na maudhui katika ujenzi na uendelezaji wa ukombozi wa wanawake katika jamii iliyotawaliwa na mfumo wa ki-ubabedume unaojitokeza katika *Natala*. Kazi hii imetufaa kwa sababu inashughulikia baadhi ya vipengele vya fani kama vile wahusika na mbinu za lugha katika kuendeleza maudhui.

Hata hivyo, utafiti huu ni tofauti na wetu kwa sababu tunachunguza jinsi mandhari, wahusika na msuko vinafanikisha uwasilishaji wa maudhui katika diwani teule za Said A. Mohamed.

Muiruri (2016) amehakiki maudhui yanavyoimarishwa na fani katika riwaya ya *Nguvu Ya Sala* ya K.M. Wamitila. Alitumia nadharia ya Umuundo. Muiruri ameshughulikia vipengele vya fani kama vile msuko, mandhari na wahusika. Anasema kwamba, fani ni dhana ambayo ni muhimu katika kufanikisha kazi yoyote ya fasihi. Aidha, fani hutumika kwa njia tofauti kutegemea utanzu husika. Utafiti wetu unashughulikia uwasilishaji wa maudhui katika hadithi fupi za Said A. Mohamed.

Kang'eri (2017) ameshughulikia uchunguzi wa vipengele teule vya fani ambavyo ni mandhari, matumizi ya lugha, usimulizi na maudhui kwa kuangalia jinsi mwandishi alivyovitumia katika kufanikisha *MashetaniwaAlepo*. Alitumia nadharia ya Umuundo na Uhalisiajabu. Amechanganua vipengele mahususi vya fani na pia kuchunguza iwapo vinabainisha riwaya hii kama riwaya ya kimajaribio. Kazi hii ni tofauti na yetu kwa sababu inashughulikia riwaya ilhali sisi tunashughulikia hadithi fupi teule za Said A. Mohamed. Kazi hii imetusaidia kufahamu mandhari katika kufanikisha uwasilishaji wa maudhui.

Katika sehemu hii tumerejelea kazi zilizoandikwa kuhusu somo letu. Kazi zilizoandikwa zinatofautiana na kufanana kwa kiasi fulani na kazi yetu. Hata hivyo, tumeonyesha tofauti na kufanana kwa kazi hizo na yetu. Kufanana kwa kazi hizo kumetusaidia kuangazia jinsi mandhari, wahusika na mianzo na vimalizio vya hadithi fupi vinachangiana na kukamilishana ili kufanikisha uwasilishaji wa maudhui.

### 1.9 Mbinu za Utafiti

Katika mbinu za utafiti, tumefafanua uteuzi wa sampuli, ukusanyaji data, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa data.

#### 1.9.1 Uteuzi wa Sampuli

Sampuli tunayotumia ni sampuli ya kimaksudi. Kwa mujibu wa Mugenda na Mugenda (1999) aina hii ya sampuli huhusu data iliyochaguliwa kwa maksudi ili kufikia malengo

mahususi. Tulisoma hadithi mbali mbali za Said A. Mohammed kisha tukachagua zile ambazo zinaangaza vyema maswala ya mandhari, uhusika na msuko.

### 1.9.2 Ukusanyaji wa Data

Katika ukusanyaji wa data, kwanza kabisa tulizisoma hadithi fupi teule za Said A. Mohamed na kuchunguza jinsi mandhari, wahusika na mianzo na vimalizio vya hadithi fupi vinavyofanikisha uwasilishaji wa maudhui. Tulichuja vipengele vya fani: mandhari, wahusika na mianzo na vimalizio vya hadithi fupi teule ili kuelewa jinsi mandhari, wahusika na mianzo na vimalizio vya hadithi fupi vinachangiana na kukamilishana ili kuwasilisha maudhui kwa njia kamilifu. Pia tulisoma tasnifu za wasomi wengine zilizoandikwa kuhusu Nadharia ya Umuundo.

### 1.9.3 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data

Data iliyokusanywa tuliichanganua kwa kutumia mihimili ya Nadharia ya Umuundo. Tulichanganua vipengele vya fani: mandhari, wahusika na mianzo na vimalizio vya hadithi fupi teule za Said A. Mohamed. Baada ya kukusanya na kuchanganua data, uwasilishaji wa matokeo yetu ulifanywa kwa njia ya maelezo, utoaji wa mifano na unukuzi wa mambo yaliyo muhimu kwa mujibu wa mada ya utafiti.

## 1.10 Hitimisho

Katika sehemu hii tumeshughulikia vipengele mbalimbali na ambavyo ni vya kimsingi katika utafiti wowote ule. Dhana na masuala tuliyogusia katika sehemu hii ndiyo yanayojitokeza katika sura tatu zinazofuata.

Tumeangazia tatizo la utafiti, maswali ya utafiti na malengo ya utafiti kwa njia ya kitaalamu kwa kuwa maelezo mwafaka kuhusu dhana hizi ni muhimu sana katika utafiti wowote. Hii inamaanisha kwamba maelezo kuhusu dhana hizi yasipojitokeza wazi, basi huenda mtafiti asiweze kumudu na kupata mwelekeo unaofaa katika kuendeleza kazi yake.

Aidha tumedhihirisha upeo na mipaka ya kazi yetu. Hii ni sehemu muhimu ya utafiti kwa kuwa inaonyesha shughuli za mtafiti na humsaidia kupanga kazi yake na kuokoa muda wa kutafiti. Pia tumefafanua msingi wa kinadharia. Kuhusu msingi wa kinadharia,

tumefafanua nadharia ya Umuundo kwa kuwa ndiyo iliyotufaa katika uchanganuzi wa kazi yetu. Tumeeleza waasisi wa nadharia hii na mihimili yake.

Mwisho tumeshughulikia yaliyoandikwa kuhusu mada yetu ya utafiti. Hatimaye, tumeonyesha mbinu zilizotumika katika utafiti huu.

# SURA YA PILI

# MANDHARI NA UWASILISHAJI WA MAUDHUI

## 2.1 Utangulizi

Mandhari ni kipengele mojawapo muhimu sana katika fasihi, (Wamitila 2008). Mandhari hurejelea mazingira, mahali au wakati ambao ni msingi wa kazi au kisa kinachosimuliwa. Ingawa utanzu wa hadithi fupi hauna upana wa mandhari kwa sababu ya ufinyu wake, mandhari yana nafasi muhimu katika hadithi fupi.

Baadhi ya majukumu ya mandhari ni kutufichulia ni wapi, lini na vipi matukio fulani yalifanyika. Mandhari hutumiwa kurejelea wakati na sehemu ambapo matukio ya kisa hutokea. Mandhari fulani inaweza kuathiri tabia na lugha ya wahusika.

Kazi yetu imetathmini mandhari ya mahali na mandhari ya wakati. Kwa hivyo, kwenye sehemu hii tumetathmini jinsi ambavyo mandhari yanavyofanikisha uwasilishaji wa maudhui katika diwani za Said A. Mohamed.

## 2.2. Mandhari ya Mahali

Hadithi fupi huakisi na kuonyesha umoja wa mahali ambako tukio kuu linatendeka. Mahali huweza kuwa nguzo muhimu ambayo inaathiri maudhui na uwasilishaji wake. Baadhi ya mandhari yaliyoteuliwa kuchunguzwa katika hadithi fupi teule ni kama ifuatavyo: mandhari ya mashambani, nyumbani na danguroni.

### 2.2.1 Mashambani

Katika sehemu hii, tumeangazia mandhari ya mashambani. Mashambani yanaweza kuwa pia ya kijijini, mahali ambapo wanajamii huishi na kutekeleza majukumu yao.

Katika hadithi fupi, ‘*Sadiki Ukipenda na Hadithi Nyingine’* (2002), ‘Sadiki Ukipenda’, Said A. Mohamed anatuchorea mandhari ya mashambani. Katika hadithi hii mwandishi anasawiri mandhari kijijini ambayo yameathiriwa na kiangazi na ukame. Wanajamii waliathiriwa sana na hali hii. Kwa mfano, Mussa alikuwa mmoja wa wanajamii walioathiriwa. Hii ni kwa sababu mandhari haya yanatufichulia kwamba Mussa aling’ang’ana kumaliza shida zilizomkabili lakini hakupata mafanikio mazuri. Mussa anasema kila mara alikuwa mbioni.

Vilevile, katika hadithi hii ya ‘Sadiki Ukipenda’ (2002) mandhari ya mashambani yanatuonyesha dhiki ambazo Mussa alizipitia. Hii ni kwa sababu Mussa alikuwa anapitia shida nyingi. Mussa anakumbuka mawaidha ya Mzee Siwa kwamba afuatilie ndoto zake kokote zitakakompeleka. Kwa hivyo, ajihadhari maishani. Pia kuna mandhari ya mashambani ambapo tunamwona Mussa akienda kumtafuta Mzee Siwa na baada ya kumkosa aliteremka bondeni, kondeni mwake. Akamkuta ameshamaliza kupalilia. Sasa akawa anakwangura jembe lililokuwa limegandia tope. Tunaambiwa baadaye akalisuuza kwa maji yaliyopita kwenye kijito kilichotiririka mbele ya kibanda chake. Hivyo, mandhari haya yanatufichulia kwamba jamii hii ilikuwa inafanya ukulima ili kuboresha maisha yao hata kama umaskini pia uliwaandama.

Katika mandhari haya ya mashambani mambo yaliyokuwa yakiendelea yaliathiri maisha ya Mussa kwa sababu alifichuliwa siri na Mzee Siwa na mpango wa baba yake dhidi yake ambao haukufaulu. Pia katika hadithi hii ya ‘Sadiki Ukipenda’ mandhari ya mashambani yamejitokeza kama mazingira ambamo ushirikina unaendelezwa. Ushirikina unajitokeza pale Mussa alipomrushia mundu wa kichwa baba yake na hakutokwa na damu. Jambo hili lilikuwa la kichawi kwa sababu tunaona baadaye baba yake Mussa aliaga dunia na kumwachia Mussa maisha yake. Pia ushirikina unajitokeza zaidi wakati ambapo Mzee Siwa alikuwa akitumia tambuu. Matumizi ya tambuu yalimwongezea Mzee Siwa maarifa katika kusema mambo hasa akiamua jambo muhimu. Pia mandhari haya yanaonyesha ushirikina, kwa sababu Mussa hangeelewa kauli ya Mzee Siwa kwamba baba yake ni Mchawi. Lakini Mzee Siwa alimhakikishia Mussa kuwa uchawi upo, asadiki akipenda na kama haamini angemthibitishia ukweli wa maneno yake. Alikuwa anaramba dari na sakafu ya kinywa chake kugundua masalio ya tambuu yaliyoganda. Kisha akaanza kumpangia Mussa vile angejiepusha na ukatili wa baba yake.

Katika hadithi ya ‘Sadiki Ukipenda’ mandhari ya mashambani vilevile yanatufichulia maudhui ya ushirikina na jinsi yanavyowasilishwa. Hii ni kutokana na jinsi watu walivyompagaza Mzee Siwa jina la mjuaji! Na wengine mchawi! Mandhari haya yanatuonyesha kuwa jamii hii ilikuwa inaamini sana mambo ya uchawi. Hata Mussa amepangiwa kuuawa na baba yake na wachawi wengine kwa njia ya urogi. Pia Mzee Siwa anamwambia Mussa kwamba uchawi upo asadiki akipenda.

Ushirikina unajitokeza zaidi pale Mzee Siwa alifanya wajibu wake kumwokoa Mussa dhidi ya uchawi wa baba yake na wachawi wengine kwa kutumia dawa ya mizizi fulani ambazo alimpa Mussa kuchemsha na kunywa. Nyingine alitaka Mussa aifukie kwenye kizingiti cha chumba chake. Pia alimpa hirizi kubwa kuifunga mkono wa kulia. Huu ulikuwa mpango wa kukabiliana na baba yake.

Katika hadithi 'Ngondo Pangoni' mwandishi pia ametumia mandhari ya mashambani kutufichulia kwamba kulikuwa na matumizi ya tambuu. Hapa ni pale ambapo mtu akitaka kusema jambo muhimu alikuwa akitumia tambuu. Tambuu hii iliweza kumwongezea maarifa fulani ya kusema jambo vizuri na kwa makini hata kama ni vigumu kusema jambo hilo. Kondo alimweleza rafiki yake Jecha kwamba watu walikuwa wameanza kushuku urafiki wao. Hii ni baada ya kutumia tambuu. Mandhari haya ya mashambani yanatuonyesha kwamba marafiki hawa walikuwa wameanza kusikia fununu kuhusu unafiki wao. Hii ni kwa sababu Jecha alikuwa akifanya mapenzi na mke wa Kondo na Kondo alikuwa akifanya mapenzi na mke wa Jecha. Hivyo, hata Jecha hakutaka kujua zaidi juu ya tetezi la Kondo kwa sababu aliogopa siri yake ijulikane na Kondo.

Katika hadithi ya 'Sadiki Ukipenda' mandhari ya mashambani yanatuonyesha utamaduni ambao unapinga elimu. Tunaelezwa kuwa wenyeji wa kijiji hiki hasa wachawi hawakuthamini elimu. Hivyo, walikuwa wamepanga kuua Mussa kwa sababu ni msomi. Jamii hii haikutaki vijana kuendelea na masomo yao. Hii ni kwa sababu wanaogopa wasomi kuwa watawasumbua hasa wachawi. Hii ni kumaanisha ya kwamba wachawi wanaogopa kwamba vijana wakisoma watagundua njama zao na mwishowe kuwamaliza. Hivyo, wanaona ni vyema wawamalize kwanza ndio waendelee na kazi zao za kichawi.

Katika hadithi ya 'Sadiki Ukipenda' mandhari ya mashambani pia yanatufichulia hali ya umaskini, pale tunamwona Mzee Siwa akiwa amejenga kibanda chake karibu na kijito. Pia Mussa anaegemea nguzo ya kibanda. Hii inadhihirisha hali ya umaskini kwa sababu Mzee Siwa hakupata mahali pazuri pa kujenga kibanda chake na kuelekea kujenga karibu na kijito. Hii nikuonyesha kwamba kulikuwa na uhaba wa ardhi ya kujenga kwa sababu ya umaskini na watu kuwa wengi. Kwa hivyo waliishia kung'ang'ania mahali pa kuishi.

Vilevile, katika hadithi ya ‘Ngondo Pangoni’ mandhari ya mashambani yanajitokeza pale tunaona kulikuwa na hali ya umaskini. Hali ya umaskini inadhihirika arusini ya mwana wa Bwana Jabu. Mwandishi anatueleza kuwa kibanda cha Bwana Jabu kilielemewa na wingi wa watu. Pia tunaona karabai nne ziliwashwa kuashiria ya kwamba mandhari haya yalionyesha hali ya umaskini.

Katika hadithi ‘Sadiki Ukipenda’ mwandishi anatuonyesha kwamba wanajamii walikuwa wacha Mungu kupitia mandhari ya mashambani. Tunaona Mzee Siwa akiomba. Pia alimhimiza Mussa kutekeleza faradhi ya sala. Tunaona Mussa anapomtazama Mzee Siwa akijitayarisha kumkabili Mungu wake huku moyo wa Mussa ukimsimanga. Kuna jambo lilikuwa likimsumbua na baada ya Mzee Siwa kuomba alipata amani moyoni. Tunaona ya kwamba mtu akiomba hujiwa na amani rohoni na kwamba Mungu anaweza mambo yote. Hii ni kweli kwa sababu Mzee Siwa alimwaarifu Mussa kwamba baba yake na wachawi wengine walinuia kumwondoa duniani. Ni kupitia sala haya hayakutimia kwa sababu Mzee Siwa aligundua mapema na kupanga na Mussa jinsi atakavyojiokoa kwa kumuua baba yake. Hivyo, tunapata maudhui ya imani.

Katika hadithi ‘Sadiki Ukipenda’ mandhari ya mashambani yanatufichulia jukumu la watoto kutunza wazazi wao wakizeeka na kuaga dunia. Hivyo, tunaonyeshwa kwamba watoto na vijana wana umuhimu mkubwa kwa wazazi wao. Watoto na vijana ndio tegemeo la wazazi wao watakapozeeka na hatimaye kuaga dunia, wao ndio watakaowatunza wakiwa wagonjwa na kuwazika watakapoaga dunia.

Katika hadithi ‘Sadiki Ukipenda’ mandhari ya mashambani yanatuonyesha ukatili wa kiwango cha juu. Hapa baba yake Mussa anapanga pamoja na wachawi wengine kumwangamiza lakini inatokea kinyume. Mussa haoni kufanya kosa la kuua baba’ake. Anaona ni bora kwa sababu anatetea roho yake. Ukatili unajitokeza zaidi katika mandhari haya ya mashambani pale wachawi walipokuwa wakicheza ngoma walitumia magongo, marungu, mawe, mapanga walipokuwa wakitwanga zuzu. Hivyo, tunaonyeshwa kuwa wachawi hawa hawakuwa na huruma. Ukatili uliwatawala na hata kuwa na furaha, vicheko na vifijo wakiimba wimbo mtamu walipokuwa wakitekeleza ukatili huu.

Katika hadithi 'Ngondo Pangoni' mwandishi anatuchorea mandhari ya mashambani. Katika mandhari haya tunawapata marafiki wawili Kondo na Jecha. Marafiki hawa hukutana hapo chini ya mwembe mkubwa kuzungumza. Baadhi ya mambo wanayoyazungumza ni kuhusu wanawake waliofanya na wao mapenzi. Hivyo tunaona wahusika hawa walishiriki uasherati na umbea. Pia tunaona urafiki wao uliishi kwa miaka. Hii ni kwa sababu walikuwa na tabia ambazo zilifanana. Tunaelezwa kuwa Kondo na Jecha wote walishiriki uasherati na uzinzi. Tabia zao za uzinzi zilifanana. Hii ni kwa sababu Kondo alikuwa anafanya mapenzi na mkewe Jecha na vilevile Jecha alikuwa akifanya mapenzi na mkewe Kondo.

Kondo na Jecha walikuwa na urafiki wa 'dhati', lakini watu waliwashuku. Hata hivyo, Kondo na Jecha walipuuza na kusema kwamba duniani lazima watu waongee kuhusu watu wengine. Hivyo, haya hayakuwashtua. Walijali zaidi masikilizano yao yalivyokuwa yakiwaendea. Hivyo, hawakujali watu walivyosema.

Katika hadithi ya 'Ngondo Pangoni' mandhari ya mashambani yanatufichulia kudunishwa kwa mwanamke na ubabedume. Tunaelezwa kuwa hata kama Kondo na Jecha wanawaheshimu wanawake bado kuna mambo ambayo wanaona si mazuri kwao. Hii ni njia ya kudhalilisha wanawake kwa sababu hawatosheki na yale wanawake wanawafanyia. Vilevile, mwandishi anatuonyesha ubabedume pale wanaume wanafikiria wao ndio wazuri zaidi kuliko wanawake. Hapa tunaelezwa kuwa wanaume ndio wenye kuweka mambo mkazo kuliko wanawake. Hivyo, wanaume wanajiona bora kuliko wanawake.

Katika hadithi ya 'Ngondo Pangoni' mandhari ya mashambani yanatufichulia kwamba wake wa Kondo na Jecha walikuwa watawa. Hii ni kumaanisha kwamba hawakuwa na uhuru wa kutoka na kujua mengi wanayoyafanya. Wanasema kwamba wake zao ni waaminifu kwa waume zao. Maneno wanayoyasema ni kujaribu kuficha uzinzi miongoni mwao. Pia Jecha na Kondo wanasema hivyo ndio kila mmoja wao aruhusu mkewe atake aende arusini wapate kuonana pale. Kondo na Jecha wanatuonyesha kwamba walikuwa wanataka wake zao wapewe uhuru wa kutoka. Walijua wakitoka kila mmoja wao angebahatika.

Katika hadithi 'Ngondo Pangoni' mwandishi pia anatufichulia unafiki kati ya Kondo na Jecha. Wanasema hawataenda arusini ilhali wanaingojea kwa hamu na ghamu. Hii ni kwa sababu Kondo alipanga waonane na Bi. Sihaba mkewe Jecha na Jecha pia wakutane na Bi. Mwamboje Mkewe Kondo.

Katika hadithi ya 'Mhanga wa Mwanamaua' mandhari ya mashambani yanajitokeza. Kuna maudhui ya utamaduni pale wanakijiji waliamini nguvu ya kupeana majina kwa watoto wao hasa wanapozaliwa. Kwa mfano, kuna kutilia mkazo ufaafu wa jina la mhusika Mwanamaua kwamba anapendeza. Kivutio kingine ni kuwa hili ni jina la kinga analokabidhiwa msichana anapozaliwa kisiwani pemba. Mwanamaua anavutia wanaume wengi kwa urembo na tabia yake. Mandhari haya ya mashambani pia yanatufichulia ufaafu wa kichwa chake! Mhanga wa Mwanamaua; Kwa sababu Dadi anakubali kupigana na ng'ombe Kipelele na hatimaye akauawa; anakuwa kafara.

Katika hadithi ya 'Mhanga wa Mwanamaua' wanakijiji wa pemba wanatuonyesha mandhari ya mashambani pale wanajitumbuiza kwa mchezo wa kutazama ng'ombe wakiwakimbiza watu katika uwanja wa Wingwi. Wanakijiji walikuwa wanasherehekea mchezo wa ng'ombe. Hivyo, wanakijiji walikuwa wanashirikiana waliposhiriki shughuli mbalimbali kama vile, biashara walipokuwa wakisubiri mchezo wa ng'ombe kuanza. Pia wanakijiji walifurahia kutazama michezo hiyo. Katika sehemu hii tumechunguza mandhari ya mashambani na jinsi yalivyofanikisha uwasilishaji wa maudhui.

### 2.2.2 Nyumbani

Mandhari ya nyumbani yanarejelea makao ambayo yanakusudiwa kukaliwa na watu. Mandhari haya yanaweza kuwa ndani ya makao au hata nje.

Katika hadithi 'Uhuru wa Subira' kuna mandhari ya nyumbani kwa Biti Shomari mama yake Subira. Mandhari haya yanatufichulia maudhui ya kudhalilishwa kwa wanawake. Mandhari haya ya nyumbani yanatueleza kuwa Bi. Shomari na wanawake wengi wanateswa na kufanywa watumwa. Tunaendelea kuelezwa kuwa kuzaliwa mwanamume ni uhuru na kuzaliwa mwanamke ni utumwa. Hivyo hakuna usawa kati ya mwanamume na mwanamke. Kulingana na mwandishi wanawake wanaendelea kudhalilishwa na wanaume.

Mandhari haya ya nyumbani katika hadithi 'Uhuru wa Subira' nyumbani mwa Biti Shomari tunafichuliwa kwamba kuolewa ni kuwa mtumwa. Hivyo, Subira alirejea kwao nyumbani kuomba wazee wake wamsaidie kudai uhuru wake. Pia katika hadithi 'Uhuru wa Subira' tunaona kwamba Subira anapata mateso mengi kutoka kwa mumewe hadiakataka wawachane. Katika mandhari ya nyumbani, tunafichuliwa kuwa Subira alitaka uhuru wake. Ndoa inaonekana kama utumwa na kupata talaka kama kupata huru.

Katika hadithi ya 'Uhuru wa Subira', tunaelezwa kuwa afya ya Subira ilikuwa imedhoofika kwa sababu ya shida nyingi za kilimwengu na hasa nyingi ni zile zilizoletwa na mumewe. Hivyo Subira alikuwa anasubiri uhuru wake. Tunaelezwa kuwa kabla hajaolewa alikuwa na nguvu nyingi kwa sababu alikuwa amelelewa vyema na mama'ake Biti Shomari. Hivyo, mandhari haya ya nyumbani yanatufichulia juu ya malezi bora ambayo yanafanya watoto kuwa na afya nzuri.

Mandhari haya ya nyumbani pia yanatufichulia kuwa baba'ake Subira pia alimsaidia mumewe kumtesa. Hii ni kwa sababu tunaambiwa kwamba baba'ake akifika tu, atampiga na kuapa kwamba akitoka kwa mumewe angemuua. Tunaelezawa kuwa baba'ake Subira alikuwa amezoea kumpiga Binti yake kila alipokuja nyumbani kutokana na habari kutoka kwa mumewe kwamba anataka waachane.

Katika hadithi ya 'Uhuru wa Subira' mandhari ya nyumbani kwa Mzee Farijala yanatuonyesha kuwa mbwa simba alikuwa anampenda Subira. Subira anaonyeshwa mapenzi na Simba ilhali baba'ake mzazi hana mapenzi naye. Vilevile mumewe Mrisho haonyeshi mapenzi kwake. Hivyo anashangaa ni vipi mnyama ana mapenzi kwake na watu ambao wanastahili kumwonyesha mapenzi hawafanyi hivyo.

Mandhari haya ya nyumbani kwa Mzee Farijala yanatuonyesha kuwa Mzee Farijala alikuwa akiwachapa wanawe na bibi yake Biti Shomari. Hivyo, aliamini kwamba lazima wanawake wachapwe kwa sababu ni watumwa na wajinga ambao hawastahili kuhurumiwa. Hivyo Mzee Farijala anaonyesha ubabedume. Hapa mandhari haya yanatuonyesha wanaume ndio wanastahili kuishi kwa uhuru wanaotaka ilhali wanawake wanastahili kudhalilishwa jinsi wanaume wanavyotaka.

Katika hadithi ya 'Mwungwana' mandhari ya nyumbani kwa Bwana Haji, anatuonyesha alikuwa na msimamo mkali, kwamba akiamua jambo lazima alitimize. Bwana Haji alimpa mkewe talaka baada ya kumfumania. Pia katika hadithi ya 'Mwungwana' mandhari ya nyumbani kwa Bwana Haji yanatufichulia kuwa Saada alikuwa msherati. Tunaelezwa kuwa Saada alikuwa mzinifu. Hii ni kwa sababu Bwana Haji alikuwa ameanza kusikia nong'ono za vitendo na uhaini wa mkewe hapo zamani. Kwa hivyo, Bwana Haji alipanga jinsi atakavyomfumania mkewe. Alijifanya ameenda pwani lakini, baadaye akarudi usiku wa manane ili ajue ukweli wa mambo.

Katika hadithi ya 'Uhuru wa Subira' mandhari ya nyumbani yanatufichulia hali ya umaskini ambao umekumba jamii hiyo. Hii ni kwa sababu Mrisho alitoa kibiriti na kuwasha taa ya kibatali iliyokuwepo juu ya kibao. Pia chumba chao kilikuwa kidogo sana. Hivyo, tunaonyeshwa umaskini uliokuwepo kwa familia ya Mrisho. Umaskini huu ndio ulichangia Mrisho kuwa mlevi wa kupindukia ili asiulizwe na mkewe na tena anarejea alfajiri asipate kutafakari zaidi juu ya maisha yake.

Katika hadithi ya 'Njia fupi', mandhari ya nyumbani kwa Fumu yanatufichulia kwamba Naima anapanga njia thabiti ya kumfumania mumewe Fumu aliyekuwa mzinzi na hatimaye anafaulu siri yake inafichuka wakati  Naima alipomfumania kwa Mama Kitimbi. Hamtolei ukali mumewe bali anamshika mkono na kumwambia warejee nyumbani. Katika hadithi 'Njia fupi' mandhari ya nyumbani yanatuonyesha ufaafu wa anwani ya Njia fupi. Inaafiki tabia ya ulaghai na uasherati wa Fumu ambaye hatimaye anagunduliwa na mkewe. Fumu anamuacha mkewe mrembo Naima na kwenda danguro la Mama Kitimbi kutafuta makahaba. Naima anapogundua siri hii, anajikwatua kwelikweli na kujipeleka huko danguroni kama mmoja wa makahaba. Fumu anapokimbilia huku kutuliza joto lake la mwili, anamkuta huko. Njia ya uwongo wake ikawa fupi, mkewe anagundua na kumwaibisha. Njia yake ni fupi. Anwani hii inaasa kuwa, uwongo huwa haudumu.

Katika hadithi ya 'Mwungwana', mwandishi anatuonyesha mandhari ya nyumbani kwa Bwana Haji kwamba kuna haki ya mke na Bwana katika ndoa. Haki ya mume ni kuonyeshwa mapenzi na mkewe lakini haki hiyo inatumiwa na mtu mwingine. Kibwana anafanya mapenzi na Mkewe Bwana Haji hivyo, kumnyanganya haki yake. Haki ya mke

kwa mumewe ni kuvalishwa mavazi mazuri na kula unono. Bwana Haji anasema kuwadunia imejaa hatari kwa sababu Kibwana anakuja mpaka nyumbani kwake kufanya mapenzi na mkewe, hivyo kamnyanganya haki yake.

Katika hadithi 'Njia fupi' mandhari ya nyumbani kwa Fumu, Fumu anajua fika kwamba yeye mwenyewe ndiye alikuwa anavunja ndoa yake. Hii ni kwa sababu anasema pia talaka haingewezekana kati yake na Naima. Mandhari haya yanatuambia kwamba ndoa kati ya mke na mume inastahili kuwa ya kuaminiana. Fumu anaonyesha kuwa si mwaminifu kwa mkewe ilhali mkewe ni mwaminifu kwake. Pia katika hadithi hii mwandishi anasema: ''Tabia ya mwanadamu ni ya uambangoma, kila mmoja huvutia kwake''. (Uk.131). Mandhari haya ya nyumbani kwa Fumu yanatufichulia kwamba Fumu anataka kujitoa lawamani kwa kuwa na jicho la nje. Fumu anasema kuwa hawezi kujizuia na daima hujifikiria kwanza bila kujali hata kama angesaliti mapenzi ya mkewe Naima. Hii ni kuonyesha mandhari haya ya nyumbani kwa Fumu yanatuonya waliojawa na uchoyo wa ubinafsi wawe wanawafikiria wengine pia. Mandhari haya yanatuonyesha usaliti wa mapenzi kati ya wapendanao katika jamii. Katika hadithi ya 'Njia fupi' mandhari ya nyumbani kwaFumu yanatufichulia usaliti wa Fumu kwa mkewe Naima. Anazoea kutembelea mahawara katika nyumba ya Mama Kitimbi.Mkewe Naima anapomfumania.

Kuna maudhui ya usaliti wa Fumu. Aibu ya Fumu ya kumlemeza viungo vyake asiweze kusonga kuchangia pakuu uelewa wa hali yake. Katika hadithi ya 'Njia fupi', Naima anajikwatua sawasawa kwa rangi ya mdomo, podari, kujirashia mafuta mazuri, kuzikoleza kope wanja na kadhalika. Anajikwatua hivi kabla ya kwenda kwa Mama Kitimbi ambapo anapanga kumnasa mume wake Fumu katika tabia zake za uzinzi.

Mandhari ya nyumbani katika hadithi 'Njia fupi' yanatufichulia uchu aliokuwa nayo Fumu. Fumu anashuhudia mkewe Naima akijirembesha chumbani mwao. Naima alikuwa ametimua shore kichwani, amepaka uso wake podari, macho ameyaimarisha kwa wanja mweusi na midomo yake imerembwa kwa rangi ya waridi.

Katika hadithi ya 'Njia fupi' tunaelezwa: "Na sasa katatizwa. Nguvu mbili zilikuwa zikizongana kichwani. Naima! Kwa Mama Kitimbi'', (Uk.133). Naima anamwacha

mumewe Fumu chumbani mwao bila kumwambia wazi anakoenda. Fumu anatatizika asijue amfuate mkewe ajue mipango yake au aende kwa Bi. Kitimbi. Hali aliyojipata kwayo Fumu ilimchochea aende kwa Bi. Kitimbi ili uozo wake kumwendea kinyume mkewe ujulikane. Hivyo, maudhui ya uzinzi. Kwingineko tunaelezwa kuwa Fumu alienda kwa Mama Kitimbi ili kujaribu kuzimua joto lake la roho. Mandhari haya yanatufichulia jinsi Fumu alikuwa anatarajia kufanya mapenzi na makahaba hivyo, maudhui ya tamaa ya mapenzi.

Katika hadithi ya 'Njia fupi', mandhari ya nyumbani kwa Fumu tunaonyeshwa kuwa Naima anajipamba na kupambika. Hivyo, tunaona Naima alikuwa mrembo kwa sababu Fumu alikuwa akimwangalia kwa upembe kujaribu kulishibisha jicho lake sirisiri uzuri wa mkewe usiochujika.  Mwandishi anamaanisha kwamba macho ya mtu hukiangalia kitu au mtu kwa hamu kwa sababu yamependezwa na yanachoangalia. Hivyo, maneno haya yanamulika nafasi ya mwanamke katika jamii. Mojawapo ni kuchukuliwa kama pambo la kurembesha nyumbani au mandhari fulani. Fumu anavutiwa sana na urembo wa mke wake Naima. Vilevile, mandhari haya yanatuonyesha kuwa Naima alipanga njia thabiti ya kumfumania mumewe na kumwaibisha ili ajirudi.

Katika hadithi ya 'Mwungwana' mandhari ya nyumbani kwa Bwana Haji, yanatuonyesha maudhui ya uungwana. Hii ni pale ambapo Bwana Haji alikuwa Mwungwana kwa kutobadilisha nia yake ya kumwacha Saada iwapo atamfumania. Tunaelezwa ya kwamba hata baada ya kumfumania mkewe na Kibwana, hakukasirika au hakumpiga mkewe au mume mwenziwe, alijifanya mwungwana kabisa. Pia baada ya kibwana kutoka, hakumuliza mkewe chochote.

Katika hadithi ya 'Mwungwana' unafiki unajitokeza katika mandhari ya nyumbani. Hii ni kwa sababu Bwana Haji anaelewa kwamba Kibwana yuko nyumbani kwake lakini anajifanya kana kwamba kila kitu kilikuwa katika hali yake ya kawaida. Tunaelezwa kwamba Bwana Haji anaelewa fika kila kitu ambacho kilikuwa kinaendelea nyumbani kwake lakini anajifanya kuwa mambo yalikuwa sawa nyumbani kwake. Hii ni kwa sababu hata anamndang'anya mkewe kuwa hakwenda pwani lakini tunaelewa kuwa alirudi kimakusudi ili amfumanie mkewe.

Unafiki unajitokeza zaidi pale Bwana Haji alipomkuta Kibwana chumbani mwake alijifanya hakuna ubaya wowote na kumwambia aendelee kustarehe na hata kumwita mgeni wake. Bwana Haji alimwambia Kibwana anaweza kuendelea kustarehe kwa sababu ana chumba kingine anaweza akalala huko na kweli alifanya hivyo. Hata kama Bwana Haji alifanya hivyo, moyoni alikuwa anaumia sana kwa sababu hata alipoingia chumba kingine kulala hakulala kwa sababu alisikia Kibwana akitoka.

### 2.2.3 Mandhari ya Danguroni

Katika sehemu hii tunachunguza mandhari ya danguroni. Mandhari ya danguroni yanaonyesha nyumba inayotumiwa na malaya kufanyia umalaya. Ni mahali ambapo uovu unaendelezwa na wahusika tofauti.

Katika hadithi ya 'Njia fupi' tunafichuliwa mandhari ya danguro kwa Mama Kitimbi, taswira ya makahaba wanaoajiriwa na Mama Kitimbi kuwafurahisha wanaume kama Fumu. Walikuwa wamesimama mstari mmoja. Wanaonyesha kutamaukwa kwa binadamu hadi kufikia kujiuza miili yao ili wajikimu. Mandhari haya yanatufichulia maudhui ya ukahaba. Mama Kitimbi anasema "Leo ndio leo asemaye kesho mwongo! Leo ni leo asiye mwana aeleke jiwe". (Uk.134). Tena mama Kitimbi anamjuza Fumu kuwa; na kuwa mwenye macho hambiwi tazama; (Uk.134). Mwandishi anamtayarisha Fumu na kumjaza hamu kutolea joto lake pale ili kuimarisha maudhui ya ukahaba.

Mandhari ya danguroni pia yanatuonyesha jinsi Naima Mambo hakuwa na haraka yoyote katika mpango wake wa kumtega na kumnasa Fumu katika jumba la Mama Kitimbi. Mandhari ya danguronikwa Mama Kitimbi yanatuonyesha jinsi Naima alipanga mumewe aaibike na kuacha tabia yake ya uzinifu.

Katika hadithi 'Njia fupi' Kuna mandhari ya nyumbani kwa Mama Kitimbi. Mandhari haya yanatufichulia maovu yanayofanyika katika danguro lile. Mama Kitimbi ni mmiliki wa 'duka la laana' (Uk.134). Anafanya biashara ya kuwauza wasichana na wanawake kwa wanaume wazinzi kama Fumu ili apate mali. Anawaita wasichana wake malaika na kumfahamisha Fumu alikuwa amepokea kitoto kipya ambacho angelipia milioni kustarehe nacho. Kazi ya Mama Kitimbi ni kudhalilisha na kutukanisha jinsia ya kike. Jina la Mama Kitimbi linaonyesha uozo wa ukahaba miongoni mwa wanajamii.

Mandhari haya ya 'duka la Laana' danguro yanatufichulia kwamba Mama Kitimbi alikuwa na tamaa ya pesa. Mama Kitimbi anamwambia Fumu kwamba angelipa milioni kwa kustarehe na kitoto kipya. Kitoto kipya kilikuwa ni Naima mkewe Fumu.

### 2.3 Mandhari ya Wakati

Katika sehemu hii tunatathmini mandhari ya wakati. Dhana hii hutumika kurejelea kipindi ambacho hali na matukio yanayosimuliwa na uwasilishaji wake hutokea (Wamitila 2003). Wamitila anaendelea kusema ya kwamba kuna wakati hadithi na wakati matini.

Wakati hadithi ni wakati ambapo huchukuliwa na kisa au hadithi fulani inayowasilishwa. Wakati katika hadithi unaweza kutambuliwa kwa kukisia au uwe umetajwa katika kisa chenyewe. Vilevile, matumizi ya njeo mbalimbali yanaweza kutusaidia kutambua wakati mahsusi wa hadithi. Hata kama hadithi nyingi huandikwa kwa kutumia njeo iliyopita, dhamira yake hulenga wakati uliopo. Yaliyosimuliwa hata kama yalipita hulenga jamii ya sasa.

Katika utafiti wetu, tumejikita katika wakati hadithi. Hivyo, tutachunguza wakati wa asubuhi, mchana na usiku na jinsi mandhari haya ya wakati yatafanikisha uwasilishaji wa maudhui.

#### 2.3.1 Mandhari ya Asubuhi

Asubuhi ni kipindi cha siku ambacho kinaleta mwanga wa kwanza wa mchana baada ya giza la usiku.

Katika hadithi ya 'Uhuru wa Subira', mwandishi anatufichulia mandhari ya wakati wa asubuhi. Mandhari haya yanatufichulia kwamba wakati kunapopambazuka jua huwa ishara ya haki. Hii ni kumaanisha kwamba kila siku kunapopambazuka jua huchomoza ili kuangazia viumbe vyote ulimwenguni, kike kwa kiume. Mandhari haya yanatuonyesha kudhalilishwa kwa mwanamke. Mwandishi anatuonyesha kuwa hakuna usawa ulimwengu huu, kwa sababu wanawake wanadhalilishwa na wanaume wanaowaoa. Tunaelezwa kuwa mwanamume anachukuliwa kama kiumbe bora kuliko mwanamke. Hivyo jua linapochomoza hakuna usawa kati ya viumbe vyote na Mungu aliumba viumbe

vyote wawe sawa lakini inaelekea kuwa kinyume pale mwanamume anamdhulumu mwanamke.

### 2.3.2 Mandhari ya Mchana

Mchana ni kipindi chote cha siku ambapo nuru ya jua inaangazia sehemu fulani. Katika hadithi 'Sadiki Ukipenda' mandhari ya wakati wa mchana yanatufichulia kifo. Kuna kifo cha baba'ake Mussa pale Mussa alipomuua akijaribu kujiokoa kutokana na ukatili wa baba yake na wachawi wengine. Baba yake Mussa aliiaga dunia saa sita mchana kila mtu akiona na kushuhudia kifo chake kwa sababu alikuwa anawauwa watoto na vijana usiku wakiwa na wachawi wengine. Hii ni kumaanisha kwamba yale mambo watu wanafanya kwa giza siku moja yatagunduliwa mchana kati ili waaibike. Hivyo Mussa alitamani baba yake afariki dunia ndiyo amwachie maisha yake kwa sababu yalikuwa yanaanza. Hii ni kwa sababu baba yake alikuwa anataka kumwondoa duniani. Hivyo maisha ya Mussa yalikuwa ni muhimu zaidi kuliko ya baba yake.

### 2.3.3 Mandhari ya Usiku

Katika sehemu hii, tunachunguza mandhari ya wakati wa usiku. Usiku ni kipindi cha siku kilichopo kati ya machweo na macheo na hasahasa kipindi cha giza kinachotokea baada ya machweo ambapo mwanga wa jua hauonekani tena angani hadi muda mfupi kabla ya macheo.

Katika hadithi ya 'Mhanga wa Mwanamaua' mandhari ya wakati wa usiku yanaonyesha Mwanamaua anatoka kwao nyumbani bila kumwambia yeyote ili akakutane na Dadi, mchumba wake. Ulikuwa ni usiku, wakati wa kuchuma karafuu. Mwanamaua anafaulu kumshawishi Dadi apigane na Ng'ombe Kipelele kinyume na kupenda kwake; Ulikuwa usiku wao wa mwisho maana anauawa siku inayofuata na ng'ombe Kipelele.

Pia Mwanamaua anakifurahia kile kiza kwa sababu ni kiza, 'buibui kubwa la wezi na wahalifu' 'Buibui'. Inaonyesha kiza, Yaani 'nguo aghalabu nyeusi ambayo huvaliwa juu ya nguo nyingine na wanawake haswa wa kislamu. Buibui hufunika nguo ya ndani na hapa kiza ni siri kati ya Mwanamaua na Dadi. Kiza kinatilia mkazo maudhui ya papara za wachumba walio tayari kufanya ya hatari mradi wakinaishe tamaa zao.

Pia mandhari haya ya wakati wa usiku katika ‘Mhanga wa Mwanamaua’, Mwanamaua na Dadi wana siku saba kabla ya kuasi ukapera na hamu zao mmoja kwa mwingine zilikuwa juu. Hii ina maana kuwa shida ya kukutana msituni kwa ajili ya kufanya mapenzi itaondoka. Mandhari haya yanatuonyesha kujitupa chini kwenye majani ili kumaliza dhiki ya kukutana msituni. Hii ni kuonyesha kwamba walifanya mapenzi, wakijificha wasionekane kwenye giza kwa sababu ya tamaa ya mapenzi. Kitendo chao kinaonyesha tamaa na uchu mkuu unaowajia vijana wawili wanaodhamiria kufunga ndoa.

Katika hadithi ya ‘Mhanga wa Mwanamaua’ mandhari ya wakati wa usiku pia yanatuonyesha maudhui ya mapenzi. Katika mazungumzo ya Mwanamaua na Dadi, tunaelezwa kuwa Mwanamaua ana mambo mawili yanayomsumbua. Tunaelezwa kuwa Dadi alingojea kwa hamu atwikwe mzigo wowote bila kujali uzito wake, madhali mtwikaji ni Mwanamaua. Mwanamaua anamfahamisha Dadi kuwa alivutiwa na huruma, ucheshi, ukakamavu na uhodari wake wa kazi. Maneno haya ya mapenzi ndiyo yanamwaminisha Dadi kuwa angeweza kumchezea Kipelele na kushinda ingawa hakuwa amewahi kucheza tena. Maneno haya ndiyo yanaonyesha nguvu za ushawishi wa mwanamke unaoweza kumtia mwanamume pabaya.

Katika hadithi ya ‘Ngondo Pangoni’ mandhari ya wakati wa usiku yanajitokeza. Hii ni kwa sababu mnamo saa tano za usiku, arusi ilikuwa imeshafikia kileleni. Watu wengi walikuwa wamefika; watoto, vijana na watu wazima. Watu hawa, wengi walikuwa na madhumuni mbalimbali: kuna wale waliokuja kutega mitego yao na wengine kulinda haki zao zisije zikachukuliwa. Hii ni kumaanisha ya kwamba jamii hii, watu walikuwa wametawaliwa na uzinzi. Kondo ni mmojawapo aliyekuwa tayari na mtego wake. Hii ni kwa sababu alijitenga kizani na kumwarifu mpenzi wake Sihaba. Mandhari ya wakati wa usiku yalifanikisha haya kwa sababu walipanga wakutane pangoni, mahali pa siri pa kujificha na kufanya mapenzi. Kwa sababu ya kiza waliweza kwenda pangoni huku wakijificha wasije wakaonekana. Pia katika hadithi ya “Ngondo Pangoni” mandhari ya usiku yanajitokeza kwa sababu tunaambiwa kulikuwa na mbalamwezi. Mbalamwezi ilitoa mwangaza ambao uliowaangazia wapenzi hawa mpaka wakafika pangoni. Hakuna mtu aliyewaona isipokuwa wanyama wa usiku walipokuwa wakifukuzana. Wapenzi hao hawakuwajali na kusahau yote na kutamani kwenda tu pangoni.

Mandhari haya ya usiku yanatufichulia jinsi wapenzi hawa walikuwa wanapendana. Pia yanatuonyesha jinsi ambavyo ndoa imeathiriwa. Hii ni kwa sababu mwandishi anatuonyesha watu katika ndoa hawaaminiani. Kuna baadhi wanaotoka nje ya ndoa kutafuta wapenzi wengine. Kwa mfano Kondo na Bi. Sihaba mkewe Jecha na Jecha na Bi. Mwamboje mkewe Kondo. Ni wazi kuwa familia hizi hawakuwa wanatosheka na wapenzi wao wa ndoa. Hivyo, walitoka nje ya ndoa na kufanya mapenzi na watu wengine. Hii ni kwa sababu Sihaba anamwambia Kondo kwamba anampenda kuliko Jecha kumi. Pia Sihaba alipitia shida nyingi njiani usiku huku akiogopa wanyama wa usiku na hatari za usiku kwa sababu ya mapenzi. Hivyo, tunaona familia hii inaathiriwa kwa sababu hakuna mapenzi ya dhati kwa waliofanya ndoa na kwa mke na mume.

Katika hadithi ya ‘Ngondo Pangoni’, mandhari ya usiku yanatuonyesha jinsi familia hizi mbili walifumaniana. Wote walipatikana peupe pangoni. Jecha na mke wa Kondo Mwamboje, Kondo na mke wa Jecha Bi. Sihaba. Ulikuwa unafiki wa hali ya juu. Hivyo wote walikuwa wamefumaniana na hakuna tena cha kuficha. Mambo yalikuwa wazi kwa marafiki hawa waliokuwa wanadang’anyana. Urafiki wao wa dhati haukuwa kati yao, bali kwa wake zao. Tunaonyeshwa ya kwamba huu ulikuwa unafiki kwa sababu wote walikaribishana pale pangoni na kuitana marafiki.

Katika hadithi ya ‘Mwungwana’, mandhari ya wakati wa usiku yanatufichulia kuwa ilikuwa saa nane za usiku ambapo Bwana Haji aligonga mlango nyumbani kwake na kumfumania mkewe wakifanya mapenzi na Kibwana. Kibwana alishtuka sana alipogundua kuwa ni sauti ya mngurumo wa kiume ukipiga hodi.

Hivyo, Saada mkewe Bwana Haji pia alishtuka na kuogopa kuwa angekuwa mumewe lakini alijipa moyo. Saada alijua kwamba kama angefumaniwa na mumewe ingekuwa balaa.

Katika hadithi ya ‘Mwungwana’, mandhari ya wakati wa usiku yanatuonyesha kuwa Saada alimpa moyo Kibwana na kumwambia asiogope, kwani aliyekuwa akibisha mlango si mumewe. Mandhari haya yanatueleza kuwa Saada alimpenda Kibwana hata kama hakuwa amemwoa. Tunaelezwa kuwa kuna hatari kubwa kwa wanandoa kwa sababu ndoa nyingi zinaharibika kwa sababu ya kutoaminiana.

Pia katika hadithi ya 'Mwungwana', mandhari ya wakati wa usiku yanatufichulia kwamba Bwana Haji alikuwa anampenda mkewe kwa dhati kwa sababu alishangaa kama kweli akimfumania ataweza kumkosa. Bwana Haji aliendelea na hali ile ya kushindwa ni vipi atafanya iwapo atamfumania mkewe lakini mkewe hakuachana na tabia yake ya umalaya. Mandhari haya yanatufichulia kuwa Bwana Haji alikuwa na msimano mkali pale aliamua kwamba akimfumania mkewe atamwacha mkewe na hatakuwa mkewe tena.

Mandhari haya ya wakati wa usiku yanatuonyesha kuwa Bwana Haji alikuwa Mwungwana. Hii ni kwa sababu aliamua akimfumania mkewe Saada, huo ndio utakaokuwa mwisho wake na Saada. Hii ni kweli kwa sababu baada ya kumfumania, hata mbele ya wazazi wa Saada, alikataa katakata kurudiana na Saada hata baada ya kubembelezwa na baba'ake Saada. Katika hadithi ya 'Mwungwana' mandhari ya wakati wa usiku yanatueleza kuwa jamii hii ilitia maanani urafiki kwa sababu hata kama ulikuwa usiku wa manane Saada alikubali kufungua mlango akifikiri ni Faraji rafiki yake Bwana Haji. Mandhari haya yanatuonyesha kuwa Saada alijali sana maslahi ya rafiki yao Faraji. Hii ni kwa sababu alikuwa tayari kumshughulikia ndio alikubali kufungua mlango.

Katika hadithi ya 'Uhuru wa Subira' mandhari ya wakati wa usiku yanatufichulia kwamba mnamo saa tano za usiku, mumewe Subira hakuwa amefika nyumbani. Hapa alipata nafasi nzuri ya kujifikiria zaidi. Alikuwa na chuki juu ya nafsi yake, hivyo, alifikiria la kufanya na afanye haraka kabla mumewe Mrisho hajarudi kwa sababu hangevumilia jela ya ndoa. Hivyo, tunaelezwa ya kwamba Subira alipanga kujiua kabla ya mumewe kurudi kwa sababu hangevumilia mateso anayoyapata kutoka kwa mumewe.

Katika hadithi ya 'Uhuru wa Subira' mandhari ya wakati wa usiku yanatuonyesha kuwa Mrisho alirejea nyumbani kwake kiasi cha saa kumi na nusu alfajiri. Mrisho ni mlevi wa kupindukia, kwa sababu anafika nyumbani saa kumi na nusu alfajiri. Mandhari haya yanatufichulia maudhui ya ulevi katika jamii, pale watu hawajali hata wakati wa kurudi nyumbani baada ya kulewa. Mrisho alikuwa anamtesa Subira kiasi kwamba hata jukumu lake la ndoa hakulitimiza.

Pia katika hadithi ya 'Uhuru wa Subira' mandhari ya wakati wa usiku yanatufichulia kuwa baba'ake Mrisho aliua mama'ake kwa sababu ya kufunga mlango. Hivyo,

tunaelezwa kuwa wanawake wanadhalilishwa kiasi kwamba hata mwanamke akiuawa hakuna shida. Mandhari haya yanatueleza kuwa, hapo mbeleni baba'ake Mrisho aliua mama'ake kwa sababu ya kutofungua mlango. Hivyo, tunaelezwa kuwa jamii ilikuwa na uozo mwingi ambao ulichangia vifo hasa vya wanawake. Ulevi ulisababisha baadhi ya vifo hivyo.

Katika hadithi ya 'Sadiki Ukipenda' mandhari ya wakati hasa usiku yanatufichulia kuwa wachawi walifanya kazi yao ya kuroga watoto na vijana usiku. Usiku unalinganishwa na uovu wa wachawi kutekeleza maovu yao. Hii ni kwa sababu usiku kuna kiza na kiza ni ishara ya maovu. Usiku wa manane ndio wakati wachawi walikuwa wanafanya kazi yao. Pia tunaelezwa kuna ngoma iliyokuwa ikipigwa wakati huo tayari kukaribisha wakati wenyewe wa kufanya shughuli zao za kichawi.

### 2.4 Hitimisho

Katika sura hii tumetathmini mandhari ambayo ni kipengele cha fani. Tumechunguza mandhari ya mahali kwa kuangazia mandhari ya mashambani, mandhari ya nyumbani na mandhari ya danguroni.

Katika mandhari ya mahali tumeona ya kwamba maudhui mengi yanawasilishwa kama vile ya ndoa na mapenzi, usaliti katika ndoa, kudhalilishwa kwa mwanamke miongoni mwa maudhui mengine.

Tumechunguza pia mandhari ya wakati. Katika mandhari ya wakati tumechunguza mandhari ya wakati wa asubuhi, mchana na usiku. Katika mandhari ya usiku maovu mengi huwa yanafanyika. Hii ni kwa sababu ya kiza ambacho kinahusishwa na maovu.

Kutokana na kipengele cha mandhari maudhui mengi yamejadiliwa kwa kuwa matukio sharti yatekelezwe wakati fulani na mahali fulani.

# SURA YA TATU

# NAFASI YA WAHUSIKA KATIKA KUFANIKISHA UWASILISHAJI WA MAUDHUI

## 3.1 Utangulizi

Kwenye sehemu hii tumeshughulikia kipengele muhimu sana ambacho ni wahusika. Kipengele hiki kimetumika katika kufanikisha uwasilishaji wa maudhui katika diwani za Said A. Mohamed. Wahusika mbalimbali huwasilishwa kwa kutumia usanii ili waweze kukuzwa kikamilifu. Hadithi fupi huwa na idadi ndogo ya wahusika. Hadithi hizo hujifunga katika tukio moja tu. Ili kulikuza tukio au tendo hilo, wahusika huwa wachache.

Kuwepo kwa wahusika wengi huhitaji muda, kipindi na wakati wa kuwakuza na kuwaendeleza, wakati ambao mwandishi wa hadithi fupi hana. Usawiri wa wahusika katika hadithi fupi hutathminiwa kwa kutumia vigezo vifuatavyo: wawe thabiti katika tabia zao, wasibadilikebadilike ila panapokuwa na sababu nzuri. Sababu za matendo yao ziwe wazi na za kuaminika. Lugha ya wahusika inatakiwa ishabihiane na ile ya watu halisi wa jamii inayohusika. Jukumu la kila mhusika katika hadithi liweze kubainika.Kwa ujumla, wahusika wawe wa kusadikika katika tabia na matendo yao (Mwenda Mbatiah 2000).

Katika hadithi hizi teule kuna wahusika wakuu na wahusika wadogo kutegemea wadhifa wao katika kazi husika. Wahusika hawa wanatumiwa na mwandishi katika kufanikisha uwasilishaji wa maudhui.

## 3.2 Wahusika Wakuu

Katika sehemu hii tulishughulikia wahusika wakuu. Wahusika wakuu katika hadithi fupi za Said A. Mohamed ni viumbe ambao wanapatikana kutoka mwanzo hadi mwisho wa hadithi. Mwandishi ametumia wahusika hawa katika kufanikisha uwasilishaji wa maudhui (Madumulla 1991) anasema kuwa matendo na wasifu wa mhusika mkuu yanachukuana na hali ya kawaida ya maisha ya jamii, na ambaye matakwa yake na malengo yake kwa namna fulani yanaoana na kilio cha walio wengi na kudhihirisha hofu na matumaini yao.

Naye Mbatiah (2001) anasema mhusika mkuu huonekana wazi kuwa ndiye nguzo ya msimulizi kwa kuwa ndiye muhimu kuliko wengine wote. Anahusika na matukio makuu ya hadithini. Wahusika wengine wanahusishwa naye na wanasaidiana kumjenga. Wanafasihi hawa wote wanakubaliana kuwa kuna mhusika mkuu na majukumu yake ni muhimu kutupatia ujumbe katika kazi ya fasihi. Katika hadithi fupi za Said A. Mohamed tutachunguza wahusika wakuu na wadogo na jinsi wanavyofanikisha uwasilishaji wa maudhui. Wahusika wakuu wa hadithi fupi huwa bapa kwa kuwa utanzu hauwapatii nafasi ya kukua. Mwandishi anawaelekeza kwa lengo maalumu, hasa kuhusu maadili fulani ya kijamii. Wahusika hawa wakuu wamebuniwa kuzingatia na kutenda matendo yanayooana na sifa walizopewa.Wanashika papo kwa papo bila kubanduka na bila kubadilika.

### 3.2.1 Mzee Siwa katika 'Sadiki Ukipenda'

Mzee Siwa ni mmoja wa wahusika wakuu. Mhusika huyu anatawala hadithi hii kutoka mwanzo mpaka mwisho. Mzee Siwa alikuwa akisema ukweli. Hii ni kwa sababu tunaambiwa kuwa Mzee Siwa si mtu wa kusema uongo. Hii ni kwa sababu tunaelezwa kuwa kwake, neno ni deni kubwa kuliko deni la fedha. Mzee Siwa alimwambia Mussa kuwa baba yake ni mchawi na kweli baba yake Mussa alikuwa mchawi kwa sababu alitaka kumroga pamoja na wachawi wengine lakini Mussa alimuua kabla hajatimiza lengo lake.

Pia Mzee Siwa alikuwa shujaa. Hii ni kwa sababu mwandishi anatufichulia kuwa penye haki Mzee Siwa husimama kidete bila ya kutetereka wala kuwa na hofu ya mtu yeyote, mkubwa au mdogo. Mzee Siwa hakuogopa kumwambia Mussa kuwa baba yake ni mchawi asadiki akipenda. Kauli hii pia imechangia ufaafu wa anwani ya hadithi hii. Hii ni kwa sababu ilikuwa vigumu sana kumwambia Mussa jambo hili, ndio sababu alikuwa akitumia tambuu. Matumizi ya tambuu yalimwongezea Mzee Siwa maarifa fulani alipokuwa akiamua jambo muhimu. Hivyo,hakuogopa kumwambia Mussa jambo hili kwa sababu ya ushujaa wake.

Mzee Siwa alikuwa mkarimu. Mwandishi anatueleza kuwa daima alikuwa tayari kugawa mafungu chochote alichokuwa nacho, ijapokuwa ndicho hichohicho. Hii ni kwa sababu alikuwa tayari kumweleza Mussa kuwa baba yake ni mchawi na hangejiwekea hayo

pekee, hivyo ilimbidi amwambie Mussa na amwelekeze jinsi angejiokoa kutokana na ukatili wa baba yake na wachawi wengine. Tunaona ukarimu wake kutokana na jinsi alivyokuwa tayari kumwokoa Mussa kutokana na ukatili huo.

Pia alikuwa hodari na mkakamavu kwa kazi yake. Mwandishi anatueleza kuwa shamba lake ndilo lililokuwa kubwa kuliko shamba la kijana yeyote pale kijijini mwao. Hivyo Mzee Siwa alikuwa mkulima hodari na jamii yake ilikuwa inategemea kilimo kwa mahitaji ya chakula.Pia Mzee Siwa alikataa kujiumiza na umaskini wa hali ya juu. Hivyo alitia bidii katika kazi yake ya ukulima ili ajiondolee umaskini. Hivyo Mzee Siwa aliupinga umaskini ambao unaangamiza wanajamii.

Mzee Siwa alikuwa mwenye busara. Hii ni kwa sababu mwandishi anasema kuwa ulimi wake daima ulikuwa nasaha. Mwandishi anaendelea kusema kuwa kichwa chake kilikuwa maarifa. Shauri lake ni busara na mwongozo wake ni mwangaza katika maisha. Mashauri ya Mzee Siwa yalimfaa sana Mussa kwa sababu ya shida nyingi vijana kama yeye walipitia. Hii ni kwa sababu Mzee Siwa aliwashauri vijana waliokabiliwa na vikwazo vya choyo, wivu, jitimai na msiba kwa jumla. Vijana walipata shida nyingi kwa sababu tunaelezwa na mwandishi kuwa Mussa aliposafiri kwa meli alipatana na vijana wenzake ambao walikuwa wametoroka nchi zao na kuhamia nchi nyingine.

Mzee Siwa alikuwa mcha Mungu. Tunaona Mzee Siwa akiomba. Alimhimiza Mussa kutekeleza faradhi ya sala. Hii ni kwa sababu Mzee Siwa anamwambie Mussa amwache asali na kutaka kujua kama Mussa ameshasali.

Mzee Siwa alikuwa na sifa za kichawi. Hii ni kwa sababu alikuwa akitumia tambuu. Matumizi ya tambuu yalimwongezea Mzee Siwa maarifa katika kusema mambo. Hii ni kwa sababu baada ya kutumia tambuu aliweza kuamua jambo hataka kama ni jambo gumu na muhimu. Mzee Siwa ni mnafiki kwa sababu anajifanya mcha Mungu ilhali ni mchawi.

### 3.2.2. Mussa katika ‘Sadiki Ukipenda’

Mussa ndiye msimuliziwa kisa hiki. Mussa alikuwa kijana msomi. Hii ni kwa sababu baba yake Mussa na wachawi wengine wamepanga kumuua kwa sababu ni msomi. Jamii hii haitaki vijana kuendelea na masomo yao. Hii ni kwa sababu wanaogopa wasomi kuwa

watawasumbua hasa wachawi. Tunaelezwa kwamba wachawi wanaogopa kwamba vijana wakisoma watagundua njama zao na mwishowe kuwamaliza.

Mussa alikuwa mwaminifu na hakupenda kusema uongo. Hii ni kwa sababu Mzee Siwa alipokuwa akitaka kumwambia siri juu ya baba yake kuwa ni mchawi na anataka kumwondoa ulimwenguni, inaonekana Mussa akishangaa kwa nini Mzee Siwa hataki kumwamini. Mussa alibabaika na kujibu kwamba hajapata Mzee Siwa kutomwamini hata siku moja. Hivyo, Mussa alikuwa kijana ambayae hatoa siri nje ndio maana alifaulu pamoja na Mzee Siwa kwa mambo waliyoyapanga kumwokoa dhidi ya ukatili wa baba yake wa kumuua pamoja na wachawi wengine.

Mussa alikuwa na busara. Hii ni kwa sababu alipoambiwa na Mzee Siwa kuwa baba yake ni mchawi, kuna maswali alikuwa anataka kumuuliza lakini akasema alihisi huo haukuwa wakati wake. Pia Mussa alizingatia yale yote alikuwa ameambiwa na Mzee Siwa juu ya mpango wa kukabiliana na baba yake na mwishowe aliweza kufanikiwa kujiokoa kutokana na ukatili wa baba yake na wachawi wengine. Hivyo baba yake na wachawi wengine hawakufaulu. Mussa alijitia moyo mpango wake wa kutoka nje ulielekea kufanikiwa hivyo aliende kwa Mzee Siwa kwa mawaidha. Mussa anasema hilo lilikuwa jambo la busara, kwa maana wachawi hawatasita kujaribu tena na tena kumwondoa duniani.

Mussa alikuwa mwenye kisasi. Hii ni kwa sababu anasema hakuwaza jambo jingine ila kisasi. Hakuogopa hata kama yule aliyekuwa akimfuata kumdhuru alikuwa baba yake hakujali kwa sababu huyo baba alitaka kuitoa roho ya mwanawe. Mussa alimuua baba yake akijaribu kujiokoa kutokana na ukatili wa baba yake na wachawi wengine.

Mussa alikuwa mnafiki. Hii ni kwa sababu alipotekeleza wajibu wake aliende kulala chumbani mwake lakini hakupata usingizi kamwe na jimbi la saa kumi za alfajiri lilipowika, aliinuka kutawadha na kusali. Huu ni unafiki kwa sababu hata kama alikuwa anasali moyoni alikuwa na chuki nyingi. Pia alimuua baba yake alipokuwa akijiokoa kutokana na ukatili wa baba yake na wachawi wengine. Unafiki unajitokeza zaidi pale anasema aliomba Mungu amhifadhi na kumzidishia maisha marefu.

Mussa alikuwa na matumaini ya maisha yake. Hii ni kwa sababu anasema asilaumiwe kwa kuua baba yake. Tena Mussa anasema ana furaha kubwa. Anasema amesafiri kuona ulimwengu mwingine kwa sababu ulimwengu alipo umemshinda na angependa kurudi pale atakapokuwa mtu kamili na atakapokuwa huru pamoja na roho yake.

### 3.2.3 Kondo katika 'Ngondo Pangoni'

Kondo ni mumewe Bi. Mwamboje na rafiki yake Jecha. Kondo alikuwa mwenye majisifu. Tunaelezwa kuwa Kondo, "bwana mmoja shababi ambaye kwake majisifu yalikuwa ni kitu cha kawaida". Majisifu ya Kondo yalimfanya kufanya mapenzi na mke wa rafiki yake Jecha Bi. Sihaba. Pia Kondo alikuwa mwenye ulaghai. Mwandishi anatueleza kuwa alikuwa mlaghai kwa sababu ulaghai ulikuwa ni ibada kubwa kwake. Ulaghai wa Kondo ulimfanya amdanganye rafiki yake Jecha kwamba hataenda arusini ilhali alikuwa anaingojea kwa hamu na ghamu. Pia alikuwa akifanya mapenzi na mke wa rafiki yake Jecha.

Kondo alikuwa domo kaya. Hii ni kwa sababu walipokutana na rafiki yake Jecha walikuwa wakizungumzia juu ya wanawake waliofanya na wao mapenzi. Hivyo, Kondo alikuwa msherati. Kondo alikuwa akifanya uasherati na mwanamke yeyote. Hii ni kwa sababu tunaelezwa na mwandishi kuwa hakukuwa na kitu chochote walichokipata, licha kukila! Hii ndio sababu kubwa iliyostawisha na kuimarisha urafiki wao ulioishi kwa miaka.

Kondo alikuwa msiri. Tunaambiwa kwa kuwa kuishi kwao na Jecha hakukuwa na siri iliyokuwa ya mmoja wao peke yake. Tunaambiwa walipeana yote yaliyokiwa moyoni mwao, ila moja tu. Hilo lilikuwa siri ya kwamba Kondo alikuwa na urafiki wa mapenzi na mkewe Jecha. Siri hii Kondo aliiweka na aling'ang'ania useme roho yenyewe ambayo akiitoa basi ameukata uhai wake. Hii ni kumaanisha kwamba siri hii hakuna angesema, labda mtu atolewe uhai itoke yenyewe lakini hakuna angeweza kusema lolote kuhusu siri hii.

Kondo alikuwa akitumia tambuu. Tambuu ilimwongezea maarifa fulani zaidi alipotaka kuamua jambo ambalo lilikuwa ngumu kulisema. Baada ya kutumia tambuu Kondo alimweleza rafiki yake Jecha kwamba watu walikuwa wameanza kushuku urafiki wao.

Kondo alikuwa ameanza kusikia fununu kuhusu unafiki wao wa kufanya mapenzi na mke wa rafiki yake Bi. Sihaba.

Kondo alikuwa mtani. Hii nikwa sababu walikuwa wanataniana na Jecha ili kuficha ukweli kwamba watu waliwashuku kwamba Kondo anafanya mapenzi na Bi. Sihaba mkewe Jecha rafiki yake. Pia Kondo alimtania Bi.Sihaba walipokuwa wanaenda pangoni. Alimwambia Bi. Sihaba kwamba anajua anampenda kupita kiasi 'nimeoza' anamwambia asije akanuka tu.

Kondo alikuwa mzinzi. Tunaambiwa baadhi waliokuwa na mitego yao, mmoja alikuwa Kondo. Alipanga pamoja na Bi Sihaba waende arusini ndio wapate nafasi ya kufanya mapenzi. Kondo alinyerereka na kujitenga kizani ndio waende na Bi. Sihaba pangoni kufanya mapenzi. Kondo alikuwa na hamu kuu ya mapenzi kwa Bi.Sihaba kwa sababu alivumilia kiza cha usiku na kwenda pangoni. Hii ni kwa sababu tunaambiwa Bi. Sihaba na Kondo walipopatana wao wakasonga mbele, wamesahau yote ya dunia iliyowazunguka na kukumbuka moja tu hisia za pangoni. Kondo wakiwa na Bi. Sihaba walifumaniwa na Jecha na Bi. Mwamboje.

Kondo alikuwa mnafiki kwa sababu baada ya kufumaniwa alimkaribisha Jecha na Bi. Mwamboje pangoni pale anamwambia 'na huyu hapa Bi. Sihaba, mkeo....karibu, karibu, karibu pangoni Bwana Jecha. Wewe na Bi. Mwamboje na mimi na Bi. Sihaba....wake na waume wazuri au sivyo?.....karibuni' (uk. 25) huu ulikuwa unafiki wa hali ya juu.

### 3.2.4 Jecha katika 'Ngondo Pangoni'

Jecha ni mumewe Bi. Sihaba na rafiki yake Kondo. Jecha alikuwa mwongo. Hii ni kwa sababu mwandishi anatwambia Jecha ni mwongo kupita kiasi na mwenye kubeza kila kitu. Alimdanganya Kondo kuwa hataenda arusi ya mwanawe Jabu lakinihiyo arusi alikuwa anaingojea kwa hamu na ghamu ili wakutane na Bi. Mwamboje.

Jecha hakuwa nadhifu, kwa sababau mwandishi anatuambia kuwa nguo zake ni matambara yasiyofuliwa na sana shati lililomganda mwilini kama kigaga. Shati alipenda kulitolea nje na kulipuuzia juu ya shuka yake. Hivyo hakuonekeana kuvutia. Pia hakuvaa kofia. Upara wake katikati ya utosi ulionekana kama kinoo kilichopakwa maji kikingojea kunolea. Pia mchanganyiko wa nywele nyeusi na nyeupe zilipiga pande pembe na hii ya

upara wenyewe, bila ya kuthubutu kuchanganya kasi na kuotea juu yake. Hivyo hakuthamini usafi.

Jecha alikuwa msherati na mwenye umbea. Hii ni kwa sababu walipokutana na Kondo mazungumzo yao yalikuwa juu ya wanawake waliofanya na wao mapenzi. Jecha hakuficha Kondo chochote alichopata. Alikuwa akimwambia kila kitu hakukuwa na kitu chochote walichokipata, licha kukila. Labda hii ndiyo sababu kubwa iliyostawisha na kuimarisha urafiki wao ulioishi kwa miaka. Pia Jecha alikuwa domo kaya na mwenye majisifu. Hii ni kwa sababu tunaambiwa mradi mara nyingine ni lile domo kaya na majisifu yao tu.

Jecha alikuwa msiri. Tunaambiwa kuwa katika kuishi kwao na Kondo, hakukuwa na siri iliyokuwa ya mmoja wao peke yake. Tunaambiwa walipeana yote yalikuwa moyoni mwao,ila moja tu. Hilo lilikuwa siri ya kwamba Jecha alikuwa na urafiki wa mapenzi na mkewe Kondo. Siri hii Jecha aliweka na aling'angania useme roho yenyewe ambayo akiiweka basi amekukata uhai wake. Hii ina maana kuwa siri hii haingetolewa hivi labda mtu atolewe uhai.

Jecha alikuwa mnafiki. Jecha alikuwa na mengi ya kufanya lakini kwanza apate kusali. Hii ni kwa sababu Jecha kila siku aliyaamini yale maneno ya ukwepaji wa hali ngumu kwa sababu kweli dunia Jecha ilimwendea Kombo kweli kweli, sikwambii, dini yake. Msala aliujua na kuinama na kuinuka kutwa mara tano hakukumpita kwa hilo, anastahiki sifa kwa uwezo au sifa alizopewa na Mungu. Pia tunaambiwa alipokwisha kusali, Jecha alikimbilia ukumbini. Unafiki wa Jecha unajitokeza pale anatekeleza wajibu wa sala ilhali moyoni mwake alikuwa amepanga kwenda arusini ili wakutane na Bi. Mwamboje kufanya usherati. Hivyo, huu ulikuwa unafiki.

Jecha alikuwa mwenye chuki. Hii ni kwa sababu alikuwa anamchukia Jabu kwa sababu Jecha na Jabu walikuwa wanang'ang'ania kuoa Bi. Sihaba lakini Jabu alipata mke mwingine na Jecha akamwoa Bi Sihaba. Bi Sihaba anashangaa kwa nini chuki hizi haziishi na kila mtu anaendelea vizuri na familia yake. Jecha alikuwa anataka wapatane na Jabu ndio apate nafasi ya kwenda arusini. Tunaambiwa kwamba Jecha anasema ugomvi usio msingi hauna maana anaona leo bora akapatane na Bwana Jabu kwa maana

ameshaoa Bi. Sihaba kwa sababu anasema "chombo ni changu maisha...". bora nende kushangiria arusi ya mwanawe (uk 19) kauli hii inatueleza kuwa Jecha alikuwa tayari kwenda arusini ili alitimiza jambo lililokuwa likimsumbua moyoni. Jambo hili ni kukutana na Bi Mwamboje iliwafanye mapenzi.

### 3.2.5 Subira katika 'Uhuru wa Subira'

Subira ni mkewe Mrisho na Binti wa Mzee Farijala na Biti Shomari. Subira alikuwa mwenye subira. Hii ni kwa sababu alisubiri sana ili apate uhuru wake lakini hakuupata. Mumewe Mrisho alimtesa sana na pia baba yake. Tunaelezwa kuwa anapokumbuka zama zake hulia. Hulia kilio cha kwikwi na machozi njia mbilimbili. Naye anatakiwa kusubiri, ataraji na kungojea kafiri kusilimu jambo ambalo ni gumu sana. Tunaelezwa kuwa zama zake alipokuwa Subira, alikuwa na nguvu mwilini. Hii ina maana kwamba, Subira alikuwa amesubiri kwa muda mrefu ili apate uhuru wake maana alikuwa amedhalilishwa na mumewe Mrisho na baba yake Mzee Farijala.

Subira alikuwa mvumilivu. Hii ni kwa sababu alivumilia mateso ya mumewe Mrisho na baba yake. Subira alikuwa akipigwa sana na baba yake aliporejea nyumbani kushtaki Mrisho kwamba anamtesa. Baba yake Subira anasema kwamba wendapo akijitia wazimu tena nakuapia Mungu, kichwa chake kitakuwa halali yangu. Tunaelezwa kuwa baada ya pigo hili alilopigwa siku hiyo na baba yake. Hivyo, baba yake Subira alikuwa amezoea kumpiga Binti yake Subira baada ya kurejea nyumbani akidai uhuru wake. Subira alikuwa anavumilia kwa sababu alikuwa ameteswa sana na mumewe Mrisho na alikuwa anataka waachane. Hii ni kwa sababu aliona kuolewa ni kama kuwa katika jela.

Subira alikuwa amekonda na kukondeana kwa sababu ya mateso ya mumewe Mrisho na baba yake mzazi. Subira alikuwa na umri wa makamu lakini hakuwa na siha nzuri. Tunaelezwa kuwa si viroja kabisa kumwona Subira leo fupa la uso limemsimama, mashavu yamemshoboka, macho yamemkodoka na kidari kimemwinuka. Hivyo Subira alikuwa hana afya nzuri na alikuwa amekonda kwa sababu ya mateso.

Subira alikuwa mfadhili wa Simba mbwa wao. Tunaelezwa kuwa Subira toka hapo zamani kabla hajaolewa alijisalimisha na kumsujudia namna hiyo. Hii ni kwa sababu Subira alikuwa mfadhili mkubwa wa Simba. Tunaambiwa kuwa hakukosa kumdhukuru

mabaki ya vyakula na hilo likageuka mapenzi. Simba alipoambiwa na Subira kwamba amekonda kama yeye, Simba aliinamisha uso wake chini na kuacha kutikisha mkia wake. Hilo lilikuwa zito kwa Subira, 'kwasababu alihisi anachomwa mwiba wa huzuni. Ilimwathiri kuona kwamba mbwa alikuwa akimhurumia zaidi kuliko mumewe na babaake. Hivyo mbwa alimpenda zaidi ya mumuwe na baba yake.

Subira alikuwa mwenye hasira. Hii ni kwa sababu, Subira alikuwa amekasirika pale alisema alijiona anapanda uchungu, joto na jeuri kinywa chake ambacho siku zote alikifumbua na kujizuia kumjibu baba yake au mama yake. Siku hiyo kilikataa kufumba, kilifunguka kwa ghafla. Hapa ni pale alisema kwa hasira kuwa hataenda, hatarudi bali anataka talaka yake na uhuru wake. Subira alisema kwamba madhila yamekuwa makubwa, unyonge umepindukia mipaka. Hivyo Subira aliona hana hila ila adai uhuru wake kwa mabavu. Pia hasira yake ilimfanya kuwa na kisasi na chuki. Hii ni kwa sababu tunaambiwa kuwa Subira alipoamka mnamo saa tano za usiku baada ya kurudi kwake na kupigwa sana na baba yake alihisi kisasi na chuki juu ya nafsi yake. Maneno hayo yalimkumbusha la kufanya. Na tena bora alifanye wakati huo kabla mumewe hajarudi. Hivyo, Subira aliamua kijitia kitanzi kwa sababu ya chuki na kisasi juu ya nafsi yake. Mwandishi anatueleza kwamba Subira alikuwa amekasirika sana hivyo hangevumilia tena jela la ndoa. Hii ni kwa sababu alikuwa ameteswa sana na mumewe na baba yake Mzee Farijala.

### 3.2.6 Mrisho katika 'Uhuru wa Subira'

Mrisho alikuwa mumewe Subira. Mrisho alikuwa anamtesa sana Subira. Hiini kwa sababu Subira alikuwa anarejea kwao kudai uhuru wake ili waachane na Mrisho. Mrisho alikuwa akidhalilisha mkewe. Hivyo, Mrisho alimdhulumu mkewe kwa kumtesa hadi Subira anarejea kwao kila wakati kudai uhuru wake. Mateso ya Mrisho kwa Subira yalisababisha kifo cha Subira. Mrisho alikuwa anadhalilisha wanawake. Hii ni kwa sababu baba yake Mrisho aliua mama yao kwa kosa la kutofungua mlango. Hii ni kumaanisha kwamba mwanamke hakuwa na uhuru kama wa mwanaume.

Mrisho alikuwa mlevi wa kupindukia. Hii ni kwa sababu tunaelezwa kuwa Mrisho alirejea kwake kiasi cha saa kumi na nusu alfajiri, na kama kawaida alikuwa chaa! Au

chordo, walichoona watu. Alipofika kwake mlango wakewa nje ulikuwa umefungwa. Mrisho aliita kwa nguvu huku akigonga mlango na kukokoteza sauti yake ya kilevi.

Mrisho alikuwa mwenye majuto. Hii ni kwa sababu baada ya kugundua ya kwamba Subira amejitia kitanzi hata ulevi ulimruka. Tunaelezwa kuwa alipata mshitukoMrisho. Subira alitumia Kanga kujitoa uhai wake. Mrisho ulevi ulimruka. Tunaelezwa kuwa mwili ulimnyongonyea na miguu ikakataa kushika, akaporomoka. Hakujijua tena. Hivyo, Mrisho alipoteza fahamu baada ya kuona maiti ya mkewe. Hii ni kumaanisha kwamba Mrisho alikuwa anajuta kwa sababu kifo cha Subira kilitokana na mateso aliyomfamfanyia.

### 3.2.7 Bwana Haji katika 'Mwungwana'

Bwana Haji ni mumewe Saada. Bwana Haji ni mwungwana. Hii ni kwa sababu Bwana Haji alionyesha kutobadilisha nia yake ya kumwacha Saada iwapo atamfumania. Tunaelezwa ya kwamba hata baada ya kumfumania mkewe na Kibwana, hakukasirika au hakumpiga mkewe au  mume mwenziwe, alijifanya mwungwana kabisa. Pia baada ya Kibwana kutoka, hakumuuliza mkewe chochote.

Bwana Haji alikuwa mnafiki. Unafiki wa Bwana Haji unajitokeza kwa sababu anaelewa kwamba Kibwana yuko nyumbani kwake lakini anajifanya kana kwamba kila kitu ki sawa. Hii ni kwa sababu hata anamdanganya mkewe kuwa hakwenda pwani lakini tunaelewa kuwa alirudi kimakusudi ili amfumanie mkewe. Unafiki wa Bwana Haji unajitokeza zaidi pale alipomkuta Kibwana chumbani mwake alijifanya hakuna ubaya wowote na kumwambia aendelee kustarehe na hata kumwita mgeni wake. Bwana Haji alimwambia Kibwana anaweza kuendelea kustarehe kwa sababu ana chumba kingine ambacho anaweza akalala huko na kweli alifanya hivyo, lakini moyoni alikuwa anaumia sana kwa sababu hata alipoingia chumba kingine kulala hakulala kwa sababu alisikia Kibwana akitoka.

Bwana Haji alikuwa na msimamo mkali.Bwana Haji akiamua jambo lazima alitimize. Bwana Haji alimpa mkewe talaka baada ya kumfumania. Pia Bwana Haji alisema na kujadili na moyo wake kwamba alikiri kumtema Saada kama alivyommeza. Moyo wake

ukimuahidi Haji kwamba, pindi akimwacha Saada, hautomchagiza kuramba matapishi aliyokwisha yatapika.

Bwana Haji alikuwa anampenda mkewe Saada. Hii ni kwa sababu tunaelezwa ya kwamba alipofunguliwa mlango na mkewe akifikiria ni rafiki yao Faraji, moyoni alikuwa na mambo mawili ambayo yalimpa ugumu wa kutenda. Kwanza utete wa moyo wake mwenyewe uliolemaa na kukubali kuzugwa na mwanamke aliyempenda na kumfia damu. Anashangaa kweli akimfumania Saada atawezaje kumkosa. Hata hivyo, tabia za Saada ziliendelea kumkera na kumtia kichefuchefu na kizunguzungu kikali.

Bwana Haji alikuwa mwenye busara. Hii ni kwa sababu kabla amue kumpa mkewe talaka alikuwa amejadiliana na moyo wake na kuamua iwapo atamfumania atamwacha kama alivyompenda. Pia alikuwa amesikia nong'ono za vitendo na uhaini wa mkewe zamani. Hii ni kumaanisha alimpa mkewe muda wa kubadilisha tabia zake lakini akaona ya kwamba, bado mkewe anaendelea na tabia zake mbaya. Pia alisema itakuwarahisi kumtia mkononi iwapo ataendelea na vitendo vibaya. Bwana Haji alikuwa mwenye busara kwa sababu pia alibadilisha sauti yake na kuiga sauti ya rafiki yake Faraji. Hii ni kwa sababu alijua kama angesema ni yeye Saada hangefungua mlango. Pia Bwana Haji alitumia busara kujifanya ameenda Pwani lakini akirudi usiku wa manane wakati anajua kama kweli Saada anashiriki uasherati atampata. Pia Bwana Haji anawaita wazazi wa Saada kisirisiri ili awajulishe kwa vitendo tabia za Binti yao. Hii ni kwa sababu wazazi walitaka kujua Bwana Haji amemfanya nini Saada, lakini Bwana Haji akawaelezea kuwa ni Saada aliyemsaliti bali si yeye.

Bwana Haji alikuwa anawajibikia mkewe. Hii nikwa sababutunaelezwa kuwa Bwana Haji anasema kila kitu ni dhiki katika dunia hii. Hii ni kwa sababu wanataka kula tena kula vinono kama anavyohimiza Saada, wanataka kuvaa, kuvaa kwa fahari kama anakong'ang'ania Saada. Bwana Haji anasema mengi,mengi anayependa kumtekelezea mkewe, na hajapata kumhini lakini anasema haidhuru. Hivyo, tunaelezwa kuwa Bwana Haji alikuwa anamtimizia mahitaji yote kama mumewe. Mahitaji hayo ni kama chakula, mavazi, nyumba nzuri na mahitaji mengine ya ndoa.

### 3.2.8 Saada katika 'Mwungwana'

Saada ni mkewe Bwana Haji. Saada alikuwa msherati. Tunaelezwa kuwa Bwana Haji alikuwa ameanza kusikia nong'ono za vitendo na uhaini wa mkewe hapo zamani. Kwa hivyo, Bwana Haji alipanga jinsi atakavyomfumania mkewe. Alijifanya ameenda Pwani lakini baadaye akarudi usiku wa manane na kweli alimfumania Saada na Kibwana wakifanya mapenzi.

Saada aliogopa mumewe. Hii ni kwa sababu wakati mlango uligongwa alishtuka sana na kusema si sauti ya mumewe. Anasema ingalikuwa hiyo sauti ni la Bwana Haji, ingalikuwa balaa. Hii inamaanisha alikuwa anamwogopa mumewe na hangetaka amkute wakifanya mapenzi na Kibwana. Pia Saada anamwambia Kibwana apoe kitandani kwani sauti ile si ya mumewe. Pia baada ya kukaa kwa siku sita, bila Bwana Haji kusema neno, Saada alihisi bora angepigwa au angechinjwa kuliko kuachwa sesa namna ile.

Saada alikuwa anajali na kuthamini urafiki. Hii ni kwa sababu ulikuwa usiku wa manane lakini anamfungulia rafiki yao Faraji. Tena anataka kujua shida zilizomleta usiku wa manane. Tunaelezwa kuwa Saada alikuwa tayari kumshughulikia hata kama ulikuwa usiku wa manane. Hivyo alijali na kuthamini urafiki. Pia Saada alikuwa rafiki wa Kibwana. Kibwana hakuwa mumewe wa ndoa lakini alimpenda kwa dhati kwa sababu tunaelezwa kuwa baada ya kusikia sauti ya mngurumo wa kiume, Kibwana alishtuka sana. Saada alimgeukia Kibwana na kwa madoido na hashuo la kike alimpa ishara ya siri kwa unyusi wa kupandishia uliorejesha na kukoloza tena hamu ya Kibwana iliyomfifia kwa woga wa kufumaniwa. Tena Saada anamwambia Kibwana apoe kitandani. Kwa kumtia moyo na kumwambia asiogope wala asijali hakuna chcochote kingevunja starehe yao. Hivyo, Saada alikuwa rafiki wa Kibwana. Hii ni kwa sababu Saada hakutaka Kibwana angaike kwa kuogofia kufumaniwa na Bwana Haji.

### 3.2.9 Mwanamaua katika 'Mhanga wa Mwanamaua'

Mwanamaua ni mchumba wa Dadi. Kuna kutilia mkazo ufaafu wa jina la mhusika Mwanamaua kwamba anapendeza. Kivutio kingine ni kuwa hili ni jina la Kinga analokabidhi msichana anapozaliwa Kisiwani pemba. Mwanamaua anavutia wanaume wengi kwa urembo na tabia yake.

Mwanamaua alikuwa mwenye mapenzi ya dhati kwa Dadi. Tunaelezwa kuwa Mwanamaua anamwambia Dadi kwamba anajua anampenda na amekubali kuolewa na Dadi miongoni mwa vijana wote wa kijiji hicho. Dadi alitambua kwamba Mwanamaua aliwakataa na kuwaepuka wote. Mwanamaua anamfahamisha Dadi kuwa alivutiwa na huruma, ucheshi, ukakamavu na uhodari wake wa kazi. Maneno haya ya mapenzi ndiyo yanamwaminisha Dadi kuwa angeweza kumchezea Kipelele ingawa hakuna amewahi kucheza tena. Pia Mwanamaua anakubali kwenda usiku kwenye kiza ili amtafute Dadi ndio wafanye mapenzi. Walifanya mapenzi msituni ili wasionekane huku wakijificha.

Mwanamaua alikuwa mkaidi. Hii ni kwa sababu tunaelezwa kuwa Mwanamaua ana uovu katika nafsi yake. Uovu wake wa dhahiri umo katika nguvu za ndani zinazomsukuma mtu kufanya kitu na ukaidi wake. Hasemezeki wala haambiziki. Tunaelezwa tokea utoto wake akishikilia kashikilia. Hakubali wala hatulii mpaka afanikiwe au labda patolewe mhanga au chano. Kauli hizi ni kweli kwa sababu Mwanamaua hakutulia mpaka Dadi aliposhawishika na kukubali kumchezea ng'ombe Kipelele. Tunaona labda alitulia wakati alihakikisha kwamba Dadi ameuawa na Kipelele.

Mwanamaua hakuwa mwoga. Hii ni kwa sababu alitoka usiku peke yake. Tunaelezwa kuwa aliukabili mwili mzima wa kiza bila ya hofu. Hakuwa na hofu ya kiza kwa sababu kiza ndio kitu alichokuwa akikitaka. Hii ni kwa sababu hakutaka kuonekana na mtu yeyote akitoka usiku na kutimiza uovu wake wa usiku. Hii ni kwa sababu Dadi alikuwa anamngoja kichakani ili wafanye mapenzi. Tunaelezwa kuwa alipomkuta Dadi, Dadi alimuuliza kama ameonekana kwa sababu Dadi alikuwa na wasiwasi kwamba Mwanamaua angepatikana na ashindwe kumkuta.

Mwanamaua alikuwa na ushawishi mkubwa. Hii ni kwa sababu aliweza kumshawishi Dadi na kukubali kumchezea Kipelele. Tunaelezwa kuwa Mwanamaua alimwambia Dadi kuwa ni mwoga na hajawahi kuonekana kupigana na hata mwenzake mmoja alipokuwa mdogo. Pia anamwambia yeye si shujaa na mwanamume hastahili kuwa mwoga. Juu ya yote hayo shutuma za Mwanamaua zilimkaba kiasi cha kumfanya asipate pumzi. Na alipojichungua akajihisi mjinga. Mwishowe, Mwanamaua alisita kwanza halafu kwa sauti ya kunong'oneza alimwambia Dadi kwamba anataka awaonyeshe walimwengu kwamba yeye sivyo wanavyodhani, kwamba yeye si mtepetepe, si mbichi kama wanavyodhani.

Maneno hayo ya ushawishi ndio yalimfanya Dadi kukubali kumchezea Kipelele. Hivyo, nguvu za ushawishi wa mwanamke unaweza kumtia mwanamume pabaya. Mwanamaua anafaulu kumshawishi Dadi apigane na ng'ombe Kipelele kinyume na kupenda kwake kwa sababu ulikuwa usiku wao wa mwisho maana anauawa siku inayofuata na ng'ombe Kipelele.

### 3.2.10 Dadi katika 'Mhanga wa Mwanamaua'

Mhusika huyu ndiye mchumba wa Mwanamaua. Dadi alikuwa anampenda Mwanamaua. Hii ni kwa sababu anamngojea kwenye kichaka usiku wa kiza. Tunaelezwa kuwa Dadi na Mwanamaua walisogeana, Dadi akanyoosha mikono yake na Mwanamaua akaishika hodari. Tunaelezwa kuwa walijitupa chini kwenye majani ili kumaliza dhiki ya kukutana msituni. Hii ni kuonyesha kwamba walifanya mapenzi wakijificha wasionekane.Tunaelezwa kuwa Dadi alingojea kwa hamu atwikwe mzigo wowote bila kujali uzito wake, madhali mtwikaji ni Mwanamaua. Hapa ni pale Mwanamaua ana mambo mawili ambayo yalikuwa yanamsumbua. Dadi hakujali yawe magumu vipi bora ni Mwanamaua anataka hivyo.

Dadi alikuwa mwoga. Tunaelezwa kuwa Mwanamaua alisema kuwa anasikitika kusema kwamba Dadi si shujaa. Mwanamume hapaswi kuwa mwoga. Mwanamaua anamwambia Dadi kuwa hajaonekana tokea utoto wake kuingia uwanjani kucheza na wenzake miereka au kuandamana nao walipofukuza fahali mkali aliyekata kamba. Pia anamwambia hajaonekana kupigana na hata mwenzake mmoja alipokuwa mdogo. Hii ni kumaanisha kwamba Dadi kweli alikuwa mwoga.

Dadi ni kijana mwenye huruma, mcheshi na mwenye bidii katika kazi za ukulima na ufugaji. Mwanamaua harithishwi na haya na anamdhihaki kwa kumwambia kuwa yeye ni mwoga maana hajawahi kupigana na wenzake akiwa mdogo wala kucheza uwanjani na fahali wakali. Dadi haoni haja ya kucheza na ng'ombe hatari kwa sababu huenda akapata msiba wa ushujaa wake. Afadhali kuitwa mwoga na kuendelea kucheka. Hivyo Dadi ni mwenye busara kwa sababu anataka kujiepusha na mchezo hatari wa kuchezea ng'ombe.

Dadi anatolewa na Mwanamaua kama kafara ingawa Mwanamaua alikuwa anataka kujivunia ujasiri wake. Wakati Dadi alikuwa akipigana na ng'ombe Kipelele, anashindwa

kujikinga na pembe zake. Kipelele anamrusha juu na anapoanguka chini anamlalia, damu inamtoka Dadi puani na kinywani. Kuuawa kwa Dadi kunafanikisha anwani ya hadithi 'Mhanga wa Mwanamaua' kwani Mwanamaua anamtoa kama kafara akitaka ujasiri wake utambuliwe na wanakijiji, hatima yake kumpoteza mchumba wake. Hivyo, Dadi anakuwa kafara huku Mwanamaua akibaki na huzuni mwingi wa kumpoteza mchumba wake.

Dadi alishawishika haraka. Tunaelezwa kuwa Kipelele alitolewa uwanjani. Kipelele alikuwa na  vijipembe vidogo vya hadaa, alikuwa mwenye misuli iliyosimama wazi mwili mzima. Pia alifoka, akatoa kipovu cha kinywa. Kipelele aliinua masikio na kusimamisha mkia na akaangaza mara huku mara huku. Maneno haya yanaonyesha ukubwa wa Kipelele na kutayarisha wasomaji kutarajia kushindwa kwa Dadi. Matumizi haya yanaonyesha athari za kukubali kushawishika kwa Dadi kupigana na Kipelele kulikosababisha kifo chake.

### 3.2.11 Fumu katika 'Njia Fupi'

Fumu ni mumewe Naima. Fumu ni msherati. Anamuacha mkewe mrembo Naima na kwenda danguro la Mama Kitimbi kutafuta makahaba. Naima anapogundua siri hii, anajikwatua kwelikweli na kujipeleka huko danguroni kama mmoja wa makahaba. Fumu anapokimbilia huko kutuliza joto lake la mwili, anamkuta huko. Tunaelezwa kuwa hakuelewa Naima alijuaje kwamba ni mtembelea na mshiriki wa matendo ya nyumba hiyo. Pia tunaelezwa Naima alijipeleka pale danguroni kama mmoja wa makahaba. Fumu anapokimbilia huko kutuliza joto lake la mwili, anamkuta huko. Pia tunaelezwa pale danguroni tunapata taswira ya makahaba wanaoajiriwa na Mama Kitimbi kuwafurahisha wanaume kama Fumu. Walikuwa wamesimama mstari mmoja. Jicho la Fumu lilikwenda taratibu lakini halikufika mwisho. Hivyo, Fumu alikuwa mzinzi. Pia tunaelezwa kuwa Mama Kitimbi alipomwona Fumu alimkaribisha kwa shangwe. Kwa hakika Fumu ni mteja maarufu penye duka lake la laana. Na yale maisha yanavyomwendea bibi huyu yamechangiwa na wateja kama hawa wengi. Maarufu miangoni mwao ni Fumu.

Fumu ni msaliti. Fumu anataka kujitoa lawamani kwa kuwa na jicho la nje. Fumu anasema kuwa hawezi kujizuia na daima hujifikiria kwanza bila kujali hata kama angesaliti mapenzi ya mkewe Naima. Fumu anajua fika kwamba yeye mwenyewe ndiye alikuwa anavunja ndoa yake. Hii ni kwa sababu anasema pia talaka haingewezekana kati

yake na Naima. Fumu anajua anastahili kuwa mwaminifu kwa ndoa yake, lakini anaonyesha kuwa si mwaminifu kwa mkewe ilhali mkewe ni mwaminifu kwake. Hivyo, Fumu ni msaliti wa mapenzi kwa mkewe Naima. Pia Fumu anazoea kutembelea mahawara katika danguro la Mama Kitimbi. Mkewe Naima anapomfumania alijiona yumo katika ndoto na aliduwaa, akaganda kama sanamu. Hii ni kumaanisha kwamba Fumu aliaibika sana kwa kumsaliti mkewe.

### 3.2.12 Naima Mambo katika 'Njia fupi'

Naima Mambo ni mkewe Fumu. Naima ni mhusika mwenye busara. Naima anapanga njia thabiti ya kumfumania mumewe Fumu aliyekuwa mzinzi na hatimaye anafaulu. Maana ya jina Mambo, ni shughuli nyingi anazofanya mtu. Naima anajifanya kuwa mmoja wa makahaba katika danguro alimoenda mumewe na kweli mumewe anamfumania huko. Hamtolei ukali mumuewe bali anamshika mkono na kumwambia warejee nyumbani. Pia Naima anajikwatua kwelikweli kwa rangi ya mdomo, podari, kujirashia mafuta mazuri, kuzikoleza kope wanja na kadhalika. Anajikwatua hivi kabla ya kwenda kwa Mama Kitimbi ambapo anapanga kumnasa mumewe Fumu katika tabia zake za uzinzi.

Naima alikuwa mrembo. Naima anajipamba na kupambika. Fumu akawa anamwangalia kwa upembe kujaribu kulishibisha jicho lake sirisiri uzuri wa mkewe usiochujika. Mwandishi anamaanisha kwamba macho ya mtu kukiangalia kitu au mtu kwa hamu kwa sababu yamependezwa na yanachoangalia. Hivyo, maneno haya yanamulika nafasi ya mwanamke katika jamii. Mojawapo ni kuchukuliwa kama pambo la kurembesha nyumbani au mandhari fulani. Fumu anavutiwa sana na urembo wa mkewe Naima. Pia Fumu anasema kuwa Naima kwa umbo mkamiifu na kwa sura ungemwita malaika.

Naima alikuwa anampenda mumewe Fumu. Hii ni kwa sababu tunaelezwa kuwa lakini juu ya yote, Naima anampenda mumewe, ingawa anajua kwamba mume mtu anamwendea kinyume yeye Naima. Tunaelezwa kuwa Naima alimwamini katika imani ya mapenzi na ndoa ni mfano wa mwanamume bora. Naima alimpenda mumewe kwa shime na shangwe mpaka alipogundua uzinzi wake. Tunaelezwa alipogundua ndipo alipouchonga ukali wake pale alipanga njia thabiti za kumnasa na kumwaibisha mumewe. Pia tunaelezwa kuwa Fumu anasema kwamba Naima mkewe hajabaini lolote kizani

anamojificha. Na kwa hakika siku zote hizo Fumu aliacha sura ya malaika kwenye akili ya mkewe.

Naima alikuwa mwaminifu kwa mumewe. Hii ni kwa sababu tunaelezwa kuwa Fumu aliungama kwamba siku zote anatoka nje na Naima hata siku moja hajapata kusema chochote. Fumu anajua fika kwamba yeye mwenyewe ndiye alikuwa anavunja ndoa yake. Hii ni kwa sababu anasema pia talaka haingewezekana kati yake na Naima. Hivyo, Naima alikuwa mwaminifu kwa mumewe Fumu.

### 3.3. Wahusika Wadogo

Katika Diwani za Said .A. Mohamed wahusika wadogo wametumika. Wahusika wadogo wamegawanyika katika makundi mawili. Kuna wahusika wasaidizi ambao hutumiwa ili kumsaidia msomajii amwelewe vyema mhusika mkuu.Wahusika wengine ni wahusika wajenzi. Hawa wamewekwa kwa lengo la kukamilisha dhamira na maudhui ya mwandishi. Hali kadhalika, wanajenga wahusika wasaidizi na wakuu. (Njogu K. na Chimera R. 1999). Wahusika wadogo katika utanzu huu huwa wachache na hawakuzwi.

#### 3.3.1 Baba yake Mussa katika 'Sadiki Ukipenda'

Mhusika huyu ni baba yake Mussa. Baba yake Mussa ni mchawi. Hii ni kwa sababu Mzee Siwa alijuza Mussa kwamba baba yake ni mchawi na alikuwa anadaiwa mwana. Na yeye kawaambia wachawi wenzake kwamba yu tayari kumtoa yeyote kati ya ndugu zake Mussa. Mzee Siwa alimweleza Mussa kuwa wenzake wamekataa, wanataka Mussa kwa sababu ni msomi. Baba yake Mussa na wachawi wengine walikuwa wamepanga kuua Mussa, lakini Mzee Siwa alimwelekeza jinsi ya kujiokoa ili asiuawe kwa njia ya urogi. Baba yake Mussa ni mchawi kwa sababu mwandishi anatueleza kuwa baba yake Mussa walikuwa wamepanga na wachawi wengine kumuua Mussa. Pia baba yake Mussa na wachawi wengine walikuwa wakisherehekea nyimbo na ngoma usiku wa manane na walikuwa wanamwita baba yake Mussa kware na baba yake Mussa akafurahia kuitwa hivyo.

Baba yake Mussa ni katili. Amepanga kumtoa mwanawe aangamizwe na wachawi na anasema kwamba yu tayari. Hivyo, ukatili wa baba yake Mussa unajitokeza zaidi pale baba yake Mussa na wachawi wengine wakicheza ngoma walitumia magongo, marungu,

mawe na mapanga walipokuwa wakitwanga zuzu. Hawakuwa na huruma walipokuwa wanatekeleza ukatili huo.

### 3.3.2 Wachawi katika 'Sadiki Ukipenda'

Wachawi walipanga pamoja na baba yake Mussa kumwangamiza lakini ilitokea kinyume. Wachawi walikuwa wakiroga watoto na vijana na hasa wasomi. Tunaelezwa kuwa warogi walikataa kutolewa ndugu yake Mussa. Walikuwa wanataka Mussa kwa sababu ni msomi. Wanasema kuwa wasomi wana hatari kwa sababu kila siku wanatafuna na kuuma. Hivyo, wachawi hawakuthamini elimu. Hii ni kwa sababu wamepanga kuua Mussa kwa sababu ni msomi. Jamii hii haitaki vijana kuendelea na masomo yao. Hii ni kwa sababu wanaogopa wasomi kuwa watawasumbua hasa wachawi. Walikuwa katili kwa sababu walikuwa wanaroga vijana na watoto ambao ni tegemeo la wazazi kwa siku za usoni. Tunaelezwa kuwa Mzee Siwa alikuwa anaeleza Mussa kuwa watoto na vijana ndio tegemeo la wazazi wao watakapozeeka na hatimaye kuaga dunia. Wao ndio watakaowatunza wakiwa wagonjwa na kuwazika watakapoaga dunia.

### 3.3.3 Bi. Sihaba katika 'Ngondo Pangoni'

Mhusika huyu ni mkewe Jecha. Bi Sihaba ni msherati. Hii ni kwa sababu wanapanga na Kondo kwenda arusini ili wakutane pangoni mahali pa siri na kufanya mapenzi. Tunaelezwa kuwa Bi Sihaba alikuwa wa namna mbili. Kwanza wa furaha. Pili wa wasiwasi. Furaha kwa sababu usiku ule kulikuwa na arusi ya kesha ambayo ingempa fursa ya kutoka na kubuga kama mnyama anayeasi msitu na nyika alivyopenda. Wasiwasi ni kuwa kama Jecha angemruhusu aende huko arusini au la. Hivyo, alikuwa amengojea arusi hiyo kwa hamu na ghamu. Pia Bi. Sihaba anasema ni arusi ya kushibisha mtu akashiba. Hivyo, Bi. Sihaba alitumia akili ili aruhusiwe kwenda arusini ndio wakutane na Kondo ili wafanye mapenzi.

Bi. Sihaba ni mhusika mwenye busara. Anapanga kumweleza mumewe Jecha kuwa hakuna haja ya kuweka uadui na Bwana Jabu. Tunaelezwa kuwa Bi. Sihaba anamwambia mumewe kuwa mbona amefanya jambo jema. Bi. Sihaba anamwambia Jecha kuwa yeye na Jabu ni majirani na watu wazima wenye akili timamu na wanakutana mabarazani kila siku, ya nini hasama za bure. Bi. Sihaba anasema na yeye Jecha akimruhusu kwenda arusini ndio itakuwa bora zaidi. Hivyo, Bi. Sihaba aliruhusiwa kwenda arusini ingawa

Jecha alikuwa anataka Bi. Sihaba abaki nyumbani ili hata yeye arusi imfae zaidi. Bi. Sihaba alitumia akili ili aruhusiwe kwenda arusini.

Bi. Sihaba alikuwa anampenda Kondo kuliko Jecha. Hii ni kwa sababu tunaelezwa kuwa ilikuwa vigumu kuweza kutoka arusini lakini mbele ya hamu na mapenzi hakuna kisichowezekana; hakuna jambo gumu. Kondo alipomuuliza mapenzi kuliko Jecha, Bi. Sihaba alisema mapenzi kuliko Jecha kumi, licha mmoja. Aliendelea kumwambia kwamba asisahau ujasiri alioupitisha, kuweza kupenya wingi wa watu, akaandamana kiguu na njia akaelemea msitu na nyika, mpaka hapo aliposimama. Anauliza Kondo kama si mapenzi yake ni nini? Hivyo, maneno haya yanatueleza kuwa Bi. Sihaba alikuwa anampenda Kondo kuliko Jecha mumewe wa ndoa. Hivyo tunaona katika jamii familianyingi zimeathiriwa kwa sababu hakuna mapenzi ya dhati kwa waliofanya ndoa na kwa mke na mume.

### 3.3.4 Bi. Mwamboje katika 'Ngondo Pangoni'

Bi. Mwamboje ni mkewe Kondo. Bi. Mwamboje ni msherati. Hii ni kwa sababu tunaelezwa kuwa alipanga na Jecha waende arusini ili wakutane huko. Pia walienda pangoni mahali pa siri ili wafanye mapenzi lakini kwa sadfa wanafumaniana huko na Bi. Sihaba na mumewe Kondo. Walipokutana huko pangoni, Kondo aliwakaribisha pangoni. Tunaelezwa kuwa Jecha alisema na huyu hapa Bi Sihaba mkeo...karibu pangoni, Jecha na Bi Mwamboje na mimi na Bi Sihaba. Hivyo marafiki wote wakafumaninana kule pangoni.

Bi. Mwamboje alikuwa rafiki wa Mama Shika mkewe Bwana Jabu. Hii ni kwa sababu tunaelezwakuwa katika wanawake waliohudhuria hapo, Bi. Mwamboje, mkewe Kondo, alionekana kashughulika sana kwa sababu arusi hiyo ilimhusu sana. Bi. Mwamboje alifunga Kibwebwe kiunoni, kilemba kichwani na kuibeba arusi kifuani, akaitumikia kwa mambo yasiyokuwa ya lazima na ya lazima. Hiyo, Bi. Mwamboje alijitolea kwa vyovyote vile ili kuona ya kwamba arusi hiyo inaenda vizuri. Pia tunaelezwa kuwa arusi hiyo ilikuwa ya Mwari wake Fedhela. Mwari wa kumlea kwa mafunzo ya siri ya unyagoni aliyepewa na Mama Shika, mkewe Bwana Jabu. Hii ni kumaanisha ya kwamba Bi. Mwamboje na Mama Shika walikuwa marafiki wa dhati. Hivyo, maudhui ya urafiki yanajitokeza.

**3.3.5 Biti Shomari katika 'Uhuru wa Subira'**

Biti Shomari alikuwa mama yake Subira na mkewe Mzee Farijali. Biti Shomari alikuwa mvumilivu. Hii ni kwa sababu alivumilia shida nyingi hasa za mumewe Farijala. Alikuwa anateswa sana na mumewe kwa sababu tunaelezwa kuwa kuzaliwa kichwa, mikono na miguu si hoja, hoja kuwa mwanamume. Hii ni kwa sababu alipitia madhila na mateso kutoka kwa mumewe. Biti shomari anasema yeye ni mtumwa na mwanawe ni mtumwa na labda wanawake wote. Hii ni kumaanisha ya kwamba yeye na mwanawe Subira walikuwa wanateswa sana hasa na waume zao. Hivyo, Biti Shomari anaonyesha kudhalilishwa kwa mwanamke. Pia Biti Shomari anasema kulizawa mwanamume ni uhuru na kuzaliwa mwanamke ni utumwa. Hivyo anasema mwanamke na mwanamume ni viumbe sawa walioumbwa na Mungu lakini hakuna usawa duniani. Mwanamume ni bwana na mwanamke ni mtumwa. Biti Shomari anaonyesha kuwa wanaume wanajiona viumbe muhimu kuliko wanawake.

Biti Shomari alikuwa mlezi bora wa familia yake. Hii ni kuwa sababu anashughulika na kazi za nyumbani za kuandaa chakula. Ana mboga ya mtoriro na pia anaandaa kinu na mchi tayari kwa utwangaji. Binti yake Subira alipofika nyumbani anamsaidia kutwanga ingawa mishindo dhaifu ilivuma kwa sababu ya kusita kwa Subira alipokuwa akitwanga alikuwa na mawazo mengi. Hii ni kwa sababu ya ugonjwa wa mateso na madhila aliyokutishiwa na mumewe. Pia tunaelezwa kuwa Biti Shomari alilea Subira vizuri kabla hajaolewa. Tunaelezwa kuwa zama zake alipokuwa Subira, alikuwa Subira kweli. Pale alipokuwa kimwana aliyeshiba maziwa ya mamake. Pia anasema mwanamke fahari ya mwanamke aliyevaa siha na nguvu kumwenda mwilini. Hivyo, Biti Shomari alikuwa akimlea Subira vizuri na kuwa na afya.

Biti Shomari alikuwa anamhurumia Subira. Anasema kuwa yeye ni mtumwa na mwanawe pia ni mtumwa. Anasema wanawake wanateswa na wanaume waliowaoa. Biti Shomari anamhurumia sana Subira kwa sababu anaona afya yake imedhoofika. Pia wakati baba yake Mzee Farijala anamchapa Subira anamsihi amuache lakini Mzee Farijala anakataa katakata. Tunaelezwa kuwa Biti Shomari anamsihi Mzee Farijala, msalie mtume bwana Farijala kwa sababu Subira aliteswa sana na mumewe. Biti Shomari anamwambia Farijala,'Mtume simama uo....mtume! msamehe mwanao'. Alilia na kusihi

Biti Shomari, lakini wapi alikuwa amechelewa. Hivyo Biti Shomari alimhurumia sana bintiye kwa kuchapwa na baba yake.

### 3.3.6 Mzee Farijala katika 'Uhuru wa Subira'

Mzee Farijala ni baba yake Subira na mumewe Biti Shomari. Mzee Farijala alikuwa katili. Hii ni kwa sababu tunaambiwa kwamba baba'ake akifika tu alimchapa na kuapa kwamba alitoka kwa mumewe angemuua. Tunaelezwa kuwa baba'ake Subira alikuwa amezoea kumpiga Binti yake kila alipokuja nyumbani kwa shitaka la mumewe kwamba anataka waachane. Pia hakuonyesha mapenzi kwa Subira bali walishirikiana na mumewe Mrisho kumtesa zaidi. Hivyo, maudhui ya udhalilishaji wa wanawake. Mzee Farijala alimsaidia mumuwe Subira kudhalilisha Subira ambaye ni mwanamke.

Mzee Farijala alikuwa akiwachapa wanawe na bibi yake Biti Shomari. Mzee Farijala alikuwa mwenye ubabedume. Hivyo, aliamini kwamba lazima wanawake wachapwe kwa sababu ni watumwa na wajinga ambao hawastahili kuhurumiwa. Hivyo, Mzee Farijala anaonyesha ubabedume. Tunaonyeshwa kuwa wanaume ndio wanastahili kuishi kwa uhuru wanaotaka ihali wanawake wanastahili kudhalilishwa jinsi wanaume wanavyotaka. Hivyo, maudhui ya ubabedume.

Mzee Farijala alikuwa mwenye hasira nyingi. Hii ni kwa sababu hasira za Subira zilikuwa ndogo ikilinganishwa na za baba'ake. Hii ni kwa sababu Mzee Farijala alimchapa sana Subira. Mama'ake Subira alijaribu kumsihi mumewe aache kumpiga mwanawe lakini hakusikia. Hii ni kumaanisha kwamba pia alikuwa na msimamo mkali. Tunaambiwa kuwa hakuna uombezi Farijala anapokamata silaha. Hakuna maneno yangemrejesha nyuma kwa lile alilokwisha liamua. Hasemi tena. Kwake mananeo mwanzo, mwisho vitendo. Hivyo, hakuna kurudi nyuma alipoamua kulitenda jambo.

### 3.3.7. Kibwana katika 'Mwungwana'

Kibwana alikuwa mzinzi. Tunaelezwa kuwa Kibwana alifumaniwa na Bwana Haji wakifanya mapenzi na Saada. Tunaelezwa kuwa ilisadifu kwamba kwa wakati huu Kibwana alikuwa kamkumbatia Saada, mke wa Bwana Haji. Kusikia sauti ya mngurumo wa kiume ikipiga hodi, Kibwana aliruka kitandani na kutua katikati ya chumba, kanga

kiunoni. Saada alimpa moyo na kumwambia aendelee kupoa kitandani na kumwambia asijali kwani hakuna chochote kingevunja starehe yao.

Kibwana alikuwa mwoga. Tunaelezwa kuwa Kibwana alikuwa na woga wa kufumaniwa. Kwa Kibwana, dunia yote aliyokuwa kaibeba kwa matokeo asiyoyatarajia, sasa ilikuwa nyepesi kama bua. Hii ni baada ya kutiwa moyo na Saada. Sasa hakuwa na haja ya kufadhaika. Aliloogopa kuwa, halikuwa kwamba aliyepiga hodi si mumewe Saada.

Kibwana alikuwa mnafiki. Tunaelezwa kuwa alitweza pumzi na kupasua kicheko cha ishara ya kuridhika na kumuunga mkono Saada kwa ugunduzi wake wa kwamba anayepiga hodi si mumewe. Pia alishukuru Mungu pahali asipostahiki kushukuriwa kwa sababu alikuwa akifanya dhambi. Pia tunaelezwa kuwa Kibwana alipotiwa moyo na Saada, alisahau haraka kile alichokuwa akiogopa. Tunaambiwa kuwa mwanadamu ni mwepesi wa sahau. Hii ni kwa sababu alijitupa kitandani kama siye Kibwana aliyekuwa akihangaika dakika chache zilizopita. Huu ni unafiki kwa sababu alijifanya kusahau kila kitu kwa kuogopa kufumaniwa na Bwana Haji.

### 3.3.8 Bi. Sikitu na Bwana Ali katika 'Mwungwana'

Wahusika hawa walikuwa wakwe wa Bwana Haji na wazee wa Saada. Bi. Sikitu na Bwana Ali walikuwa wavumilivu. Hii ni kwa sababu Bwana Haji alipowaalika kwa siri kwake, hawakuwa na haraka ya kutaka kujua ni nini walichoitiwa. Walikaa siku nne ndio Bwana Ali aliandaa mkutano wa dharura. Bwana Ali alimwita Bwana Haji kwa jina la heshima 'baba' na kumwambia Bwana Haji kwamba wamemwita kumuuliza mbona toka walipofika nyumbani kwa Bwana Haji wanaona Saada hana furaha na analia na kutaka kurudi nyumbani. Bwana Ali alimuuliza Bwana Haji kama amemfanya nini. Bwana Haji aliwajibu nimemfanya nini mimi, au amenifanya nini yeye? Bwana Ali na Bi. Sikitu wakawa wameelewa na kitandawili. Hivyo, walitumia busara yao kuelewa kuwa Saada ndiye aliyemkosea Bwana Haji. Baadaye Bwana Ali alimsihi mkwewe Haji kwamba awasamehe. Bwana Ali aliendelea kumsihi Haji aishi na Saada lakini Haji alikataa katakata kuishi nayo. Hivyo, maudhui ya uvumilivu yanawasilishwa na wahusika hawa.

### 3.3.9 Ng'ombe Kipelele katika 'Mhanga wa Mwanamaua'

Mhusika huyu ni ng'ombe anayeitwa Kipelele. Kipelele alikuwa mkubwa kiumbo na mwenye kutisha. Alikuwa ng'ombe hatari aliyesababisha kifo cha Dadi. Pia alikuwa ng'ombe kisirani kwa sababu aliuwa watu wengi. Hii ni kwa sababu tunaelezwa kuwa ni ng'ombe ziraili aliyekwisha ua watu watatu katika mchezo wa ng'ombe. Kila mtu anazielewa hamaki zake Kipelele. Tunaelezwa kuwa Kipelele alikuwa fahari la gombe. Ukubwa wake kiumbo unajitokeza pale tunaelezwa sifa zake kwamba: Kuza lenye vijipembe vidogo vya hadaa, lakini lenye misuli iliyomsimama wazi mwili mzima. Linafoka. Linatoka kipovu cha kinywa. Limeinua masikio. Limesimamisha mkia. Katoa macho yaliyomwaa. Maneno haya yanatuonyesha kuwa Kipelele alikuwa ng'ombe hatari wa kuchezea. Macho ya Kipelele yanang'ara kwa hamu ya kumhujuma mtu. Kipelele alimuua Dadi kwa kuwa alikuwa ng'ombe hatari. Pia maneno haya yanatuonyesha ukubwa wa Kipelele na kutayarisha wasomaji kutarajia kushindwa kwa Dadi. Matumizi haya yanaonyesha athari za kukubali kushawishika kwa Dadi kupigana na Kipelele kulikosababisha kifo chake.

Kipelele alikuwa amezoea kuchezea watu. Hii ni kwa sababu alikuwa na ujuzi wa kupigana. Tunaelezwa kuwa Kipelele alipita kama upepo, akageuka, akamkabili tena mchezaji wake. Huu ulikuwa ujuzi wake wa kucheza kwa sababu alitunga shabaha kwa nia zaidi. Tunaelezwa alivundumka tena na Dadi hakuwahi kukwepa na Kipelele alimteka na kumrusha juu hewani. Dadi alianguka na kuvunjika shingo na mwishowe alinyooka.

### 3.3.10. Wanakijiji wa Pemba katika 'Mhanga wa Mwanamaua'

Wanakijiji wa pemba walikuwa wanashirikiana hasa kupitia michezo ya ng'ombe. Walikuwa wanajitumbuiza kwa mchezo wa kutazama ng'ombe wakiwakimbiza watu katika uwanja wa wingwi. Tunaelewa kuwa machumi ya karafuu huja na furaha na misiba yake. Hii ni kumaanisha kuwa wanapemba wanafurahia neema ya kuchuma karafuu na pia kuomboleza vifo vya wale wanaoshindwa kuwaepuka ng'ombe na hivyo kuuawa. Dadi anakuwa mmoja wa wanaouawa na ng'ombe Kipelele. Hivyo, wanakijiji wa pemba wanaendeleza maudhui ya ushirikiano. Hii ni kwa sababu walishirikiana katika mchezo wa kutazama ng'ombe na pia kusherehekea walioshinda mashindano hayo, pia

kuchuma karafuu na kuomboleza vifo vya walioshindwa katika michezo hiyo. Dadi akawa mmoja wa wale walioshindwa katika mchezo wa ng'ombe Kipelele.

Wanakijiji pia walikuwa wanafanya biashara wakifurahia mchezo wa ng'ombe. Tunaelezwa kuwa waliuza tindi za mua waliokuwa wakikata vipande harakaharaka. Wengine waliuza njugu, kashata na jumla ya vyakula vya udohoudoho.Walikuwa wakipasua tabasamu kwa jinsi biashara ilivyokuwa ikiwaendea vyema. Hivyo wanakijiji walifurahia wakati kama huu.

Wanawake nao pia walisherehekea kwa nyimbo na hoihoi. Tunaelezwa wakati huu hoi hoi za wanawake zilisikika kwa nguvu. Kila mmoja akipaza sauti asikiwe na mpenzi wake. Wacheza wanne walikuwa uwanjani, Dadi akiwa mmoja wao. Nyimbo za wanawake zilimiminika. Sautiya Mwanamaua, ambayo ilimpenya Dadi na kumtia wazimu. Hivyo, nyimbo hizo ziliwatia moyo wacheza ng'ombe Kipelele. Tunaelezwa Dadi madadi yalimpanda. Dadi akawa na ujasiri wa kumkabili Kipelele.

### 3.3.11 Mama Kitimbi katika 'Njia fupi'

Kitimbi ni kitendo cha ila au cha kudhalilisha kinachotendwa dhidi ya mtu fulani. Mama Kitimbi ni mmiliki wa duka la laana. Anafanya biashara ya kuwauza wasichana na wanawake kwa wanaume wazinzi kama Fumu ili apate mali. Anawaita wasichana wake malaika na kumfahamisha Fumu alikuwa amepokea kitoto kipya ambacho angelipia milioni kustarehe nacho. Kazi ya Mama Kitimbi ni ya kudhalilisha na kutukanisha jinsia ya kike. Jina la Mama Kitimbi linaonyesha uozo wa ukahaba miongoni mwa wanajamii.

Mama Kitimbi alikuwwa na tamaa ya pesa. Mama Kitimbi anamwambia Fumu kuwa siku hiyo angelipa milioni nzima kwa kujistarehesha na Naima. Milioni nzima ni pesa nyingi inayozidisha sana pesa wanazotoa wanaume kwa kwenda kwa danguro la Mama Kitimbi. Maneno haya yanatilia mkazo tamaa yake ya pesa.

Mama Kitimbi alitumia mbinu za ushawishi ili kumtia Fumu hamu ya kutazamia siku ile. Hii ni kwa sababu alikuwa amepokea kisura kipya katika danguro lake. Anasema leo ni leo asemaye kesho mwongo! Leo ni leo, asiye mwana aeleke jiwe (uk 134). Tena Mama Kitimbi anamjuza Fumu kuwa 'Na kwa mwenye macho haambiwi tazama (uk 134).

Methali hii inamtayarisha Fumu na kumjaza hamu kutolea joto lake pale ili kuimarisha maudhui ya ukahaba.

### 3.3.12 Makahaba katika 'Njia fupi'

Taswira ya makahaba wanaoajiriwa na Mama Kitimbi kuwafurahisha wanaume kama Fumu. Walikuwa wamesimama mstari mmoja. Wanaonyesha kutamaukwa kwa binadamu hadi kufikia kujiuza miili yao ili wajikimu. Tunaelezwa kuwa wanawake wa sura mbalimbali, wengi vijana, wengine makamu. Kuna baadhi walitia fora na waliokubuhu. Jicho la Fumu lilikwenda taratibu, lakini halikufika mwisho. Maneno haya yanatuonyesha wanawake wa marika mbalimbali walikuwa wanauza miili yao ili wapate pesa. Wanawake hawa walikuwa wengi kwa sababu jicho la Fumu halikufika mwisho. Hivyo, makahaba wanatufichulia ukahaba na uozo wa binadamu wa kuuza miili yao.

## 3.4 Hitimisho

Katika sura hii tumeshughulikia nafasi ya wahusika katika kufanikisha uwasilishaji wa maudhui katika diwani zilizoteuliwa za Said A. Mohamed. Tumeona ya kwamba hadithi fupi huwa na idadi ndogo ya wahusika ambao pia uhusika wao si wa kina.Wahusika hujifunga tu kwa tukio moja kuu. Tumechunguza wahusika wakuu na wahusika wadogo. Wahusika wakuu ndio nguzo ya masimulizi kwa kuwa ndio muhimu kuliko wengine wote. Wanahusika na matukio makuu ya hadithini. Wahusika wakuu wa hadithi fupi huwa bapa kwa kuwa utanzu huu hauwapatii nafasi ya kukua. Wahusika wadogo katika utanzu huu huwa wachache na huwa hawakuzwi kutokana na ufinyu was utanzu husika. Wahusika wadogo wanasaidia kumjenga mhusika mkuu. Hawa wamewekwa kwa lengo la kukamilisha dhamira na maudhui ya mwandishi.

Wahusika wakuu katika diwani zilizoteuliwa ni Mzee Siwa na Mussa katika 'Sadiki Ukipenda', Kondo na Jecha katika 'Ngondo Pangoni', Subira na Mrisho katika 'Uhuru wa Subira', Bwana Haji na Saada katika 'Mwungwana', Mwanamaua na Dadi katika 'Mhanga wa Mwanamaua' na Fumu na Naima katika 'Njia fupi'. Wahusika hawa wametawala hadithi fupi kutoka mwanzo hadi mwisho.

Wahusika wadogo katika diwani hizi teule wametumika katika kuwajenga wahusika wakuu. Kwa mfano baba yake Mussa anashirikiana na wachawi wengine kuroga vijana

na watoto. Bi. Sihaba mkewe Jecha wanafanya mapenzi na Kondo ambaye ni mumewe Bi. Mwamboje. Wote wanafumaniana pangoni na tabia zao zinajulikana. Biti Shomari anamhurumia Bintiye Subira kwa kuteswa na mumewe na pia Mzee Farijala pale anasema kwamba wanawake wanadhalilishwa na wanaume waliowaoa.

Kibwana anafumaniwa na Bwana Haji wakifanya mapenzi na Saada. Hivyo, Kibwana anasaidia katika kumjenga Saada ambaye ni mzinzi. Ng'ombe Kipelele ni mhusika ambaye anaua Dadi katika mchezo wa ng'ombe huku Mwanamaua akiachwa na mchumba wake. Mwisho tumechunguza Mama Kitimbi ambaye ni mmiliki wa 'Duka la Laana' ambako Fumu anatembea na kuwa mteja wa duka lile. Makahaba wanakutana kwa Mama Kitimbi ili wauze miili yao na kujikimu.

Matendo ya wahusika mbali mbali katika hadithi hizi yanadhihirisha uhalisia wa jamii ambayo imekithiri maovu na mielekeo isiyofaa.

# SURA YA NNE

## MIANZO NA VIMALIZIO VYA HADITHI FUPI KATIKA UWASILISHAJI WA MAUDHUI

### 4.1.Utangulizi

Katika sura hii tumechunguza jinsi mianzo na vimalizio vinavyofanikisha uwasilishaji wa maudhui. Mianzo na vimalizio ni mojawapo ya vipengele vya msuko. Msuko ni mpangilio wa matukio pamoja na ubainishaji wa vyanzo vyake. Msuko wa hadithi fupi huwa sahili. Matukio huwa yanatiririka na kufululiza moja kwa moja kutoka mwanzo hadi mwisho.

Kulingana na Wamitila (2002), msuko wa hadithi fupi huwa na mwanzo, kati na mwisho. Sehemu hizi huwa na maana kuliko tanzu nyinginezo. Katika ufunguaji wa hadithi fupi, mwandishi anadhihirisha waziwazi dhamira yake katika hadithi hiyo. Hadithi fupi inapaswa isukwe kwa namna ambayo inapofika mwisho, msomaji anahisi mkokotezo fulani au anajiwa na athari kubwa.

### 4.2.Uanzaji wa Hadithi Fupi katika Diwani za Said A. Mohamed

Katika sehemu hii tumeangazia uanzaji wa hadithi fupi. Hadithi fupi huanza kwa mtindo unaoacha athari au mchomo wa aina fulani kwa msomaji ambaye anavutwa na kunaswa na hadithi fupi hiyo. Ufupi wa utanzu huu huathiri uteuzi wa mbinu za uandishi, uwasilishaji wake pamoja na athari nzima ya uandishi wenyewe. Katika hadithi teule za Said A. Mohamed kuna mianzo tofautitofauti inayoonyesha kuwa hadithi imeanza. Mianzo hii ni kama ifuatavyo:

#### 4.2.1.Mwanzo wa Kitathmini

Katika mwanzo wa aina hii, mtunzi wa hadithi anaanza kwa kutoa kauli ambayo ni ya kitathmini. Tathmini hii inajifunga kwenye ulimwengu wa hadithi, ambapo msimulizi anatoa kauli za kutathmini kuwahusu wahusika, matukio, mambo au hali katika ulimwengu huo (Wamitila 2008).

Katika hadithi fupi ya ‘Sadiki Ukipenda’ hadithi inaanza hivi:

> Kuna mengi. Mengi yaliyonivutia kwa Mzee Siwa
> hata nikaungama naye. Kwanza, ukweli wake. Kwake,
> neno ni deni kubwa kuliko deni la fedha.
> Pili, ushujaa wake. Penye haki husimama
> kidete bila ya kutetereka wala kuwa na hofu na
> mtu yeyote: mkubwa au mdogo.
> Tatu, imani yake, hasa kwangu – daima alikuwa
> tayari kugawa mafungu chochote alichokuwa
> nacho, ijapokuwa ndicho hichohicho. Nne… (uk. 1).

Hadithi hii inahusu Mussa ambaye ni kijana msomi. Kijana huyu alikuwa amepangiwa na baba yake pamoja na wachawi wengine kumroga kwa sababu yeye alikuwa Msomi. Maudhui makuu katika hadithi hii ni ushirikina na kutotilia maanani elimu. Hata hivyo, sehemu hii ya ufunguaji haionyeshi hivyo. Hii ni kwa sababu hadithi fupi haina nafasi ya kueleza kila kitu kwa kina kwa sababu ya ufinyu wake. Pia mwandishi wa hadithi fupi hana uhuru wa kutumia maneno mengi au kuwa na ulumbi usiokuwa na maana (Wamitila 2002).

Katika hadithi hii, Mzee Siwa anamfichulia kwamba baba yake ni mchawi na akampangia jinsi ya kujiokoa kutokana na ukatili wa baba yake pamoja na wachawi wengine. Mzee Siwa pamoja na Mussa wanafaulu katika kutekeleza wajibu huu.

Katika hadithi hii msuko ni wa moja kwa moja. Mussa ndiye msimulizi na anatueleza kuwa alijuzwa na Mzee Siwa kuwa baba yake ni mchawi na amepangiwa kuuawa. Mussa anaonyesha kutoamini kuwa baba yake ni mchawi. Mzee Siwa anamhakikishia kuwa baba yake Mussa ni Mchawi na kweli mambo haya yanadhihirika wazi wakati baba yake na wachawi wengine walitoka usiku wa manane kutekeleza wajibu wao.

### 4.2.2. Mwanzo wa Kirejeshi

Huu ni mwanzo ambao unatumia mbinu rejeshi au unamrejesha msomaji kwenye wakati aghalabu unaotangulia wakati wa msuko wa hadithi fupi inaoyahusika. Mbinu rejeshi hutumiwa katika hadithi fupi wakati mfiko na upana wake ni finyu. Pawepo na mwanzo wa aina hii ni sharti hadithi ianze kwanza kabla ya kurejeshwa nyuma kiwakati (Wamitila 2008). Katika hadithi ya ‘Ngondo Pangoni’ mwanzo wa aina hii unadhihirika:

> Dakika chache zilizopita walikuwa pamoja wamekaa kikaoni pao wakizungumza. Hii ilikuwa ni kawaida yao kila siku.
> Muda mfupi kabla magharibi, huiweka baraza chini ya mwembe mkubwa uliojimwaya kama mwamvuli. Pahali kame kabisa ambapo waliweza kupata faragha yote waliyotaka, (uk.16).

Hadithi hii inahusu marafiki wawili Kondo na Jecha. Kondo na Jecha walikuwa wazinzi. Walikuwa wamezoea kila wakati kukaa kikaoni pao wakizungumza. Baadhi ya mambo waliozungumza ni majisifu na umbea na pia juu ya wanawake waliofanya na wao mapenzi. Marafiki hawa walikuwa wamejiwekea siri ambayo hawangependa ijulikane. Hiyo siri walikuwa wamejiwekea kila mtu rohoni mwake. Walisema hiyo siri isingejulikana labda mtu atolewe roho yake ndio hiyo siri ingejulikana. Baadaye, siri hii inajulikana kwa sababu Jecha alikuwa na urafiki wa kimapenzi na mkewe Kondo ambaye ni Bi. Mwamboje na vilevile Kondo alikuwa na urafiki na mkewe Jecha ambaye ni Bi. Sihaba.

Tunaelezwa kuwa marafiki hawa walihudhuria arusi ya mwanawe rafiki na jirani wao Bwana Jabu. Huko arusini kila mtu alipanga kukutana na mpenziwe mahali pa siri ambako ni pangoni. Tunaona kisadfa wote wanafumaniana huko pangoni na uzinzi wao unajulikana.

Katika hadithi hii msuko wake umeelezwa kwa njia ya moja kwa moja. Mwandishi anatueleza kuwa familia nyingi zimeathiriwa kwa sababu ya ukahaba. Hii ni kwa sababu Bi. Sihaba anamweleza Kondo kuwa anampenda kuliko Jecha kumi. Hii ni kuonyesha kuwa hakuna uaminifu kati ya mke na mume kwenye ndoa. Hivyo, jamii hii iliathiriwa na uzinzi.

### 4.2.3.Mwanzo wa Kitaharuki

Kazi nzuri ya kifasihi inaweza kuwa na mwanzo wa kitaharuki. Hata hivyo, zipo ambazo kutokana na kusukwa kwa ploti au msuko, taharuki hiyo ina uwezo mkubwa zaidi. Taharuki ni kipengele muhimu katika hadithi fupi. Mianzo ya hadithi fupi huwa inamletea msomaji au mhakiki maswali ya: ‘Kwa nini?’ ‘Mbona?’ ‘Kisha?’ na kadhalika (Wamitila 2008).

Katika hadithi fupi ya ‘Uhuru wa Subira, taharuki inajitokeza ifuatavyo:

> Kuzaliwa kichwa, mikono na miguu si hoja, hoja kuwa mwanamume. Biti Shomari alikuwa akiwaza moyoni mwake. Na kwa kawaida, wakati anaponyerereka kwa madhila na mateso, shingo yake hulalia bega, na macho yake dhaifu, machozi. Hasemi kinywa kipana, ila humeza maneno yake ndani ya nadhari yake, kwa kuchelea mumewe, mwanamume kama wanaume wengine. Yeye ni mtumwa, na mwanawe ni mtumwa, na labda wanawake wote. Shahidi wake Mungu na labda nafsi yake, vile wanavyoteswa. (uk. 88).

Hadithi hii inahusu Subira ambaye alikuwa mkewe Mrisho. Subira aliteswa na mumewe na pia baba yake Mzee Farijala. Mama yake Subira ambaye ni Biti Shomari anasema kwamba yeye na mwanawe Subira ni watumwa kwa jinsi wanavyoteswa. Hivyo, Biti Shomari anatuelezea kuwa kuolewa ni kama kuwa mtumwa. Ndoa ni jela na yeye na mwanawe wako ndani ya jela. Vilevile, Biti Shomari anasema wanawake wote ni watumwa. Anaendelea kusema mwanaume ndiye bwana na mwanamke ni mjakazi.
Subira anadhalilishwa na mumewe na baba yake kwa sababu yeye ni mwanamke. Hadithi hii inatueleza kuwa Subira alikuwa amezoea kurejea kwao nyumbani akitaka waachane na mumewe Mrisho ili apate uhuru wake. Hivyo, ufaafu wa anwani ‘Uhuru wa Subira’. Kila aliporejerea nyumbani kwao kudai uhuru wake, baba yake hakumsikiza bali alikuwa akimchapa kichapo cha mbwa kinywa juu. Mama yake Biti Shomari alikuwa akimsihi mumewe aache kumchapa mwanawe lakini hakusikia kwa vile alikuwa na msimamo mkali na kufikiri kuwa wanawake wanastahili kuchapwa kwa sababu ni wajinga na hawastahili kuhurumiwa.

Tunaelezwa ya kwamba, baada ya Subira kuchapwa sana baba yake, ilimbidi arudi kwake. Alipofika kwake alimkuta bado mumewe Mrisho hakuwa nyumbani. Hapo kwa sababu ya shida nyingi alizozipitia aliamua kujitia kitanzi. Mumewe alirejea kwake saa kumi na nusu alfajiri huku akiwa mlevi wa kupindukia. Alifikiri ya kwamba Subira anaendelea na shughuli zake. Mrisho alishtuka sana na kupoteza fahamu alipogundua ya kwamba maiti ya Subira ilikuwa ikining’inia kwenye boriti. Hivyo, Subira alijiua kwa sababu ya kuteswa na mumewe na hata baba yake anamsaidia mumewe kumtesa. Msuko wa hadithi hii ni sahili kwa sababu tunasimuliwa matukio kwa njia ya moja kwa moja.

### 4.2.4.Mwanzo wa Kidrama

Drama inayozungumziwa hapa ni ile inayozushwa na swali linalomjia msomaji akili: Je, mhusika anayehusika atafanikiwa katika jambo analolifuata? Je, atakabiliana na vikwazo vyenyewe kwa jinsi gani? Ipo drama ambayo inalenga kwenye mgogoro wa hadithi fupi na ile inayoibuliwa katika akili ya msomaji na mgogoro huo (Wamitila, 2008).

Katika hadithi ya 'Mwungwana' mwanzo wa Kidrama unajitokeza:

> Saa nane za usiku.
> Ko, ko,. ko …. "Hodi," sauti nzito ya kiume ilibisha hodi.
> Kimya … Hakukutoka jibu lolote nyumbani mwa Bwana Haji.
> Si kama mlikuwa hamna mtu, bali hali ya mambo haikuruhusu.
> Ilisadifu kwamba, kwa wakati huu,
> Kibwana alikuwa kamkumbatia Saada, mke wa Bwana Haji.
> Kusikia sauti ya mngurumo wa kiume ikipiga hodi,
> Kibwana aliruka kitandani na kutua katikati ya chumba;
> Kanga kiunoni. (uk. 138).

Hadithi hii inahusu Bwana Haji na mkewe Saada. Saada ni mzinifu. Hii ni kwa sababu tunaelezwa kuwa hapo zamani Bwana Haji alikuwa amesikia nong'ono za mkewe za uhaini na vitendo viovu. Bwana Haji alizungumza na nafsi yake na kuapa iwapo atamfumania Saada huo ndio utakuwa mwisho wake kwa sababu atampa talaka. Anasema atampatika vile alivyommeza. Katika mwanzo huu tunaona Bwana Haji anarudi nyumbani usiku wa manane. Alipobisha mlango hakuna aliyekuwa tayari kufungua mlango kwa sababu Saada na Kibwana walikuwa wakifanya mapenzi. Mlango ulipobishwa Saada na Kibwana walishtuka sana kwa sababu walisikia sauti wa mngurumo ya kiume. Kibwana anaruka kitandani na kutua katikati ya chumba akiwa na kanga kiunoni. Saada anamtia moyo na kumwambia kuwa ile si sauti ya mumewe na hakuna chochote kingevunja starehe yao. Hii ni kumaanisha ya kwamba Saada alimpemda Kibwana na hivyo mapenzi nje ya ndoa.

Bwana Haji alipogundua hatafunguliwa mlango aliiga sauti ya rafiki yake Farija na mwishowe Saada akafungua mlango akifikiri ni rafiki yao Farija. Bwana Haji aliwafumania Saada na Kibwana wakifanya mapenzi. Bwana Haji alikuwa amerejea nyumbani usiku wa manane ili amfumanie mkewe. Alijifanya kuwa ameenda pwani lakini akarudi kimakusudi ili ajue tabia za mkewe. Baada ya kumfumania Saada na

Kibwana, Bwana Haji alijifanya mwungwana na hakumuuliza wala kumchapa Saada na mume mwenziwe Kibwana.

### 4.2.5.Mwanzo wa Kiishara

Hadithi fupi hutegemea mbinu ambazo zinamwezesha mtunzi wa hadithi fupi inayohusika kutumia mbinu za kujieleza kimkato. Mojawapo wa mbinu hizi ni ishara. Mwanzo wa aina hii basi huwa na ishara au sitiari. Sitiara inaweza kuwa ishara ambayo huwa na jukumu la kubeba maana au dhamira kuu ya hadithi fupi inayohusika (Wamitila 2008). Mwanzo wa aina hii unaonekana katika hadithi fupi ya ‘Mhanga wa Mwanamaua’ ambayo inaanza hivi:

> Na iwe vyovyote vile, jina la Mwanamaua limemsibu!
> Kule kisiwani pemba, binti akipewa jina hilo anapozaliwa,
> huwa amepewa jina la kinga, maana hukabidhiwa
> pepo mashuhuri- mzuka wa wazuka, shetani wa mashetani
> na mkuu wa vilinge, amlinde kijakazi na ubaya na husuda
> za ulimwengu. Utasikia wazee wa mtoto wakiahidi, “Bimkubwa,”
> (yaani huyo pepo au shetani). “Wewe si mdogo wa kutoelewa
> ulimwengu uliojaa ubaya. Tunakupa amani hii,”
> (yaani huyo mtoto wao wa kike), “amana llahu wa amana
> Rasulu, utuhifadhie na shari ya mahasidi, na sisi twaijua
> tunza yako.” (uk. 76).

Hadithi hii inahusu wachumba wawili Mwanamaua na Dadi. Mwanzo huu unatueleza kuwa Mwanamaua ana ushetani katika nafsi yake. Ushetani wake wa dhahiri umo katika nguvu za ndani zinazomsukuma mtu kufanya kitu na ukaidi wake. Tangu utotoni wa Mwanamaua alikuwa akishikilia kashikilia. Tunaeleza kuwa hakubali wala hatulii mpaka afanikiwe au labda patolewe Mhanga au chano.

Hadithi hii inatufichulia kwamba Mwanamaua na Dadi walikuwa wamebakisha siku saba ili wafunge ndoa. Hivyo, walikuwa na hamu kuu ya kufanya arusi kwa sababu walikuwa wanakutania msituni ili kufanya mapenzi. Wachumba hawa walikuwa wanapendana sana. Tunamwona Mwanamaua akitoka kwao usiku wa kiza na kwenda kumtafuta Dadi kwenye vichaka. Dadi anafurahia sana anapomwona Mwanamaua. Mwanamaua anamweleza Dadi kwamba kuna mambo yanayomsumbua. Jambo moja ni kwamba Dadi ni mwoga na Mwanamaua akamshawishi apigane na Ng’ombe Kipelele. Dadi anachelea

kwa sababu anaona jambo ili likiwa ngumu kwake, lakini kwa sababu ya mapenzi yake na Mwanamaua akakubali kupigana na Ng'ombe Kipelele.

### 4.2.6.Mwanzo wa Kimgogoro/ Kipeo

Ipo kauli ambayo hutolewa na wahakiki wa hadithi fupi kuwa hadithi fupi haina utangulizi. Mgogoro unaopatikana katika hadithi fupi unatangulizwa au kusimuliwa karibu na upeo wake. Huu ndio msingi wa kueleza mwanzo huu kama mwanzo wa kipeo. Hivyo, hadithi fupi zote zinachukuliwa kama zinaanza karibu na au kwenye upeo, lakini zipo hadithi fupi ambazo zinaakisi upeo huo kwa njia dhahiri kabisa (Wamitila 2008).

Katika hadithi ya 'Njia fupi.' Mwanzo wa kipeo unadhihirika:

> Fumu sasa kajitupa sesa juu ya kitanda chake
> cha samadari. Kichwa chake kimelalia viganja vyake
> wazi juu ya mto. Macho juu! Alikuwa akijaribu kuiiba
> nadhari yake ikimbie humo chumbani, Yende nje,
> ikabuge, ikazurure, mpaka ifike itakapofika kwenye
> upeo wa mawazo. Lakini nadhari ng'o, haikutaka kubanduka!
> Na kiasi ikatae kubanduka, matakuro na purukushani za
> mkewe zilikuwa zimejaa chumba tele, nazo
> hazikuipa nafasi ile nafsi ya ndani ya mumewe itoke nje.
> Unafanya mchezo nini? Ukisikia Naima Mambo ndiye
> huyu. Ana mambo kushinda! Anaweza kukigonganisha
> kijiti kwa chuma navyo vikawaka moto na kugeuka jivu.
> Na Mungu kampa uwezo huo! Kwa umbo mkamilifu.
> Kwa sura ungemwita malaika. Kwa mizungu kungwi
> wa makungwi au nyakanya manyakanya ukipenda.
> Lakini juu ya yote hayo Naima anampenda mumewe,
> ingawa anajua kwamba mume-mtu anamwendea kinyume
> yeye Naima. Na alipogundua ndipo alipouchonga
> ukali wake. Na leo ndio leo, asemaye kesho mwongo! (uk. 130).

Katika hadithi hii tumesimuliwa juu ya mume na mke. Fumu ni mumewe Naima Mambo. Mwanzo wa hadithi unaonyesha kuwa Fumu alikuwa akiwaza. Mawazo yake yalikuwa ni juu ya jinsi mkewe alivyokuwa akijikwatua na kushindwa kwa nini alikuwa akifanya hivyo. Mwanzo huu unatuonyesha kuwa Naima anapanga njia thabiti ya kumfumania mumewe Fumu aliyekuwa mzinzi na hatimaye anafaulu.

Naima anajifanya kuwa mmoja wa makahaba katika danguro alimoenda mumewe na kweli mumewe anamfumania huko. Hamtolei ukali mumewe bali anamshika mkewe na kumwambia warejee nyumbani. Tunaona ya kwamba Fumu ni mzinzi. Anaona ni vibaya

kumwacha mkewe mrembo na kukimbilia makahaba danguroni kwa Mama Kitimbi lakini anapuuza jambo hili.

Mwanzo wa hadithi hii unatuonyesha kuwa Naima anampenda mumewe na alikuwa mwaminifu kwake. Fumu hakuwa mwaminifu kwa Naima ndio maana siku moja aliamua kumfumania na kweli uzinzi wake ukajulikane na kuaibika. Naima alifikiri kwamba ulaghai wa mumewe ukijulikana ataiacha tabia zake mbaya na kuwa mwaminifu katika ndoa yake. Mwandishi anatuonyesha kuwa ndoa nyingi zimeathiriwa kwa sababu ya mapenzi nje ya ndoa. Makahaba katika danguro ya Mama Kitimbi wanaonyesha uozo wa jamii wa kuuza miili yao ili wapate mali.

### 4.3. Miisho na Utamatishaji wa Hadithi Fupi za Said A. Mohamed

Katika sehemu hii tumetathmini miisho na utamatishaji wa diwani za Said A. Mohamed. Mwisho wa hadithi fupi unachukua nafasi kubwa katika muundo mzima wa utanzu wenyewe (Wamitila 2002). Hadithi fupi hizi zinaonyesha miisho na utamatishaji wa aina mbali mbali kama tutakavyoonyesha katika visehemu vinavyofuata:

#### 4.3.1.Mwisho wa Kikwelikinzani

Kwelikinzani ni mbinu ya kifasihi ambapo kauli au hali inaonyesha mkinzano au ukinzani fulani kijuujuu lakini ina maana au ukweli fulani katika undani wake. Katika hadithi fupi ya ‘Sadiki Ukipenda’ kwelikinzani katika muktadha wa hadithi hii, kinachotokea katika sehemu ya mwisho kinaakisi mgongano fulani wa kimaana kijuujuu ingawa katika undani wake una maana. Hadithi ya ‘Sadiki Ukipenda’ inamalizika hivi:

> Na kwa hayo msinilaumu. Nakwambieni roho tamu; na penye ukatili wa kulana roho, msione ajabu mtu kutetea roho yake. Kisa Mkasa! Zaidi nina furaha kubwa. Hapo nilipo, nimo melini nikisafiri kuona ulimwengu mwingine. Wangu umenishinda kwa muda. Ningependa kurudi pale nitakapokuwa mtu kamili nitakayekuwa huru mimi na roho yangu. Nitakapoweza kusema hii ni nchi aliyoniachia baba’angu aliyejaribu kuniua. Na si kuwa peke yangu niliyekuwa na mori huo – nilipoingia melini niligundua vijana wengi kama mimi wamo humo. Wengine hata hawajui wanaelekea wapi, lakini wanajua wanakotoka. Na wala hawajuti kwa nini wameondoka kwao, ingawa hawana uhakika na wanakokwenda. Sijui kunatokezea nini katika

> dunia hii? Na wengine walinihadithia kwamba wenzetu wengi wako nje wameshatangulia. Wengine wameshaukata. Wengine wanahangaika na kubuga na njia. Heri ya hayo wanasema. Huzuni yangu kubwa ilikuwa tu kumwacha mtu kama Mzee Siwa – mtu adimu, au unasemaje? Lakini Mzee Siwa anaweza kuyamudu maisha ya pahali popote: hata motoni! Aliniambia hivyo, na akataka n'ende na dunia yangu! Ati siku zake zimekwisha na zangu ndio kwanza zinaanza! (uk.10).

Hadithi hii inahusu kijana Mussa. Mussa ni msimulizi wa hadithi hii na anasema asilaumiwe. Hii ni kwa sababu aliua baba yake akijaribu kujiokoa kutokana na ukatili wa baba yake ambaye alipanga kumua pamoja na wachawi wengine. Jamii ya mwandishi inaamini sana mambo ya urogi. Mzee Siwa anatumia maarifa yake ya mazingaombwe na kumwambia ya kwamba baba yake ni mchawi na amepanga pamoja na wachawi wengine kumuua kwa sababu yeye ni msomi.

Mussa anapitia changamoto nyingi, kwa sababu anasema kila mara alikuwa mbioni. Kila alipokumbwa na shida nyingi alikuwa akimwendea Mzee Siwa. Mzee Siwa alikuwa akimshauri pamoja na vijana wenzake. Baada ya kuepuka kifo alichopangiwa na baba yake mzazi na wachawi wengine, anasikia yu huru. Anasafiri kwa meli na kwenda nchi nyingine anakutana na vijana wengine huko. Anasema ya kwamba vijana hao walikuwa wametoroka kwenda nchi nyingine kwa sababu ya shida zinazowakumba. Mussa anasema wengine hata hawakuju walikokwenda. Tunaambiwa wengine wameshatangulia na wengine wametorokea nchi nyingine ili kuepuka umaskini. Tunaelezwa na mwandishi kuwa nchi ya msimulizi haikuwapa vijana nafasi ya kujiendeleza kimasomo. Hii ni kwa sababu wachawi walikuwa wanaroga vijana na hasa wasomi. Hivyo, vijana waliamua kutorokea nchi nyingine kuogopea usalama wao. Pia hali ya umaskini iliwafanya vijana kutafuta riziki mahali kwingineko.

Mzee Siwa alikuwa akishauri Mussa kwamba aende na dunia yake. Hii ni kwa sababu maisha yake ndio kwanza yalikuwa yanaanza. Kauli hii inatueleza ya kwamba vijana ni tegemeo la sika za usoni. Anasema wazee siku zao zimekwisha. Hii ni kumaanisha ya kwamba wazee wanapozeeka huwa wanategemea vijana kwa sababu vijana wana nguvu.

Jamii ya mwandishi haikuwa inathamini elimu. Hii ni kwa sababu warogi walikuwa wanawangaisha vijana kwa sababu tunaelezwa ya kwamba wengine wanahangaika na kubuga na njia. Hivyo, vijana waliteseka na kuamua kuhamia nchi nyingine mbali na kwao ili kutafuta riziki yao na pia kutafuta mahali pazuri pa kuishi mbali na warogi.

### 4.3.2Mwisho wa Kidhamira/ Kimotifu

Katika hadithi fupi ya ‘Ngondo Pangoni’ kuna mwisho wa kidhamira au kimotifu. Hadithi hii inaisha kwa kutaja kichwa cha hadithi. Ishara inayofumbatwa na anwani yenyewe ni muhimu katika kujenga hisia za hadithi na kukikweza kinaya cha Kondo kumkaribisha Jecha wakiwa na mkewe Mwamboje kule pangoni. Mwisho wa hadithi ya ‘Ngondo Pangoni’ unakuwa hivi:

> “Na huyu hapa Bi. Sihaba, Mkeo …. Karibu, karibu pangoni
> Bwana Jecha. Wewe na Bi. Mwamboje na mimi na Bi. Sihaba ….
> wake na waume wazuri au sivyo? … karibuni.”
> Ikawa ngondo pangoni! (uk.25).

Hadithi hii inahusu marafiki wawili Jecha na Kondo. Marafiki hawa walikuwa wazinzi. Kondo alikuwa akifanya mapenzi na mkewe Jecha na Jecha alikuwa akifanya mapenzi na mkewe Kondo. Marafiki hawa ni wanafiki kwa sababu wanapanga kukutania mahali pa siri huko pangoni.

Kondo na Bi. Sihaba wanatangulia kwanza pangoni. Baada ya muda mfupi jozi nyingine ya wapenzi iliwasili penye mlango wa pango. Marafiki hawa walipokutana wote pangoni ikiwa kinaya cha Kondo kuwakaribisha wote pangoni. Pia Kondo anawaita wake na waume wazuri. Hivyo kuonyesha unafiki. Marafiki hawa pamoja na wake zao wakafumaniana peupe pale pangoni. Ikawa ngondo pangoni. Hivyo, ufaafu wa anwani kuwa kasheshe ilitokea pale pangoni. Siri yao kubwa hatimaye ikajulikana.

### 4.3.3. Mwisho wa Kiasilia au Kikawaida

Mwisho wa Kiasilia au Kikawaida unajitokeza katika hadithi fupi ya ‘Uhuru wa Subira. Mwisho huu unafuata sifa ambazo zinaweza kuelezwa kama za kawaida. Sifa za aina hii zinaweza kuwa kama usingizi, kurejea, kuhisi kuwa umefikia hatima yako, mwisho wa sherehe au tukio, au kifo. Hatima ya maisha ya binadamu ni kifo. Hii ndiyo maana miisho ya aina hii inaelezwa kama ya kawaida. Kifo kinatumiwa katika hadithi fupi hii kama njia

ya kuufumbua msuko wa kazi yenyewe. Katika hadithi fupi ya 'Uhuru wa Subira' kunamwisho wa kifo.

Hadithi hii inamalizika ifuatavyo:

> Alitoa kibiriti na kuwasha taa ya kibatali
> iliyokuwepo juu ya kibao. Jicho chini aliangaza
> chumba chote. Chumba kidogo kama hicho
> dakika moja ilitosha kumhakikishia kuwa Subira
> hakuwemo chumbani humo. Alikuwa kesha
> geuka kutaka kutoka nje, ndipo alipotupa jicho
> juu, na pale darini … Alipata mshituko Mrisho.
> Maiti ya Subira ilikuwa ikining'inia kwenye boriti
> ya dari isiyotandikwa. Kanga ndiyo iliyotoa roho
> yake. Mrisho ulevi ulimruka. Mwili ulimnyongonyea
> na miguu ikakataa kushika, akaporomoka.
> Hakujijua tena. (uk.97).

Hadithi fupi hii inaisha kwa kifo cha Subira. Subira alikuwa ameteswa sana na mumewe Mrisho huku akisaidiwa na baba yake Mzee Farijala. Subira alikuwa akirejea kwao akitaka waachane na Mrisho kwa sababu Mrisho alikuwa mlevi wa kupindukia na alikuwa anamtesa sana. Kila alipoenda kwao kudai uhuru wake, alikuwa akichapwa na baba yake. Tunaelezwa ya kwamba siku moja alipochapwa na baba yake alienda nyumbani kwake huku akihisi kulemewa na maisha ya ndoa. Hii ni kwa sababu anasema amerejea tena katika jela la ndoa. Kulingana na Subira ndoa ni jela kwa sababu ya madhila na mateso anayopata kwa mumewe Mrisho.

Mwisho huu ni wa moja kwa moja kwa sababu tunaelezwa ya kwamba, baada ya Mrisho kufika kwake saa kumi na nusu alfajiri, alikuta mlango wa nyumba yake umefunguliwa na kujua ya kwamba Subira alikuwa amerudi. Alimwita kwa sauti ya kilevi lakini hakusikia sauti yoyote. Aliwakisha taa ili apate kumtafuta Subira chumbani mwake.

### 4.3.4 Mwisho wa Kitatuzi

Huu ni mwisho ambao unatatua tatizo kuu la msuko wa hadithi fupi yenyewe. Utatuzi huu unahusisha kuchunguza kama mgogoro uliopatikana mwanzoni mwa hadithi, na unaotawala katika hadithi fupi yenyewe, umesuluhishwa. Je, ni nani ambaye amefanikiwa katika nini? Mwisho wa kitatuzi umejitokeza katika hadithi fupi ya 'Mwungwana'. Hadithi hii inamalizika ifuatavyo:

> "Ha," alicheka Haji, kicheko kifupi cha

> mkato, kicheko kilichopenya na kumuuma
> yeye mwenyewe Haji seuze Bwana Ali na Bi.
> Sikitu. "Mzee," aliendelea," samahani,
> lakini ubaya na uzuri wa Mwungwana ni
> kwamba hatapiki nyongo akarudi
> akaramba." (uk. 144).

Hadithi fupi hii ya 'Mwungwana' inaonyesha kusuluhishwa kwa mgogoro uliojitokeza hapo mwanzoni. Mgogoro ulijitokeza pale ambapo Bwana Haji alijifanya ameenda pwani lakini akarejea kwake usiku wa manane. Alikuwa amesikia nong'ono za vitendo na uhaini wa mkewe Saada. Bwana Haji aliapa kwamba akimtia mikononi huo ndio utakuwa mwisho wake na Saada. Alisema na kujadili na moyo wake kwamba akimfumania Saada atamtema kama alivyommeza na kuapa hautamchagiza kuramba matapishi aliyokwisha yatapika. Hivyo, Bwana Haji alikuwa na msimamo mkali na akiamua jambo analitimiza.

### 4.3.5Mwisho wa Kitanakuzi/ Kilinganuzi

Tanakuzi ni mbinu ya kifasihi ambayo hujengwa kwa matumizi ya vinyume. Mwisho wa aina hii basi huwa ni aina ya kinyume cha mwanzo au utangulizi wa hadithi fupi inayohusika. Hadithi fupi inayoanza kwa 'furaha' inaweza kuishwa kwa 'huzuni'. Huu utakuwa mfano wa mwisho wa kitanakuzi, furaha inachukuliwa kama kinyume cha huzuni. Katika hadithi fupi ya Mhanga wa Mwanamaua, mwisho huu unajitokeza ifuatavyo:

> Kwa nukta chache uwanja ulikuwa baridi.
> Kimya kama kaburini. Na katika ukimya
> huo ukwenzi mkali wa mwanamke ulipasua.
> Hicho kilikuwa kilio cha Mwanamaua
> akijua kwamba Dadi amemtoa mhanga wakati
> alipomhitaji. (uk. 85).

Katika hadithi fupi hii, tunaelezwa ya kwamba hapo mbeleni Mwanamaua alikuwa na furaha kwa sababu zilikuwa zimebakia siku saba ndio wafanye arusi yeye na mchumba wake Dadi. Wachumba hawa walikuwa wanapendana kwa sababu wanatafutana usiku na kufanya mapenzi kwenye msitu huku wakijificha wasionekane. Hivyo, walikuwa na furaha kujua ya kwamba zilibakia siku saba tu ndio shida ya kukutana vichakani iishe.

Kulikuwa na matumaini ya kufanya arusi kwa sababu kila kitu kilikuwa tayari. Dadi anamweleza Mwanamaua kwamba wazee wake wameshapokea fedha za mahari, siku ya arusi ilikuwa imeshatangazwa, matayarisho murua yalikuwa yameshafanywa na walioalikwa walikuwa wameshaalikwa. Hivyo, mipango ya arusi ilikuwa imeshakamilika na familia za pande zote mbili walikuwa wanatarajia arusi ya Mwanamaua na Dadi.

Mwisho wa hadithi hii unatuonyesha kinyume cha jambo lililotarajiwa. Jambo hili ni badala ya arusi ikawa mazishi ya Dadi.

### 4.3.6.Mwisho wa Kiadili

Adili ni funzo ambalo hutokana na kisa, ngano, hadithi au simulizi yoyote. Hadithi fupi imepata chocheo lake kuu kutokana na simulizi za kijadi kama ngano. Sifa mojawapo ya ngano za kifasihi ni kuwepo kwa adili au maadili yanayobainika waziwazi kwenye sehemu ya mwisho ya ngano inayohusika. Mwisho wa adili huakisi au huelekeza kwenye adili inayotawala katika hadithi fupi inayohusika. Mwisho wa adili ni aina ya mwisho wa kifomula lakini miisho ya kifomula hutambulishwa zaidi vishazi au maneno fulani maalum.

Mwisho wa mada ni ule ambao unaakisi mada ya hadithi fupi. Zipo hadithi fupi ambazo zinaisha kwa kukaririwa kwa mada kuu kama tunavyoona katika hadithi fupi ya 'Njia fupi'. Katika hadithi fupi hii, mada yenyewe inaashiria au kuelekeza kwenye adili. Tuangalie mfano ufuatao:

> "Twende zetu mume wangu," alimwambia,
> "njia ya mwongo fupi".
> Fumu alitamani ardhi ipasuke aingie! (uk. 136).

Mwisho wa mada 'Njia fupi', inaafiki tabia ya ulaghai na uasherati wa Fumu ambaye hatimaye anagunduliwa na mkewe. Fumu anamuacha mkewe mrembo Naima na kwenda danguro la Mama Kitimbi kutafuta makahaba. Naima anapogundua siri hii, anajikwatua kwelikweli na kujipeleka huko danguroni kama mmoja wa makahaba. Fumu anapokimbilia huko kutuliza joto lake la mwili, anamkuta huko. Njia ya uwongo wake ikawa fupi, mkewe anamfumania na kumwaibisha. Njia yake ni fupi. Mwisho huu unaasa kuwa, uwongo huwa haudumu.

## 4.4 Hitimisho

Katika sura hii, tumeangalia msuko kwa kumulika mianzo na vimalizio vya hadithi fupi kwa sababu sehemu hizi ni muhimu katika hadithi fupi. Umuhimu wa mianzo na vimalizio katika hadithi fupi hutokana na ukweli kwamba utanzu huu huhusisha mawanda finyu kwa hivyo mwandishi sharti, atumie ufundi maalum kukuza na kuendeleza sehemu hizi (Mbuthia 2005).

Tumesema ya kwamba mpangilio wa matukio wa hadithi fupi huwa sahili.Matukio pia hutiririka na kufululiza moja kwa moja toka mwanzo hadi mwisho. Hadithi fupi huwa na sifa za kimuundo ambazo zinaweza kuwa za uanzaji wa hadithi fupi na miisho na utamatishaji.Katika hadithi fupi za Said A. Mohamed, hadithi fupi hizi zinahusu mawanda finyu na kwa kawaida haitumii misuko ambayo ni changamano bali ni sahili. Mianzo na miisho hufanikisha uwasilishaji wa maudhui.

## SURA YA TANO

## MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 5.1Utangulizi

Katika sura hii tumeshughulikia matokeo ya utafiti wetu na mikakati tuliyotumia ili kufikia madhumuni yetu. Tulikusudia kuchunguza uwasilishaji wa maudhui katika hadithi fupi za Said A. Mohamed. Tumechunguza jinsi mandhari, wahusika na mianzo na vimalizio vinachangiana na kukamilishana ili kufanikisha uwasilishaji wa maudhui. Sehemu hii pia itaangazia mapengo zaidi ambayo yanafaa kushughulikiwa ili kufanikisha mahitaji ya wasomaji.

### 5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Tumegundua kuwa mwandishi ametumia mandhari mbalimbali katika kufanikisha uwashilishaji wa maudhui. Tumepata kuna mandhari ya mahali na mandhari ya wakati. Katika mandhari ya mahali, tumeangazia mandhari ya mashambani, nyumbani na pia ya danguroni. Katika mandhari ya mashambani tumeona ya kwamba maudhui mbalimbali yamewasilishwa kupitia mandhari haya. Kwa mfano maudhui ya ushirikina, ukatili na kutothamini elimu miongoni mwa mengine katika hadithi ya 'Sadiki Ukipenda' na maudhui ya unafiki, ndoa na mapenzi katika hadithi ya Ngondo Pangoni. Mandhari ya nyumbani yametuonyesha maudhui ya kudhalilishwa kwa mwanamke, ubabedume miongoni mwa mengine katika hadithi ya 'Uhuru wa Subira'. Katika hadithi ya 'Njia fupi' kuna maudhui ya usaliti katika ndoa na ukahaba. Tumeona kuna maudhui ya talaka na uungwana katika hadithi ya 'Mwungwana' vilevile mandhari ya danguroni yametufichulia maudhui ya mapenzi nje ya ndoa, ukahaba na tamaa ya pesa. Katika hadithi ya 'Njia fupi' Fumu anamwacha mkewe mrembo Naima na kukimbilia kwa danguro ya Mama Kitimbi kutafuta makahaba ili kutuliza joto lake la mwili.

Tumegundua pia ya kwamba mandhari ya wakati mbalimbali hufanikisha uwasilishaji wa maudhui. Kwa mfano kuna mandhari ya wakati wa asubuhi, mchana na usiku. Tumeona mandhari ya wakati wa usiku uwasilisha maudhui ya maovu. Kwa mfano katika hadithi ya 'Sadiki Ukipenda', baba yake Mussa na wachawi wengine wanafanya kazi yao ya kuroga watoto na vijana wakati wa usiku wa manane. Pia katika hadithi ya 'Mwungwana' Saada na Kibwana wanafumaniwa wakifanya mapenzi na Bwana Haji usiku wa manane.

Vilevile Katika hadithi ya 'Mhanga wa Mwanamaua' Mwanamaua na Dadi wanakutania msituni ili kufanya mapenzi huku wakijificha wasionekane. Katika hadithi ya 'Ngondo Pangoni' Kondo na Bi. Sihaba na Jecha na Bi. Mwamboja wanapanga kukutania pangoni ili wafanye mapenzi. Tunaona kisadfa marafiki hawa wanafumania peupe huko pangoni na kasheshe ikatokea. Utendakazi wa mandhari katika hadithi fupi za Said A. Mohamed umedhihirika kibayana kutokana na mandhari hayo tofauti ambayo yamefanikisha uwasilishaji wa maudhui.

Katika sura ya tatu, tumeangazia nafasi ya wahusika katika diwani zilizoteuliwa za Said. A. Mohamed. Utafiti wetu umepata kuwa mwandishi ametumia wahusika mbalimbali katika kufanikisha uwasilishaji wa maudhui. Hivyo, tumeona ya kwamba hadithi fupi huwa na idadi ndogo ya wahusika ambao pia uhusika wao si wa kina. Wahusika waliotumiwa ni wachache katika kila hadithi fupi. Pia wahusika hujifunga tu kwa tukio moja kuu. Tumechunguza wahusika wakuu na wahusika wadogo. Kila hadithi fupi tulipata wahusika wakuu wawili. Wahusika hawa ni wa maana na wanapatikana katika kazi hizi kutoka mwanzo hadi mwisho. Mchango wao ni muhimu katika kufanikisha uwasilishaji wa maudhui katika hadithi fupi ya 'Sadiki Ukipenda'. Wahusika wakuu ni Mussa na Mzee Siwa. Mussa ni msimulizi wa hadithi.

Katika hadithi ya 'Uhuru wa Subira' wahusika wakuu ni Subira na Mrisho. Subira anateswa sana na mumewe Mrisho huku wakisaidiana na baba yake Mzee Farijala. Subira anaonyesha kudhalilishwa kwa mwanamke kunakomsababishia kifo. Mrisho naye anawasilisha maudhui ya ulevi pale anatesa Subira sana huku akirejea nyumbani saa kumi na nusu alfajiri na kushindwa kutekeleza wajibu wake wa ndoa. Subira anaona kuolewa na kama kuwa katika jela. Hivyo, Subira alikuwa anataka uhuru wake kwa kutaka kuachana na Mrisho.

Katika hadithi fupi ya 'Mwungwana' Bwana Haji anamfumania mkewe Saada na Kibwana na kumpa talaka. Bwana Haji anakuwa mwungwana kweli kwa kukataa kurudiana na Saada baada ya kumfumania. Saada ni mzinzi ambaye alikuwa anamsaliti mumewe Bwana Haji kimapenzi. Wahusika hawa wanafanikisha uwasilishaji wa maudhui ya usaliti katika ndoa, uzinzi na uungwana.

Katika hadithi fupi ya ‘Mhanga wa Mwanamaua’ kuna wahusika wakuu Mwanamaua na Dadi. Mwanamaua na Dadi wamepanga kufanya arusi baada ya siku saba. Mwanamaua anamshawishi Dadi kupigana na ng’ombe Kipelele na mwishowe anauawa na Ngombe yule. Maudhui ya ushawishi yanadhihirika kwa sababu Dadi alijua kwamba kupigana na ng’ombe Kipelele kulikuwa hatari lakini kwa sababu ya mapenzi yake na Mwanamaua anakubali. Mhusika Mwanamaua anaonyesha ushetani ndani yake kwa sababu hangetulia mpaka aone ya kwamba lengo lake limetimia. Mwanamaua labda alitulia baada ya kumtoa Dadi kama kafara. Tumeona ya kwamba ushawishi wa mwanamke unaweza kumtia mwanamume mahali pabaya.

Katika hadithi ya ‘Njia fupi’ Fumu na Naima ni wahusika wakuu. Fumu ni mzinzi ambaye anatembelea danguro ya Mama Kitimbi kutafuta makahaba. Naima anapanga njia dhabiti ya kumfumania mumewe kule danguroni na kumwaibisha.

Tulipata kuwa kuna wahusika wadogo ambao waliwasaidia wahusika wakuu kuendeleza na kufanikisha uwasilishaji wa maudhui. Wahusika hawa pia ni muhimu lakini mchango wao sio mkubwa kama wa wahusika wakuu. Tumegundua kuwa hata ingawa hawana mchango mkubwa kuweko kwao ni muhimu. Kwa mfano baba yake Mussa anashirikiana na wachawi wengine kuroga vijana, na watoto. Hivyo, maudhui ya ushirikina na ukatili. Bi. Sihaba mkewe Jecha wanafanya mapenzi na Kondo ambaye ni mumewe Bi. Mwamboje. Wote wanafumaniana pangoni na tabia zao za uzinzi zinajulikana. Biti Shomari anamhurumia Bintiye Subira kwa kuteswa na mumewe. Bi. Shomari anamsaidia Subira kwa kuonyesha kudhalilishwa kwa mwanamke. Pia Mzee Farijala anamsaidia Mrisho kutesa Mkewe Subira.

Kibwana anafumaniwa na Bwana Haji wakifanya mapenzi na Saada. Hivyo, Kibwana anasaidia katika kumjenga Saada ambaye ni mzinzi. Ng’ombe Kipelele ni mhusika ambaye anaua Dadi katika mchezo wa ng’ombe huku Mwanamaua akiachwa na mchumba wake. Pia tumechunguza na kugundua ya kwamba Mama Kitimbi ambaye ni mmiliki wa ‘duka la laana’ ambako Fumu anatembelea na kuwa mteja wa duka lile. Makahaba wanakutana kwa Mama Kitimbi ili wauze miili yao na kujikimu. Mama Kitimbi na makahaba wanaonyesha uhalisia wa jamii, pale kuna mapenzi nje ya ndoa.

Katika sura ya nne, utafiti wetu umepata kuwa mwandishi ametumia mianzo na vimalizio vya hadithi fupi katika kufanikisha uwasilishaji wa maudhui. Mianzo na vimalizio ni mojawapo ya vipengele vya msuko. Tumegundua kuwa msuko wa hadithi fupi huwa sahili na si changamano. Matukio huwa yanatiririka na kufululiza moja kwa moja kutoka mwanzo hadi mwisho. Tumegundua msuko hufanikisha uwasilishaji wa maudhui kwa kumlika ufunguaji na ufungaji wa hadithi fupi.

Tumegundua katika ufunguaji wa hadithi fupi, mwandishi huwa anadhihirisha waziwazi funzo lake katika hadithi hiyo. Hadithi fupi huwa na mianzo tofautitofauti. Inaweza kuanza kwenye upeo, mwisho au ianze kama kawaida. Tumeona kuwa uanzaji wa hadithi fupi huwa na mchomo wa aina fulani kwa msomaji ambaye anavutwa na kunaswa na hadithi fupi hiyo.

Tumeona ya kwamba ikiwa mwandishi ameshindwa katika uanzaji wa hadithi fupi basi ameshindwa kama mwandishi. Said A. Mohamed ameonyesha ujuzi wake wa hali ya juu ya uanzaji wa hadithi fupi. Kwa mfano katika hadithi fupi ya ‘Sadiki Ukipenda’ ameonyesha uanzaji wa kitathmini. Mwandishi ametoa kauli ambaye ni ya kitathmini. Mussa anatoa kauli za kitathmini ambayo inajifunga kwenye ulimwengu wa hadithi, kumhusu mhusika katika ulimwengu wa hadithi hiyo. Mwanzo huu unaonyesha kuwa Mzee Siwa alikuwa na maarifa na sifa ambazo zilimfurahisha Mussa. Mzee Siwa anamfichulia Mussa kwamba baba yake ni mchawi na alikuwa amepanga pamoja na wachawi wengine kumroga kwa sababu ni msomi.

Katika hadithi ya ‘Ngondo Pangoni’ mwandishi ametumia mwanzo wa kirejeshi. Pale kuna kurejeshwa nyuma kiwakati. Mwanzo huu unaonyesha kuwa Jecha na Kondo walikuwa marafiki ambao walipenda umbea na uzinzi. Tabia zao zilikuwa zinafanana kwa kuwa walikuwa wazinzi na wanafiki. Katika hadithi fupi ya ‘Uhuru wa Subira’ kuna mwanzo wa kitaharuki. Mwanzo huu unamletea mhakiki maswali ya ‘Kwa nini’ ‘Mbona?’, ‘Kisha?’ na kadhalika. Tumeona Biti Shomari akiwaza na kusema kuwa yeye ni mtumwa na Binti yake Subira ni mtumwa. Hii ni kuonyesha kuwa wanawake walidhalilishwa na wanaume. Katika hadithi ya ‘Mwungwana’ mwanzo wa kidrama unajitokeza pale kuna maswali kama anayehusika atafanikiwa katika jambo analolifuata. Bwana Haji anarejea kwake nyumbani usiku wa manane na kugonga mlango. Saada na

Kibwana wanafumaniwa wakifanya mapenzi. Tunaona Bwana Haji alifanikiwa kutekeleza wajibu wake pale alimpa talaka Saada kwa kuonyesha uungwana wa hali ya juu.

Katika hadithi ya 'Mhanga wa Mwanamaua' mwanzo wa kipenyezi unajitokeza. Mwandishi anaonyesha kwa jina la Mwanamaua lilikuwa na ushetani ndani yake. Aliweza kumshawishi Dadi apigane na Ng'ombe Kipelele na akahakikisha ya kwamba Dadi amepigana na Ng'ombe hatari na mwishowe kuuawa. Dadi alitolewa na Mwanamaua kama kafara. Katika hadithi 'Njia fupi' kuna mwanzo wa kimgogoro. Mgogoro unapatikana karibu na upeo wake kwa sababu Fumu anafikiria juu ya mkewe Naima jinsi alivyojikwatua. Naima alikuwa anapanga njia dhabiti ya kumfumania mumewe Fumu ambaye alikuwa anaenda kwa makahaba danguroni kwa Mama Kitimbi. Naima anajifanya mmoja wa makahaba na kumfumania Fumu huko. Fumu anaaibika uzinzi wake unapojulikana.

Tumegundua ya kwamba mwisho wa hadithi fupi huwa na mkokotezo na msisitizo fulani. Msisitizo mkubwa huwekwa kwenye jinsi hadithi itakavyokwisha. Ikiwa mhakiki ana haja ya kujua ni kitu gani kitakachotendeka, ni lazima atamani kuona mwisho wa hadithi fupi. Tumegundua kuna miisho na utamatishaji tofautitofauti katika hadithi fupi za Said A. Mohamed. Kwa mfano katika hadithi fupi ya 'Sadiki Ukipenda' kuna mwisho wa kikwelikinzani. Mussa anasema asilaumiwe kwa kutetea roho yake. Hii ni kwa sababu Mussa alimuua baba yake baada ya kuambiwa na Mzee Siwa kwamba baba yake ni mchawi na kumpangia jinsi ya kukabiliana na baba yake. Mussa anamuua baba yake na kuachiwa uhuru wake wa kuishi.

Katika hadithi ya 'Ngondo Pangoni' kuna mwisho wa kidhamira. Hadithi hii inaisha kwa kutaja kichwa cha hadithi. Kondo na Jecha ni marafiki lakini wana tabia ya uzinzi. Jecha anafanya urafiki wa mapenzi na Bi. Mwamboje mkewe Kondo. Vilevile Kondo anapanga kufanya mapenzi na Bi. Sihaba mkewe Jecha. Wote walipanga kukutania pangoni ili kufanya mapenzi na kwa sadfa wote wanafumaniana huko. Tumeona mwisho huu kuna kasheshe kwa sababu tabia zao zinajulikana.

Katika hadithi fupi ya 'Uhuru wa Subira' tumeona mwisho wa kiasilia au kikawaida pale kunatokea kifo cha Subira. Mrisho anashtuka sana na kupoteza fahamu alipogundua ya kwamba ni yeye aliyesababisha kifo cha mkewe kwa kumdhalilisha na kuwa mlevi wa kupindukia. Katika hadithi ya 'Mwungwana' kuna mwisho wa kitatuzi pale Bwana Haji alijifanya Mwungwana na kumpa Saada talaka baada ya kumfumania na Kibwana wakifanya mapenzi. Katika hadithi ya 'Mhanga wa Mwanamaua' kuna mwisho wa kitanakuzi pale tunamwona Mwanamaua na Dadi wakiwa na furaha kwa sababu zilibakia siku saba ili wafunge ndoa, lakini inatokea kinyume wakati Dadi aliuawa na Ng'ombe Kipelele na badala ya arusi ikawa mazishi ya Dadi. Mwanamaua anahuzunika sana alipogundua ameachwa na mchumba wake. Katika hadithi ya 'Njia fupi' kuna mwisho wa adili. Tumegundua kuwa 'Njia fupi' inaafiki tabia ya ulaghai na uasherati wa Fumu ambaye hatimaye anagunduliwa na mkewe. Adili ya hadithi hii inaasa kuwa uwongo huwa haudumu.

### 5.3 Hitimisho

Katika hadithi fupi zilizoteuliwa za Said A. Mohamed ametumia vipengele vya fani kwa ufundi wa hali ya juu. Ujumbe aliokusudia kuuwasilisha umewasilishwa kwa njia inayoeleweka na kwa urahisi. Kupitia kwa vipengele vya fani, ujumbe wake unavutia na kumpatia msomaji ari ya kusoma. Vipengele vyenyewe ni kama vile mandhari. Mandhari ni mojawapo wa vipengele vilivyotumiwa kwa ufundi wa hali ya juu katika diwani teule za Said A. Mohamed. Mwandishi ametumia wahusika kuupitisha ujumbe wake. Baadhi ya wahusika hawa ni wakuu na wadogo. Wahusika wakuu wa hadithi fupi huwa bapa kwa kuwa utanzu huu hauwapatii nafasi ya kukua. Wahusika wadogo katika utanzi huu huwa wachache na hawakuzwi. Hatimaye tumeshughulikia mianzo na vimalizio vya hadithi fupi na kugundua umuhimu wa mianzo na vimalizio vya hadithi fupi katika kufanikisha uwasilishaji wa maudhui.

### 5.4 Mapendekezo

Utafiti huu umejikita katika vipengele vya fani ambavyo ni mandhari, wahusika na mianzo na vimalizio. Kuna haja ya wahakiki wa baadaye kushughulikia vipengele vya fani ambavyo hatujashughulikia kama vile:  usimulizi na matumizi ya lugha katika kufanikisha uwasilishaji wa maudhui katika hadithi fupi za Said A. Mohamed. Pia

tungependekeza wahakiki wa baadaye wahakiki maudhui katika diwani za Said A. Mohamed na kulinganisha na kazi za waandishi wengine kama vile Ken Walibora.

Sisi tumetumia Nadharia ya Umuundo. Tungependekeza wahakiki wa baadaye watumie nadharia nyingine kama vile ya Urasimu wa Kirusi, au nyingine mwafaka. Watafiti wakishughulikia maswala haya bila shaka watachangia katika ukuaji wa fasihi ya Kiswahili hasa utanzu wa hadithi fupi.

# MAREJELEO

Buchbinder, D. (1991). *Contemporary Literary Theory and The Reading of Poetry*. Moray: Macmillan Education Australia PTY Ltd.

Culler, J.D. (1975). *Structuralist Poetics*. London: Routledge and Kegan.

Fokkema, I. (1978). *Theory of Literature in the Twentieth Century.* London: Hurst and Co. Ltd.

Forster, E.M. (1927). *Aspects of the Novel.* London: Penguin Publisher.

Iribemwangi, P.1 na Babusa, H. (2017).*Vazi la Mhudumu na Hadithi Nyingine.* Nairobi: East African Education Publishers Ltd.

Kanyua,G.M. (2013). "Mtindo Unavyoendeleza Maudhui katika Natala". Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Kang'eri, S. N. (2017). "Uchunguzi wa Vipengele Teule vya Fani katika Riwaya ya Mashetani wa Alepo". Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Kasilu, P.N. (2003). "Mwingiliano wa Fani na Maudhui katika Ushairi wa Kithaka wa Mberia". Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Katutu, R.M. (2013). "Mtindo katika Diwani ya Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine". Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Magare, F.A; (2002). "Uhakiki wa Tamthilia ya 'Amezidi' Kama kazi ya Kiubwege". Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Mbatiah, M. (2000). *Mwendawazimu na Hadithi Nyingine.* Nairobi: Phoenix Publishers.

__________ (2002). *Kamusi ya Fasihi.* Nairobi: Standard Textbooks.

Mbuthia, E.M. (2005). "A Stylistic and Thematic Analysis of Kiswahili Short Stories". Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Mlacha, S. A. K & Madumulla, J. S. (1991). *Riwaya ya Kiswahili.* Dar-es-salaam: Dar-es-salaam University Press.

Mohamed, S.A. (2002). *Sadiki Ukipenda na Hadithi Nyingine*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation Publishers Ltd.

_________ (2005). *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine.* Nairobi: Longhorn Publishers Ltd.

__________ (2005). *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation Ltd.

Mohochi, E. (1995). *Fani katika hadithi fupi za Kiswahili.* Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Egerton. (Haijachapishwa).

Msokile, M. (1993). *Msingi wa Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: East African Educational Publishers.

Mugenda, O. M. & Mugenda, A. G. (1999). *Research Methods: Quantitative and Qualitative Approaches.* Nairobi: African Centre for Technology Studies Publishers Limited.

Muiruri, S.N. (2016). "Maudhui yanavyoimarishwa na Fani katika Riwaya ya Nguvu ya Sala". Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Murage, J.N. (2011). "Uhakiki wa Fani katika Utendi wa Mwana Ninga". Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Musyoka, F.M. (1996). "Uhakiki wa Fani katika Tamthilia za Jay Kitsao". Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Mwanzi, H.O. (1995). "The Style of the Short Story in Kenya: An analysis of the Short Stories of Ngugi wa Thiong'o, Leonard Kibera and Grace Ogoti". Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Mwilaria, R. (2011). "Fani katika Utenzi wa Ayubu". Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Ndung'u, N. (1996). “Uhakiki wa Fani katika Riwaya za Katama Mkangi”. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Ongarora, S. (2007). “Mtindo katika Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine”. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Saussure, F. de (1966). *Course in General Linguistics.* Wade Baskin (mtafsiri). New York: McGraw Hill.

Scholes, R. (1974). *Structuralism in Literature.* New Haven: Yale University Press.

Senkoro, F. E. M. K. (1982). *Fasihi.* Dar-es-salaam: Press and Publicity Centre.

Tambasi, P. (2011). *Uhakiki wa Fani katika Tambuka.* Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Wafula, R. M. na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi, Misingi na Vipengele vyake.* Nairobi: Phoenix Publishers.

________ (2008). *Kanzi ya Fasihi 1: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi.* Nairobi: Vide-Muwa Publishers Limited.

________ (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia.* Nairobi: Focus Publication Ltd.

Were, E. (2012). “Jinsi Vipengele vya Fani: Ploti, Wahusika, Dayolojia na Monolojia vinavyohusiana na kufanikisha Ujenzi wa Tamthilia za *Kilio cha Haki na Kijiba cha Moyo*”. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Wesa, W. (2005). “Uhakiki na Uchambuzi wa Kifani katika Utenzi wa Mwana Fatuma na Siri Li Asirali”. M.A Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).